BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KIDATO CHA SITA, 2019

# 121 KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE), 2019

# 121 KISWAHILI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI……………………………………………………………………………………
……..iv
1.0 UTANGULIZI ..................................................................................... 1
2.0 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA ............................... 2
2.1 TATHMINI KWA KILA SWALI................................................................ 2
2.2 SEHEMU A:UFAHAMU......................................................................... 2
2.2.1 Swali la 1: Ufahamu ......................................................................... 2
2.2.2 Swali la 2: Ufupisho ......................................................................... 6
SEHEMU B: MATUMIZI YA SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA ................. 10
2.2.4 Swali la 3: Utumizi wa Lugha. .......................................................... 10
2.2.5: Swali la 4: Matumizi ya Sarufi ......................................................... 15
2.2.6 Swali la 5: Matumizi ya Sarufi. ......................................................... 20
2.2.6 Swali la 6: Matumizi ya Sarufi. ......................................................... 28
2.3. SEHEMU C: UTUNGAJI ..................................................................... 32
2.3.1 Swali la 7: Utungaji ......................................................................... 32
2.4. SEHEMU D: MAENDELEO YA KISWAHILI ............................................ 40
2.4.1 Swali la 8: Maendeleo ya Kiswahili. ................................................... 41
2.4.2 Swali la 9: Maendeleo ya Kiswahili ................................................... 49
2.5: SEHEMU E: TAFSIRI NA UKALIMANI ................................................. 58
2.5.1: Swali la 10: Tafsiri na Ukalimani. ..................................................... 58
3.0 SEHEMU YA II: MTIHANI WA KISWAHILI KARATASI YA PILI. ............. 65
3.1 TATHMINI KWA KILA SWALI ............................................................. 65
3.2 SEHEMU A: FASIHI KWA UJUMLA ....................................................... 65
3.2.1 Swali la 1: Nadharia ya Fasihi. ......................................................... 65
3.2.2 Swali la 2: Fasihi kwa Ujumla. .......................................................... 75
3.3 SEHEMU B: USHAIRI.......................................................................... 84
3.3.1 Swali la 3: Uhakiki wa Ushairi. ......................................................... 84
3.3.2 Swali la 4: Uhakiki wa Ushairi .......................................................... 92
3.4 SEHEMU C: RIWAYA ......................................................................... 102
3.4.1 Swali la 5: Uhakiki wa Riwaya.......................................................... 102
3.4.2 Swali la 6: Uhakiki wa Riwaya.......................................................... 117
3.5 SEHEMU D: TAMTHILIYA ................................................................... 129
3.5.1 Swali la 7: Uhakiki wa Tamthiliya. .................................................... 129
3.5.2 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya ..................................................... 138
3.6 SEHEMU E: USANIFU WA MAANDISHI ............................................... 149
3.6.1 Swali la 9: Usanifu wa Maandishi ..................................................... 149
HITIMISHO............................................................................................ 161
MAONI NA MAPENDEKEZO ..................................................................... 163
Kiambatisho A ........................................................................................ 165
KIAMBATISHO B......………………………………………………………166

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa kuhusu uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa Kidato cha Sita mwaka 2019 katika somo la Kiswahili. Taarifa hii inatoa mrejesho wa kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi, walimu, wazazi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho yenye lengo la kuonesha ni jinsi gani mfumo wa elimu nchini umefanikiwa kutoa elimu kwa ujumla hususan katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Aidha, majibu ya watahiniwa katika mtihani huu yanalenga kuonesha namna mfumo wa elimu ulivyoweza au ulivyoshindwa kuwapa maarifa watahiniwa wa kidato cha sita.

Taarifa hii imechambua sababu mbalimbali zilizochangia watahiniwa kujibu vizuri, wastani au vibaya maswali ya mtihani huu. Sababu za baadhi ya watahiniwa kutojibu maswali kwa usahihi ni pamoja na kushindwa kutambua matakwa ya swali na kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada mbalimbali katika somo la Kiswahili. Aidha, uchambuzi huu umeonesha sababu za watahiniwa kujibu maswali kwa usahihi kama vile: kutambua matakwa ya swali, kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa na kuzingatia kanuni na matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Pia, sababu za watahiniwa kupata alama za wastani zimebainishwa haswa katika kutoa majibu yasiyojitosheleza. Sababu hizi na nyinginezo zilizoainishwa katika taarifa hii zitawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa shule, walimu na wanafunzi kupata mbinu muafaka katika kuboresha kiwango cha kufaulu katika mitihani ijayo.

Mwisho, Baraza linapenda kuwashukuru maafisa mitihani, walimu wa somo na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii. Shukrani za pekee ziwaendee wafanyakazi wa Idara ya Utafiti, Tathmini na Huduma za Kompyuta walioshiriki katika uchambuzi wa data zilizotumika katika taarifa hii.

Dr. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Kiswahili kwa watahiniwa wa kidato cha sita ulifanyika Mei 2019. Mtihani huu ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili wa kidato cha V na VI. Mtihani huu ulikuwa na karatasi mbili (2) yaani 121/1 Kiswahili 1 na 121/2 Kiswahili 2.

Mtihani wa 121/1 kiswahili 1 uligawanywa katika sehemu A, B, C, D na E kwa kuzingatia mada za Ufahamu na Ufupisho, Utumizi wa Lugha, Matumizi ya Sarufi, Utungaji, Maendeleo ya Kiswahili na Tafsiri na Ukalimani. Kila sehemu ilikuwa na alama ishirini (20). Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali saba (7) kati ya maswali kumi (10). Sehemu A na B maswali mawili kwa kila sehemu; Sehemu C, D na E, swali moja kwa kila sehemu.

Mtihani wa 121/2 Kiswahili 2 uligawanyika katika sehemu A, B, C, D na E kwa kuzingatia mada za Fasihi kwa Ujumla, Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi na Usanifu wa Maandishi. Kila sehemu ilikuwa na alama ishirini (20) na mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja tu kwa kila sehemu, hivyo kutakiwa kujibu jumla ya maswali matano (5).

Jumla ya watahiniwa 21,783 ambapo wasichana walikuwa 11,132 na wavulana walikuwa 10,651 walifanya mtihani wa 121. Kiswahili Ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa 121 Kiswahili kwa mwaka 2019 ulikuwa wa kiwango cha asilimia 100 ambapo watahiniwa wote waliofanya mtihani huu walipata wastani wa alama 35. Ufaulu huu umegawanyika katika viwango vitatu ambavyo ni vizuri, Wastani na dhaifu. Kiwango kizuri cha kufaulu kinaanzia alama 60 hadi 100; kiwango cha wastani kinaanzia 35 hadi 59 na kiwango hafifu kinaanzia 0 hadi 34. Aidha, chati za viwango vya kufaulu kiasilimia zimeambatanishwa ili kufafanua kufaulu kwa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha kufaulu kwa kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha kufaulu kwa kiwango cha wastani na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu wa kiwango hafifu.

Taarifa hii imechambua maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na hafifu ili kukuza kiwango cha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Uchambuzi huu, unalenga kuonesha hali halisi ya jinsi watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani karatasi ya kwanza (121/1) na karatasi ya pili (121/2) ya somo la Kiswahili. Sampuli za majibu yao zimeambatanishwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na kilichofanywa na watahiniwa. Hivyo uchambuzi huu umeweka mpango mkakati wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa mada hizo na kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

## 2.0 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA

## 2.1 TATHMINI KWA KILA SWALI

## 2.2 SEHEMU A:UFAHAMU

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili yaliyotaka mtahiniwa kuonesha umahiri katika kusoma habari, kujibu maswali na kisha kufanya ufupisho.


### 2.2.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali lilihusu Ufahamu ambapo watahiniwa walipaswa kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yaliyofuata.

Swali lilitoka katika mada ya Ufahamu na lililenga kupima ufahamu wa mtahiniwa katika kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho. Swali hili liligawanyika katika vipengele (a) hadi (d) na lilikuwa na alama 10.


Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kuandika kichwa cha habari aliyosoma. Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa aeleze maana za maneno; (i) Muungwana (ii) Arifu (iii) Hajitwezi na (iv) Mwadilifu kama yalivyotumika katika kifungu cha habari. Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa aeleze mawazo makuu mawili ya mwandishi na kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa kutaja tabia tatu za mtu muungwana kutokana na habari.

Swali lilikuwa la lazima na lilijibiwa na watahiniwa 21774. Lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi. Asilimia 99 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani na zaidi kutokana na kutoa majibu sahihi katika vipengele vingi. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 1**: *Kufaulu kwa Watahiniwa Kiasilimia*

Asilimia 91.5 ya watahiniwa walipata alama za juu ambazo ni kuanzia 6 hadi 10. Hii inaonesha watahiniwa walikielewa vyema kifungu cha habari na kuweza kujibu vipengele vingi kwa usahihi. Miongoni mwao, asilimia 61.7 walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10 kwa kuweza kuandika kwa usahihi kichwa cha habari, kutoa maana za maneno kama yalivyotumika katika habari, kuelezea mawazo makuu mawili ya mwandishi na kutaja tabia tatu za mtu muungwana. Kielelezo 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kwa kujibu kwa usahihi vipengele (a), (c) na (d) na kutoa ufafanuzi usiojitosheleza katika kipengele (b) (ii) pekee.


1 a/ UUNGWANA WA MTU.

b/ i/ muungwana - ni mtu anayejiheshimu na kuwaheshimu watu wengine

ii/ Anifu - kamili

iii/ Hajitwezi - Hajipandishi

iv/ muaadilifu - muema

1:(c) Muandishi - ni mtu anayeandika kazi yeyote ile. Katika habari ya ~~AA~~ uungwana wa mtu yafuatayo ni mawazo makuu yaliyojitokeza.

Uadilifu - muandishi amezungumzia suala la uadilifu kwa kila mtu ambaye anahitaji kuwa muungwana lazima awe kuwa muadilifu kwa wenzake.

Uvumilivu - vile vile muandishi amezungumzia kuwa mtu yeyote hana budi kuwa na uvumilivu katika jamii yake ili awe kuwa muungwa na kuwa mtu mwenye kuwajali wenzake.

d/ i/ mvumilivu

ii/ Mkarimu

iii/ Hana makuu


iv/ Hauna ulivu.

**Kielelezo 1.1**: Mtahiniwa aliyepata alama nzuri.

Kielelezo 1.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu kwa usahihi vipengele (a), (c) na (d) isipokuwa kipengele (b) (ii).

Watahiniwa wengine asilimia 7.5 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 5.5 kutokana na kutoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali kwa baadhi ya vipengele. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yasiyo sahihi katika kipengele (a) ambapo aliandika

kichwa cha habari “Muungwana” kwa herufi ndogo badala ya kutumia herufi kubwa, (b) (ii) alitoa maana ya neno “Arifu” ambayo haikuwa sahihi, katika kipengele (c) alieleza wazo moja lisilojitosheleza. Kielelezo 1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kipengele (a), (b) pamoja na kipengele (c) kwa usahihi na kupata alama za wastani.




1.
(a) Kichwa cha habari ni Muungwana.
(b)
(i) Muungwana Ni mtu mwenye uvumilivu, Mkarimu na kushauri wenzie vema na pia yeye kushauriwa na kusikiliza.
(ii) Arifu ni mtu mwenye heshima kubwa au cheo katika jamii anayoishi
(iii) Hajitwezi Ni mtu asiyejikweza kwa vitu alivyonavyo
(iv) Mwadilifu Ni mtu mwenye hekima, busara na kujituma sana.
(c) Mawazo makuu Mawili
(i) Matumizi mabaya ya neno la Muungwana na jinsi inavyotumika tofauti katika jamii
(ii) Kuwajenga watu ili wajue Maana kamili ya mtu Muungwana na Tabia zake
(d) Tabia za mtu Muungwana
(i) mKarimu
(ii) Mwadilifu
(iii) Anajituma.

**Kielelezo 1.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani

Kielelezo 1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani

Aidha, watahiniwa wachache, asilimia 1 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kutokielewa kifungu cha habari na hivyo kushindwa kujibu vipengele vingi vya maswali yaliyoulizwa. Kwa mfano; mtahiniwa mmoja alipata alama hafifu kutokana na kushindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele (a) aliandika kichwa cha habari kuwa ni “UMUHIMU WA MAADILI MEMA” ambacho kilikuwa kinyume na habari aliyosoma na katika kipengele, (b) (ii) alitoa maana ya “Arifu” kuwa ni mtu *mwenye*

*utiifu kwa watu wote* badala ya mtu *mwenye maarifa/ujuzi* na kushindwa kujibu kabisa kipengele (c) na (d). Kielelezo 1.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.



1 (a) UMUHIMU WA MAADILI MEMA.

b)(i) Muungwana, Ni mtu mwenye maadili mema katika jamii au mtu mtiifu

(ii) Arifu. Ni mtu mwenye utiifu kwa watu wote.

(iii) Hajiwezi. - Ni mtu ambaye hana dharau.

(iv) Mwadilifu - Ni mtu mwaminifu

**Kielelezo 1.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.


Kielelezo 1.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kupata alama hafifu.

### 2.2.2 Swali la 2: Ufupisho

Swali lilitoka katika mada ya Ufupisho katika kipengele cha ufupisho na lililenga kupima uundaji. Swali lilimtaka mtahiniwa kufupisha habari aliyosoma kwa maneno tisini (90) na lilikuwa na alama 10.


Swali hili lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani na lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 96.5 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani kwa kupata alama kuanzia

3.5 hadi 9. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 2**: *Kufaulu kwa Watahiniwa Kiasilimia*

Asilimia 77.9 ya watahiniwa walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 9. Kati yao, asilimia 21.1 walipata alama za juu kuanzia alama 8 hadi 9.Watahiniwa hawa waliweza kutumia maarifa stahiki katika kufupisha habari kwa kuzingatia taratibu zote za ufupisho kama vile: *kutumia maneno yao wenyewe bila kupotosha kiini cha habari waliyopewa, mtiririko mzuri wa mawazo wenye mantiki na kuzingatia taratibu za uandishi, matumizi ya lugha sanifu na kuzingatia idadi ya maneno*. Kielelezo 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuandika ufupisho kwa kuzingatia taratibu zote za kufupisha habari.




2. Muungwana ni mtu mwenye utu, upendo, uvumilivu na ustahimilivu kwa watu wengine. Uungwana uliopo kwenye jamii zetu umekuwa ni wakinafiki, kitabaka, na wakimaslahi binafsi watu hujifanya wema ili tu kuonekana machoni pa watu lakini ndani yake amejaa chuki, fitina, uvuda, wivu, visasi.

Uungwana ndani ya jamii ni tabia ambayo huleta usawa kwa watu wote bila kujali elimu, cheo, mtoto, hata mtu mzima, kwa wakemavu. Jamii iliyo jengewa kwenye msingi ya utu na kujaliana ndiyo yenye maendeleo kwa jamii nzima. Pia tabia za kiungwana zinamuwezesha mtu kuishi popote dunia.

**Kielelezo 2.1**: Mtahiniwa aliyepata alama nzuri.

Kielelezo 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufupisha habari vizuri kwa kuzingatia matakwa ya swali.

Asilimia 18.6 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5 kutokana na kuandika ufupisho wenye mapungufu kama vile: kuzidisha idadi ya maneno, kutokuwa na mtiririko mzuri wa mawazo wenye mantiki, kutozingatia taratibu za uandishi na kutumia baadhi ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari. Kielelezo 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa kufuata taratibu na kanuni za ufupisho wa habari.



2 Muungwana sio mtu mwenye tabia za ajabu wala mtanashati au mtu arifu, muungwana ni mtu mwenye adabu wakutosha kutosana na mambo yanayo mzunguka pia muungwana ni mtu anaye a heshimu kumudhi wala kudharau mtu. Pia vile vile muungwana ni mtu anaye tambua wajibu wake katika jamii kwani ni katika kuchukua katika maendeleo ya jamii. Ngao na ngozi si kitu cha msingi wakati wa kutambua muungwana bali muungwana ni mtu yupo katika utendaji wa kazi na kutatua matatizo yake kwa nafsi hivyo basi muungwana hautokani na malezi ya shule ila hutokana na muungwana wa kwali.

**Kielelezo 2.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa yote ya uandishi wa ufupisho.

Licha ya swali hili kuwa na kiwango kizuri cha kufaulu, asilimia 3.5 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kuandika ufupisho wenye mapungufu kama vile: kuzidisha idadi ya maneno, kuandika habari tofauti kabisa na ile ya awali, kutokuwa na mtiririko mzuri wa mawazo wenye mantiki, kutozingatia taratibu za uandishi ipasavyo na kutumia baadhi ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari. Kwa

mfano, mtahiniwa mmoja alifupisha habari kwa kuandika habari tofauti kabisa na habari aliyopewa kama kielelezo 2.3 kinavyoonesha.


2. Katika jamii zetu tunaishi sana wazazi walezi kuleta mabadiliko na
atakayegundua kuwa sahihi kwa kila jambo la kweli na
haki hivyo basi lazima [illegible] vijana kuwa watu
wenye haki katika jamii yetu wanawe wazazi wa kujali
kuheshimu kuthamini, maoni ya kila mtu kwa nafasi yake
tuwe waadilifu katika kazi, katika masomo tunajali ata-
wale ambao ni masikini ili kuleta jamii mpya na yenye
uelewa kuhusu maisha binadamu inatakiwa hivi kwa-
kuoneana huruma ili [illegible] [illegible] wa mungu lazima tuwe waadilifu.

**Kielelezo 2.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 2.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.

### 2.2.3 SEHEMU B: MATUMIZI YA SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA


Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4). Kila swali lilikuwa na alama 10. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili tu.

### 2.2.4 Swali la 3: Utumizi wa Lugha

Swali lilitoka katika mada ya Utumizi wa Lugha, mada ndogo ya Misimu. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi maana ya misimu kisha kutumia mifano kueleza njia zitumikazo kuunda misimu ya lugha ya Kiswahili. Swali lililenga kupima Uchambuzi na lilikuwa na alama 10.

Swali lilikuwa la kuchagua hivyo asilimia 12.3 ya watahiniwa walijibu swali hili. Swali lilijibiwa vizuri ambapo asilimia 82.1 walifaulu kwa

kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 3 linaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 3**: *Kufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia*

Asilimia 65.4 ya watahiniwa walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Miongoni mwa watahiniwa hao asilimia 30.1 walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10 kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu misimu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kueleza maana ya misimu kwa usahihi na aliweza kufafanua njia nne za uundaji wa misimu kama vile: *Kufupisha maneno, tanakali sauti, kutumia sitiari na njia ya kukopa maneno* hivyo, kupata alama za juu. Kielelezo 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali vizuri.


3. Misimu, Ni maneno yasiyo rasmi yanayozuka na kutoweka. sifa za misimu hupendwa na vijana, huwa hisisha mawasiliano, hukuza lugha. pia hutumia kufi cha jambo kwa klasio husika. Yafuatazo ni njia ya kuunda misimu ya lugha ya Kiswahili:

Njia ya kufupisha Maneno, Misimu huundwa kwa kutumia njia hii ya kufupisha maneno mfano kal ika hili neno "Disco" lina na maana ya kutokuendelea na masomo pia maneno mengine mengi amb ayo hutumia kuunda maneno hilo neno lina maana ya mwanafunzi kutokuendelea na masomo kwahiyo njia mojawapo ya kuunda misimu ni njia ya ku fupisha maneno

Njia ya kutumia tanakali sauti, Misimu hutumia njia mbalimbali ikiwemo njia ya kutumia tanakali sauti kwa mfano fu tu tu fu tu hii huashiri a kuwa ni sauti ya risasi lap lap lap hii huashiria kuwa ni sauti ya viatu au malapa wakati mtu anatembea husikia sauti hiyo. kwahiy o Msamiati au Misimu hutumia njia ya tanaka li sauti.

Njia ya kutumia sitiari, hii hulinganisha vitu viwili vyenye hadhi sawa Mfano Juma amevaa Ngozi wa chupa inamaanisha Juma amevaa nguo au suruali iliyobana sana kwahiyo Misimu huu ndwa kwa njia nyingi sana ikiwepo njia ya kulinganisha vitu viwili tofauti na kupa hadh i sawa.

Njia ya kukopa maneno kutoka lugha za kigeni, Misimu hukopa maneno kutoka lugha za kigeni kwamf ano "fag" hili neno limechukuliwa kutoka lugha ya kiingereza lenye maana ya sigara kali hu


3. tumia Misimu ili kurahisisha Mawasiliano pia hu
tokana na hii njia tunaweza kukuza lugha kuto
kana na kupata Misamiati mipya kwahiyo Misim
u hutumia njia ya kukopa Maneno kwenye lugha
zingine.
Njia ya kubadili Maana ya Msingi ya neno,
Mfano "nimempia" badala ya kusema nimempe
nda sana kwahiyo Misimu huundwa kwa kutum
ia njia Mbalimbali ikiwemo njia ya kubadili
maana ya Msingi ya neno kama huyu Misimu
hutatambua Maana iliyotumika ndiyo Maana wat
u hupenda sana kutumia Misimu kwa sababu hu
kuza lugha.

**Kielelezo 3.1**: Mtahiniwa aliyepata alama nzuri.

Kielelezo 3.1 Kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefafanua kwa usahihi maana ya neno Misimu na njia zitumikazo kuunda misimu ya lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, asilimia 16.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili, walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5 kutokana na kutoa majibu ambayo hayakujitosheleza. Aidha, baadhi ya watahiniwa waliweza kueleza maana ya misimu na kufafanua kwa usahihi njia mbili tu za uundaji wa misimu lakini walishindwa kufafanua kwa usahihi njia ya kutohoa maneno kutoka lugha ya kigeni. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

3.

Misimu, ni maneno ambayo huzushwa na kikundi cha watu wachache wenye tamaduni moja, maneno haya huzuka na kutoweka, na mengine husanifishwa na kuwa lugha sanifu ya kiswahili. Mfano mboga saba, walalahoi, kimobiteli na mengine mengi ambayo hutokana na mabadiliko ya kila siku, matabaka, utani na kadhalika. Kuna misimu zagao, ya tarafa na pekee. Zifuatazo ni njia zitumikazo kuunda misimu ya lugha ya kiswahili.

Kutohoa maneno kutoka lugha ya kigeni, hii inasababishwa na kutojitosheleza kwa msamiati wa kiswahili hivyo kukopa au kuazima maneno kutoka lugha ya kigeni mfano kiingereza, kireno au lugha nyinginezo. mfano, kimobiteli, uko powa, fresh na kadhalika.

Tanakali sauti, hii inahusisha muigo wa sauti za kitu fulani kutokana na mlio wake au muigo wa sura au umbo lake. Misimu huundwa kwa njia ya kuiga sauti mfano. Malapa hii ni msimu unaomaanisha kandambili ambazo hulia lap! lap! wakati wa kutembea, pia mtaputapu, pombe ya machicha ambayo hulia tap! tap! wakati wa kuichuja.

Sitiari, hii pia ni njia ya kuunda misimu ambapo sitiari hutumika katika kuunda maneno mbalimbali mfano, "amevaa chupa" yenye maana ya kuamba amevaa kiunuali kinachambana sana ~~kwa~~ au chembamba sana mfano wa chupa "modo".

Kuhusianisha maisha ya watu na hali halisi katika jamii, misimu huundwa kwa kuangalia hali za watu kama vile maskini na matajiri. Mfano maskini → walalahoi

Matajiri → Mboga saba

**Kielelezo 3.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kushindwa kufafanua kwa usahihi baadhi ya hoja zake.

Asilimia 17.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kushindwa kutoa maana sahihi ya misimu na kufafanua njia nne zitumikazo kuunda misimu ya lugha ya Kiswahili. Kushindwa huko kunatokana na kuchanganya dhana ya misimu na njia za uundaji wa maneno. Kielelezo 3.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa maana ya misimu na kufafanua njia za uundaji wa misimu.

03 Misimu ni maneno zagao, maneno yanayoibuka kutokana na mazingira na nyakati.

Njia za kuunda misimu.

(i) Matukio, matukio yanapotokea watu kutumia lugha na misemo mbalimbali ambayo huibua misimu. Mfano Hapakazi tu! ni misimu uliotokea wakati wa kipindi cha kampeni za uchaguzi kwenye chama cha CCM.

(ii) Uambishaji

(iii) Mnyumbuliko

(iv) Urudufishaji

**Kielelezo 3.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.


Kielelezo 3.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefafanua maana ya misimu badala ya njia za kuunda misimu .

### 2.2.5: Swali la 4: Matumizi ya Sarufi

Swali lilitoka katika mada ya Matumizi ya Sarufi, mada ndogo ya Mofimu. Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha mofimu na kisha kutaja

kazi ya kila mofimu katika maneno aliyopewa. Swali lililenga kupima uchambuzi na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Watahiniwa 2,673 sawa na asilimia 12.3 walijibu swali hili kwa kuwa lilikuwa la kuchagua. Kiwango cha kufaulu kilikuwa cha wastani, kwani asilimia 70.3 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati 4.1 kinaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 3**: *kufaulu kwa Watahiniwa Kiasilimia*


Aidha, asilimia 23.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 9.5. Miongoni mwao, asilimia 3.3 walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 9.5 kwa kuwa waliweza kubainisha mofimu na kutaja kazi za mofimu. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alipata alama za juu kwa kubainisha mofimu na kutaja kazi zake japokuwa alishindwa katika vipengele (b) na (d). Kielelezo 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha mofimu na kutaja kazi zake.

4. (a) Akijikingia
→ A - ki - ji - king - i - a
A → kiambishi awali kinachodokeza nafsi ya tatu umoja.
ki → kiambishi awali kinachodokeza hali ya masharti na pia kuonesha njeo
ji → kiambishi awali kinachomlejelea mtendwa wa jambo ambaye ndiye mtenda pia.
king → Mzizi wa neno.
i → kiambishi tamati kinachodokeza kijenzi kinachodokeza kauli ya kutendea.
a → kiambishi tamati maana.

(b) Mchezaji
→ M - chez - a - ji
m → kiambishi awali kinachodokeza nafsi ya tatu umoja.
chez → mzizi wa neno

a → kiambishi tamati kinachosaidia kujenga mzizi wa neno
ji → kiambishi tamati kinamlejelea mtenda wa jambo.

(c) Asiyekujua
→ A - si - ye - ku - ju - a
A → kiambishi awali kinachodokeza nafsi ya tatu umoja.
si → kiambishi awali kinachodokeza ukanushi


4 (c) ye → kiambishi awali kinachomrejelea mtenda wa jambo.
ku → kiambishi awali kinachomrejelea mtendwa wa jambo.
ju → mzizi wa neno
a → kiambishi tamati maana.


(d) Mmeachiliana
m-me-achili-an-a
m → kiambishi awali kinachodokeza nafsi ya pili wingi.
me → kiambishi awali kinachoonesha wakati timilifu
achili → mzizi wa neno.
an → kiambishi awali cha kauli ya kutendana.
a → kiambishi tamati maana

**Kielelezo 4.1**: Mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Kielelezo 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali na kupata alama za juu kwa kuweza kubainisha na kutaja kazi za mofimu kwa usahihi.

Asilimia 46.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5 kutokana na kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele. Watahiniwa hao waliweza kubainisha baadhi ya mofimu kwa usahihi kama vile *m-chez-aji* na *a-si-ye-ku-ju-a* lakini wakashindwa kubainisha baadhi ya mofimu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kipengele (a) na (b) aliweza kubainisha na kutaja kazi za mofimu “Akijikingia” na “Mchezaji” kwa usahihi isipokuwa katika mofimu mbili za mwisho, Kipengele (c) na (d) aliweza kubainisha na kutaja kazi za mofimu “Asiyekujua” na “Mmeachiliana” katika mofimu ya kwanza na ya pili isipokuwa mofimu tatu za mwisho alishindwa

kubainisha na kutaja kazi za mofimu hizo. Kielelezo 4.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.



4 (a) Akijikingia
A - Nikiambishi awali cha nafsi ya tatu umoja.
-Ki - Kiambishi awali cha masharti
-ji - Kiambishi awali cha kauli ya kujitendea
-King - Mzizi wa neno
- ia Kiambishi tamati kauli ya kutendea.

(b) Mchezaji
M - Kiambishi awali nafsi ya tatu umoja
chez - Mzizi wa neno
-aji Kiambishi tamati kauli ya mtenda.

(c) Asiyekujua
A - Kiambishi awali nafsi ya tatu umoja
-si - Kiambishi awali cha ukanushi
-ye - Kiambishi awali cha urejeshi
-kuj - Mzizi wa neno
-ua Kiambishi tamati kauli ya mtenda.


(d) Mmeachiliana
M - Kiambishi awali nafsi ya pili wingi
-me - Kiambishi awali cha wakati timilifu
-ach - Mzizi wa neno
-ili - Kiambishi tamati kuonyesha mtenda.
-ana Kiambishi tamati kauli ya kutendeana.

**Kielelezo 4.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu baadhi ya vipengele vya mofimu na kutaja kazi zake na kupata alama za wastani.

Asilimia 29.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu hivyo walipata alama kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kushindwa kubainisha mofimu na kazi za kila mofimu katika maneno

waliyopewa. Hii ilitokana na watahiniwa hao kuwa na mawanda madogo ya maarifa juu ya kubainisha mofimu na kazi zake. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kipengele (a) alitoa maana ya neno “Kinga” badala ya kubainisha mofimu za neno “Akijikingia” na kipengele (b) alitoa maana ya neno “Mchezo” badala ya kubainisha mofimu za neno “Mchezaji” na kutaja kazi zake. Kielelezo 4.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.


4. (a) Ni kitendo cha kujizuia kwa kutumia kitu fulani,

4. (a) Kinga – Kujikingia ni kitendo cha kujizuia kwa kutumia kitu fulani kama vile mwamvuli au ngao.

(b) Mchezo – Ni mtu mwenye ujuzi wa kucheza mchezo fulani yaweza kuwa mpira wa miguu au muziki.

(c) Kujua – Ni kitendo cha kukijua kitu fulani au mtu fulani, neno "asiyekujua" ni hali ya mtu kutofahamika na mtu fulani.

(d) Achilia – kitendo cha kufoshoka kitu neno "kuachilians" ni hali au kutokamalika

5 (i) Kielezi – ni sentensi neno linalo simama kuelezea jambo fulani, mfano kilimo kinanyofanyika.

(ii) Kiwakilishi – ni neno linalo simama kumwakilisha mtu, au kitu, mfano John amekuja kwa niaba ya Juma.

(iii) Kivumishi – Ni neno linalo simama kuvumisha au kutoa sifa juu ya mtu au kitu fulani mfano merry anakimbia kwa nguvu.

**Kielelezo 4.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 4.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha mofimu na kutaja kazi ya kila mofimu hivyo kupata alama hafifu.

### 2.2.6 Swali la 5: Matumizi ya Sarufi

Swali lilitoka katika mada ya Utumizi wa Sarufi na lilipima Kuunda. Swali lilimtaka mtahiniwa (a) kufafanua maana ya istilahi alizopewa kwa kutumia mifano na (b) kutumia neno ‘‘ZURI’’ kutunga sentensi

mbili kwa kila aina ya maneno alizopewa. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Watahiniwa 13,721 sawa na asilimia 63 ya watahiniwa wote walifanya swali hili. Kwa ujumla swali hili lilijibiwa vizuri ambapo asilimia 98.3 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Jedwali Na 1 inaonesha viwango vya kufaulu katika swali hili kiasilimia.

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0 – 3.0 | 236 | 1.7 |
| 3.5 – 5.5 | 1,475 | 10.7 |
| 6.0 – 10 | 12019 | 87.5 |

**Jedwali Na 1**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Watahiniwa wengi, asilimia 87.5 walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Miongoni mwao, asilimia 61.7 walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10 kutokana na kutoa hoja zilizosahihi na kufafanua maana ya istilahi walizopewa katika kipengele (a) Pia katika kipengele (b) waliweza kutumia neno‘‘ZURI’’ kutunga sentensi mbili kwa kila aina ya maneno walizopewa kwa usahihi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi katika kipengele (a) (i) hadi (iv) na kipengele (b) kipengele (ii) na (iii) lakini alishindwa kutunga sentensi ya pili katika kipengele kidogo (i). Kielelezo 5.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kupata alama za juu.

5 a) i) Kielezi

- ni aina ya maneno au neno ambayo hutumika kuelezea jambo lililotendeka au linalotendeka. Kielezi huweza kuonesha idadi ya kitu, huweza kuonesha namna au jinsi jambo lilivyotendeka, huweka kuelezea mahali jambo linapotendeka au lilipotendeka.

mfano, Hospitali imetembelewa kwa mara ya tatu

Anna amependa upande wa Mashariki

Juma anatembea kibabe.

ii) Kiwakilishi

- ni maneno ambayo hutumika kuwakilisha nomino, au maneno ambayo huweza kusimama badala ya nomino na kukamilisha maana ya sentensi kuna viwakilishi vya mahali, viwakilishi vya namna au jinsi, viwakilishi vya dhahania

mfano, Yule pale ni rafiki yangu

Mimi napenda kucheza ngoma

Wale wanatembea kwa maringo


iii) Kivumishi

- ni maneno ambayo hutumika kuelezea au kuonesha sifa za mtendaji au mtendwa wa jambo fulani hutumika zaidi kuelezea nomino katika sentensi mbalimbali kuna vivumishi vya mahali vivumishi vya a-unganifu na aina nyingine za vivumishi

mfano, Kijana mwerevu amepata ajira

Msichana mrembo ameolewa

Watoto watoro wamekamatwa.




**Kielelezo 5.1**: Mtahiniwa aliyepata alama nzuri.

Kielelezo 5.1 Kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kufafanua maana za istlahi na kutunga sentensi mbili kwa kila istlahi kwa usahihi.

Aidha, asilimia 10.8 ya watahiniwa walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5 kwa kuwa walitoa hoja zisizojitosheleza. Baadhi yao walitoa majibu sahihi kwa baadhi ya hoja na kushindwa katika hoja nyingine. Kwa mfano; mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile: *kiwakilishi ni maneno yanayowakilisha nomino, kivumishi ni maneno yanayotoa taarifa ya kiwakilishi na nomino, kielezi ni maneno yanayotumika kueleza sifa ya kitenzi, kitenzi ni maneno yanayotumika kueleza tendo linalofanyika, lililofanyika na litakavyofanyika*. ila alishindwa kutunga sentensi mbili kwa usahihi kwa kutumia neno "ZURI" kwa kila aina za maneno aliyopewa isipokuwa alipata sentensi moja tu katika kipengele (b) (i) Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyojitosheleza.

5 a.

i. Kielezi

Ni aina ya maneno ambayo hutumika kueleza a sifa ya kitenzi (tendo).

Mfano: Aisha anaimba vizuri sana

E

ii. Kivumishi

Ni aina ya maneno yanayoelezea nomino

Mfano: ~~A~~ Neya ni mrefu sana


W

iii. Kivumishi

Ni maneno yanayotumika kutaja sifa ya kivumishi na nomino.

Mfano: Tanzania ni nchi yenye amani

V


3 a.
iv. Kitenzi
Ni aina ya maneno inayotumika kueleza tendo linalofanyika, lililofanyika au litakalofanyika.
Mfano: Juma anacheza mpira.
T

b.
i. Kielezi
- Mwalimu wa sayansi hufundisha vizuri.
E
- Mtoto mzuri anatambaa.
E

ii. Kiwakilishi
- Yeye huimba vizuri kanisani
- Yule ni mchezaji mzuri mno.


iii. Kivumishi
- Wanafunzi wote wamefaulu vizuri sana
- ~~Tanzania inavutia vizuri barani Afrika.~~
- Hiki kikombe ni kizuri

**Kielelezo 5.2:** Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 5.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa kujibu kwa usahihi vipengele vingine.

Watahiniwa asilimia 1.7 waliofanya swali hili walipata alama hafifu kuanzia alama 0 hadi 3. Watahiniwa hawa walikosa uelewa wa kutosha kufafanua maana za istilahi walizopewa na kutumia neno ‘‘ZURI’’

kutunga sentensi mbili kwa kila aina za maneno walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kipengele (a) (i), (iii) na (iv) alitoa maana zisizosahihi pia katika kipengele (b) alishindwa kutunga sentensi mbili zilizosahihi kwa kutumia neno "ZURI". Vile vile katika kipengele cha (iii) alitunga sentensi moja tu. Kielelezo 5.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata alama hafifu.


5a i) Kielezi
- Ni aina ya maneno yanayotumika kuelezea sifa ya kitu chochote kwa mfano "nzuri".
ii) Kiwakilishi
- ni aina ya maneno ambayo yanawakilisha nomino ya kitu fulani kwa mfano: yeye, huyu.
iii) Kivumishi
- ni aina ya maneno yanayo simama badala ya nomino kwa mfano: anakuja.
iv) Kitenzi
- ni aina ya maneno yanayo kueleza kuhusu kiwakilishi mfano: kulima.
B) ~~Kielezi~~
B i) yule mtoto amevaa shati zuri sana.
ii) Gari lake ni zuri zaidi.
iii) Gari zuri limepita sasa hivi.


**Kielelezo 5.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 5.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vipengele (a) na (b) na kupata alama hafifu.

### 2.2.6 Swali la 6: Matumizi ya Sarufi.

Swali hili lilitoka katika mada ya Matumizi ya Sarufi na lililenga kupima Uundaji. Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja dhima tano za mofimu ‘‘KI’’ kisha kutunga sentensi mbili kwa kila dhima. Swali lilikuwa na alama 10

Swali hili lilikuwa la kuchagua na lilijibiwa na watahiniwa 2,106 sawa na asilimia 14.2. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo asilimia 94 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na 4 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 4**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 73.3 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10 kwa kuwa waliweza kutaja dhima tano za mofimu ‘‘KI’’ na kutunga sentensi mbili kwa kila dhima. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alijibu vizuri swali hili kwa kutaja dhima za mofmu kama vile: *(a) kuonesha hali ya masharti (b) kuonesha hali ya udogoishi (c) hutumika kuonesha upatanisho wa kisarufi (d) hutumika kama kitenzi kishirikishi (e) hutumika katika ngeli ya nne KI – VI* na kuweza kutunga sentensi mbili kwa usahihi kwa kila dhima. Kielelezo 6.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyetaja dhima tano za mofimu KI na kutunga sentensi mbili kwa kila dhima.

06. Dhima za mofimu "ki".

(a) Huonesha hali ya masharti.

Mfano: Akija, niambie

Akilala tuondoke.

- Mofimu "ki" katika sentensi zimetumika kuonesha hali ya masharti.

(b) Huonesha hali ya udogoishi (kudogoisha).

Mfano: Kitoto ni kizuri

Ki-meza ni kichafu.

- Mofimu "ki" zimetumika kudogoisha "mtoto" kuwa "kitoto" na "meza" kuwa "kimeza".

(c) Hutumika katika upatanisho wa kisarufi.

Mfano: Kiti kimevunjika

Kiatu kimechanika

- Mofimu "ki" zimetumika katika kupatanisha nomino na vitenzi vilivyofuatana.

(d) Hutumika kama kitenzi kishirikishi.

Mfano: Kiatu ki ndani.

Chakula ki mezani.

- Mofimu "ki" zimetumika kama vitenzi vishirikishi katika sentensi

(e) Hutumika katika ngeli ya nne (KI-VI).

Mfano: Kikombe kimevunjika


Vikombe vimevunjika

- Mofimu "ki" imetumika kuonesha hali ya umoja katika ngeli ya KI-VI.

**Kielelezo 6.1:** Mtahiniwa aliyepata alama nzuri.

Kielelezo 6.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetaja dhima tano za mofimu “KI” na kutunga sentensi mbili kwa kila dhima.

Asilimia 20.7 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5 kutokana na kutaja baadhi tu ya dhima za mofimu “KI” na kutunga baadhi tu ya sentensi za dhima za mofimu "KI" kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutaja dhima mbili za mofimu “KI” lakini alishindwa kutaja dhima nyingine kwa usahihi na kuzitungia sentensi. Kielelezo 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.


6. (i) Kuonyesha ngeli ya Ki-Vi
mfano:- Kijiko kimevunjika - vijiko vimevunjika
= Kikombe cha babu kimechaka - vikombe
vya babu vimechaka.

(ii) Kuonyesha udogoshi wa kitu.
Kwa mfano,
- Kitoto kidogo kinalia sana
- Kijito cha maji kimefurika leo.

(iii) Kuonyesha hali ya kutendeka kwa jambo (maagizo)
mfano. ukisoma utafaulu
ukiondoka usisahau kuniaga


(iv) Kuonyesha nomino ya vitu au watu,
mfano, Kikombe cha bluu ni kizuri
Kikwetwe ni raisi mstaafu

(v) Kuonyesha sifa ya kitu au mtu,
mfano. Kizuri chajiuza
Kibaya chajitembeza

**Kielelezo 6.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 6.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutaja dhima mbili za mofimu “KI” na kuzitungia sentensi lakini alishindwa kutaja na kutunga sentensi za dhima tatu**.**

Asilimia 6 ya watahiniwa walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kushindwa kutaja dhima tano za mofimu "KI" kwa usahihi na kushindwa kutunga sentensi mbili kwa kila dhima. Hii ni kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhima za mofimu “KI”. Watahiniwa wengi walitaja dhima na kutunga sentensi zisizosahihi kama kielelezo 6.3 kinavyoonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutaja dhima tano za mofimu "KI" na kutunga sentensi mbili kwa kila dhima tajwa.



6 Mofimu ni kipashio kidogo kabisa katika lugha chenye maana ya kisarufi. Zifuatazo ni dhima za Mofimu "ki"

(i) kutumika kudunisha kitu. Mfano kitoto kinasoma shule, kiti kidogo

(ii) Kuonyesha mahali
Mfano - Kiti kipo darasani
- lete kile kitabu

(iii) kuonyesha wakati au nyakati
Mfano chakula kimeisha.
kiti kilivunjika.

(IV) kuonyesha hali ya ukanushi
Mfano kitabu hakikuibwa
kitabu hakikuchanika

(V) kuonyesha hali ya kisababishi
Mfano kisu kile kimeniumiza
kilimo hiki kina madhara

**Kielelezo 6.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 6.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na kushindwa kutaja na kutunga sentensi sahihi za mofimu "ki".


## 2.3 SEHEMU C: UTUNGAJI

Sehemu hii ilikuwa na swali moja na lilikuwa na alama 20. Watahiniwa wote walitakiwa kujibu swali hili kwa kuwa lilikuwa la lazima.

### 2.3.1 Swali la 7: Utungaji

Swali lilitoka katika mada ya Utungaji katika mada ndogo ya Uandishi wa Insha. Swali lililenga kupima Uundaji na lilimtaka mtahiniwa aandike insha yenye maneno yasiyopungua 350 na yasiyozidi 400 kuhusu jitihada za serikali ya Tanzania katika kuleta maendeleo kwa wananchi na aoneshe changamoto zinazokwamisha jitihada hizo.

Asilimia 98.8 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha ya kuandika insha kwa kuzingatia vigezo muhimu. Chati Na. 5 imeonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na 5**: *Kufaulu kwa Watahiniwa Kiasilimia*

Asilimia 74.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu na kupata alama kuanzia 12 hadi 19.5. Kati yao, asilimia 9.9 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19.5 kwa kuwa waliweza kutunga insha kwa kuzingatia mambo muhimu kama vile:

*kichwa cha habari kwa herufi kubwa, kutoa utangulizi mzuri unaoendana na swali, kueleza kiini kwa kutoa hoja sahihi na kutoa hitimisho linalotoa mapendekezo yanayoendana na swali.* Kielelezo 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetunga insha kwa usahihi.

7 JITIHADA ZA SERIKALI YA TANZANIA KATIKA KULETA MAENDELEO.

Maendeleo ni kitendo cha kubadilika kutoka hatua ya chini na kwenda hatua ya juu. Serikali yetu ya Tanzania inafanya jitihada mbalimbali katika kuleta maendeleo kwa mananchi wake. Jitihada hizo ni kama zifuatazo:-

Kuboresha miundombinu. Serikali inafanya jitihada kuboresha miundombinu ili kuleta maendeleo katika jamii. Miundombinu hizo ni kama vile barabara, njia za reli ili kurahisisha usafirishwaji wa bidhaa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Kuboresha huduma za afya. Serikali yetu inajitahidi ~~kuf~~ kuboresha sekta ya afya kwa kujenga hospitali ambayo

7 ina ~~kidhifdhi~~ kidhi mahitaji ya watu na kuwatafuta wataalamu walio bobea katika huduma hizo ili ku-okoa maisha ya wananchi wake.

Kuboresha huduma za maji safi na salama. Serikali yetu ina jitahidi kuboresha huduma ya maji kwa kuwapatia wananchi maji safi na salama kwani walinejaribu kuvuta mabomba ya maji na kujenga tenki kub-wa ambazo zinatunza maji kwa muda ~~mr~~ mrefu. au kuhifadhi maji

Imeboresha huduma za elimu. Serikali yetu ya Tanzania imeweza ku borasha sekta ya elimu kwa kuwapatia wanafunzi vitabu mba limbali vya kiada na ziada na pia imetoa miongozo mbalimbali kwa waalimu ili kuweza kuwa fundisha wanafunzi.

umuhimu wa Imeweza kuwasisitiza wananchi kutunza mazingira; Serikali ~~inawa~~ si imeweza kuwapa elimu wana-nchi wake umuhimu wa kutun-za mazingira ili kuepukana na magonjwa mbalimbali kama vile kipindupindu na malaria.

Kutokana na jitihada hizo pia Serikali inapata changamoto ambazo hukwamisha maendeleo hayo. cha-ngamoto hizo ni kama zifuata

7 Uhaba wa fedha; Serikali. ~~AU~~
inakumbwa, na tatizo la kutokuwa na
fedha ya kutosha ili kukidhi mahita
ji ya wananchi hivyo hukwamisha
maendeleo.
Uhaba wa wataalamu; Serikali
pia inakumbwa na tatizo la kutoku-
wepo kwa wataalamu wa kutosha
katika nyanja za elimu. Mfano
katika Masomo ya Sayansi amb-
ayo hufanyika kwa vitendo.
Uhaba wa zana za kufa-
nyia kazi; Pia Serikali yetu inaku-
bwa na tatizo la uhabwa wa
vifaa vya kufanyia kazi kama vile
vifaa vinavyotumika katika maso
mo ya Sayansi, na pia vifaa vina
vyo tumika katika ujenzi wa barabara.
Wananchi kutokuwa na ushiriki-
ano na Serikali. Pia jambo hili
lina weza kuleta changamoto kwa
serikali kwani umoja ni nguvu na
utengano ni udhaifu.
Hivyo basi japokuwa Serikali
yetu imekutana na changamoto
nyingi lakini imejitahidi kutimi-
za wajibu wake na kuleta
maendeleo kwa watu wake
kiuchumi, kisiasa na kijamii.
(Maneno 400)

**Kielelezo 7.1**: Mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Kielelezo 7.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeandika insha kwa kuzingatia taratibu zote za uandishi na kupata alama za juu.

Watahiniwa 5,318 sawa na asilimia 24.4 walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kuandika insha kwa kuzingatia vigezo vichache na kutoa ufafanuzi usio dhahiri kuhusu "Jitihada za serikali ya Tanzania katika kuleta maendeleo kwa wananchi na kuonesha changamoto zilizokwamisha jitihada hizo". Mtahiniwa mmoja aliandika hoja zinazoonesha jitihada zote za serikali ya Tanzania katika kuleta maendeleo kwenye aya moja, changamoto zote zinazokwamisha jitihada hizo kwenye aya moja kinyume na taratibu na kanuni za uandishi wa insha. Aidha, hakuwa na utangulizi wala hitimisho. Hii inadhihirisha kuwa mtahiniwa hakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu utungaji wa insha. Kielelezo 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika insha isiyojitosheleza na kupata alama za wastani.

7 JITIHADA YA SERIKALI YA TANZANIA KULETA MAENDELEO KWA WANANCHI


Tanzania ni nchi mojawapo ambayo ipo miongoni mwa nchi za Afrika mashariki, Serikari ya Tanzania imefanya Juhudi mbalimbali katika kuleta maendeleo kwa wananchi wa Tanzania Juhudi hizo ni Juhudi zilizofanywa na Serikari katika nyanja zote za kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni na mila. Juhudi hizo ni kama vile, kujenga barabara, kusambaza umeme hadi vijijini, kujenga Shule kwa

7. ajili ya kutolea elimu pia hata kuanzishwa kwa upatikanaji wa vyanzo vya maji, kwa maeneo mengi sana hapa Tanzania yalikuwa na matatizo ambayo yaliyokuwa yakiwakumba watu, kutokana na Serikali kutazama kwa jicho la karibu sana.

Serikari pia imesaidia katika kutoa elimu na kuwahamasisha watu kufanya kazi kwa bidii ili waweze kuleta maendeleo katika maswala ya nyanja zote za kijamii na kiuchumi, kwa mfano katika Sera ya Sasa "hapa kazi tu" imewahamasisha watu kufanya kazi kwa bidii, kama wakulima na wafanyabiashara, Hivyo kupitia Sera ya Tanzania Serikali imejitahidi katika kutatua na kupunguza changamoto chache nchini Tanzania.

Kutokana na Serikari kufanya juhudi zote za maendeleo ya wananchi kuna changamoto nyingi zilizokwamisha jitihada hizo kama vile magonjwa, Ukosefu wa fedha za kuendeshea miradi kama ya ujenzi, Pia hata Suala la njaa, kuna baadhi ya maeneo kama vile Singida na Dodoma yamekuwa yakikubwa na Tatizo la Ukame kwa muda mrefu hivyo kupitia changamoto hizo zimepelekea Serikali kushindwa kukidhi na kuleta maendeleo kwa wananchi.

Pia Serikari ya Tanzania imefanya


7 Juhudi katika uanzishaji wa viwanda vidogovidogo pamoja na kwamba tumeingiliwa na Sayansi ya nchi za nje imepelekea viwanda vyetu kudumaa na kuwa tegemezi kwa nchi za nje, Ukiangalia katika masuala ya ajira kutokana na ujuzi mdogo, Wageni wamewekeza katika nchi yetu na kutonyonya Rasilimali zetu pasipo sisi kujua pia hata katika nguvu kazi zetu, wageni wametunyonya Sana, kwa kutumia kazi nzito kwa kulipa ujira mdogo, pia hata katika Rasilimali tulizonazo kama madini na mazao. Hizi ni changamoto zinazokwamisha maendeleo ya Tanzania pia hata Serikali kutoa huduma kwa jamii yetu.

**Kielelezo 7.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 7.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kuzingatia baadhi tu ya mambo muhimu ya uandishi wa insha.

Asilimia 1.2 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama za chini kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kukosa uelewa wa kutosha juu ya uandishi wa insha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika insha yenye kichwa cha habari "JITIHADA ZA SERIKALI KUKUZA KISWAHILI" kinyume kabisa na matakwa ya swali lililomtaka aandike insha inayohusu "JITIHADA ZA SERIKALI KATIKA KULETA MAENDELEO KWA WANANCHI". Kielelezo 7.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuandika insha kwa usahihi.

07

# JITIHADA ZA SERIKALI KUKUZA KISWAHILI

Kiswahili ni lugha inayotambulika Tanzania kama lugha rasmi, lugha ya mawasiliano, na lugha ya kufundishia. Pia zipo nchi zinazotumia Kiswahili kama Kenya, Uganda, Congo kama lugha ya mawasiliano na kama somo. Serikali inashiriki sana kukuza na kuendeleza Kiswahili ndani na Duniani jitihada hizo ni kama.


Matumizi ya Kiswahili katika bunge; bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hutumia Kiswahili katika vikao vyake.

Uwezeshaji wa Wataalamu wa Kiswahili nchi za nje; Mfano Marekani, China Kanada. kupo wataalamu kama Wataalamu wa Kiswahili ambao huenda huko kwa lengo na wataalamu waishio nje za nchi za nje.

Serikali ilichagua lahaja ya Kiunguja; lahaja hii ndio Kiswahili ambayo ilichaguliwa Mwaka 1930 na kufanya Kiswahili kuwepo mpaka leo. Pia zipo changamoto katika kukuza Kiswahili kama vile.

Upinzani kutoka lugha za kigeni; Mfano, Kiingereza kutumika kwa wingi na kufanya watu waache kutumia Kiswahili.

Upungufu wa Machapisho ya lugha ya Kiswahili, Mfano Vitabu, na Majarida yapo kwa uchache zaidi


07 Wanajenzi kukosa desturi ya kusoma, hii inapelekea wao kutojinolewa kujua maendeleo ya Kiswahili kwani wanajikita na mitandao peke kama facebook!!.
Hivyo basi hii ni wajibu wa kila mtanzania kuwa na hamu ya kujua lugha ya Kiswahili kwa kusoma makala za Kiswahili na kuzungumza popote pale.

**Kielelezo 7.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 7.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeandika insha kwa kutumia kichwa cha insha tofauti na alichopewa hivyo kupata alama hafifu.


## 2.4. SEHEMU D: MAENDELEO YA KISWAHILI

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili. Kila swali lilikuwa na alama 20. Mtahiniwa alipaswa kujibu swali moja kati ya mawili aliyopewa.

### 2.4.1 Swali la 8: Maendeleo ya Kiswahili

Swali lilihusu mada ya Maendeleo ya Kiswahili na mada ndogo ya kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki. Swali lililenga kupima tathmini na lilimtaka mtahiniwa atumie hoja sita kutathmini mafanikio ya lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Watahiniwa 10,692 sawa na asilimia 49 ya watahiniwa wote walijibu swali hili. Asilimia 99.8 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na 6 inaonesha viwango vya kufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 6**: *Kufaulu kwa Watahiniwa Kiasilimia*

Zaidi ya nusu ya watahiniwa, (asilimia 92.9) walijibu swali hili na kupata alama nzuri kuanzia 12 hadi 19. Miongoni mwao asilimia 6.2 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mafanikio ya lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki. Watahiniwa walionyesha kuwa Kiswahili kilitumika katika *elimu, mikutano ya kimataifa, vyombo vya habari, shughuli za kiofisi, biashara na kama lugha ya taifa*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu vizuri swali hili kwa kutathmini mafanikio ya lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki japokuwa, katika utangulizi wake hakutoa maana ya lugha. Kielelezo 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama nzuri kutokana na kutathimini mafanikio ya lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki kwa usahihi.

SEHEMU D


8. Lugha ya kiswahili imepitia changamoto nyingi kuanzia kipindi cha ukoloni mpaka sasa. Lakini pamoja na changamoto hizo pia kuna mafanikio mengi yanayojitokeza ndani ya Afrika mashariki. Mafanikio hayo yanafanya lugha ya kiswahili kuzidi kukua katika eneo kubwa na kupata msamiati mpya. Ifuatayo ni tathimini ya mafanikio ya lugha ya kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki kama ifuatavyo:-

Kiswahili kutumika katika elimu; hii ni miongoni mwa mafanikio ya lugha ya kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki kwani kiswahili kimekua kikitumika kufundishia shule za msingi. Lakini pia kiswahili ni moja ya somo katika shule za msingi mpaka vyuoni. Haya ni mafanikio makubwa sana. Mfano Tanzania na Kenya zinatumia kiswahili katika elimu.

Kiswahili kutumika kama lugha ya taifa; hii pia ni miongoni mwa mafanikio ya lugha ya kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki kwani kimetumika kama lugha ya kuunganisha makabila yote ndani ya nchi. Mfano Tanzania na Kenya kiswahili ni lugha ya taifa

Kiswahili kutumika katika mikutano ya kimataifa; lugha ya kiswahili imekua ikitumika katika shughuli mbalimbali za mikutano ya kimataifa. Mfano Jumuia ya nchi za Afrika mashariki yaani Tanzania, Kenya, Uganda na nyingine wamekua wakitumia lugha ya kiswahili kuendesha shughuli na mikutano hiyo.

Kiswahili kutumika katika vyombo vya habari; ni mafanikio makubwa kwani imerahisisha watu kupata habari mbalimbali kwa urahisi hata kama utakua nje ya nchi yako. Mfano lugha ya kiswahili inatumika-



2. Kuwepo vituo vya radio, vituo vya televisheni, magazeti na hata majarida mbalimbali.

Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za kiofisi, haya ni mafaniko makubwa kwani ofisi zote za serikali za nchi za Afrika Mashariki zinasisitiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli zote. Mfano shughuli za bunge na shughuli za mahakama

Lugha ya Kiswahili kutumika katika biashara Wafanya biashara wa nchi mbalimbali za Afrika ya Mashariki wanapokutana, hutumia lugha ya Kiswahili kuwasilisha mawasiliano miongoni mwao. Mfano wafanya biashara kutoka Burundi wanapoenda Kenya hutumia lugha ya Kiswahili na hivyo kudhihirisha wazi maendeleo ya lugha ya Kiswahili Afrika mashariki.

Kwakumalizia, pamoja na mafaniko hayo ya lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki, bado kuna upinzani unaoikumba. Kama vile upinzani kutoka lugha za makabila na lugha za kigeni kama vile Kiingereza. Pamoja na uhaba wa wataalamu kwa ajili ya kufundisha lugha ya Kiswahili, kwani wasomi wengi wamekuwa wakibagua kusoma Kiswahili wawapo vyuoni kutokana na kasumba.

**Kielelezo 8.1**: Mtahiniwa aliyepata alama nzuri.

Kielelezo 8.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa ufasaha na kupata alama nzuri.

Aidha, watahiniwa asilimia 6.9 waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5 kutokana na kutotathmini vizuri baadhi ya mafanikio ya lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa *Kiswahili hutumika kwenye vikao vya umoja wa mataifa* na *kwenye mahakama za kimataifa* ambazo si hoja sahihi. Pia, alieleza *Kiswahili kutumika kwenye biashara* bila kutoa mfano wa nchi ambako biashara zinafanyika kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Kielelezo 8.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu baadhi ya hoja na kushindwa nyingine.


8. Lugha, ni mfumo wa sauti za
nasibu zenye mpangilio maalumu
ili kukidhi mawasiliano, lugha ya
kiswahili ni lugha ya kimataifa
kwani inatumika katika mataifa
mbalimbali kama vile kenya na nchi
zingine zote za Afrika mashariki.
Kuna mafanikio ya lugha ya ki
swahili katika nchi za Afrika ma
shariki kama ifuatavyo,
Kiswahili kinatumika katika miku
tano ya kimataifa kama vile Umoja wa
mataifa, katika mkutano huu kiswahili
kinatumika katika kuongoza shughuli
zote za mkutano kama vile kutolea
hoja fulani ya mjadala uliopo mezani
kama ni vita au uhasama uliowote
ulitokea, hutumika lugha ya kiswahili.
Kiswahili kutumika katika biasha
ra za kimataifa, katika suala la bia
shara hutumika kiswahili katika kuuza
bidhaa hizo hivyo katika masoko
ya kimataifa Kiswahili kinatumika
katika zoezi zima la kuuza na ku
nunua vitu.
Kiswahili kinatumika katika
elimu, katika vyuo vya kimataifa
kiswahili hufundishwa kama somo
mfano chuo kikuu cha Makerere Uga
nda kuna somo la kiswahili amba
lo wanafunzi hupata stashahada zao

8. Kwa kufaulu somo la kiswahili hivyo ni mafanikio makubwa sana katika lugha.

Kiswahili kimefanikiwa kutumika katika vyombo vya habari kama vile redio, televisheni au runinga, mfano katika redio BBC (Breatish Broadcasting corperation) katika kutoa matangazo mbalimbali hutumia lugha ya kiswahili mfano kila siku asubuhi saa 12:00 hutoa habari za kimataifa kwa lugha ya kiswahili.

Kiswahili kinatumika katika shughuli za mahakama, katika mahakama za kimataifa kiswahili hutumika katika ngazi ya juu kabisa ya mahakama, katika mahojiano hutumia lugha ya kiswahili katika hukumu au katika kutoa maagizo yao kwani kiswahili ni lugha ya kimataifa.

Kiswahili kuhumika katika ulimwengu wa sanaa na fasihi, katika fasihi kuna vitabu vihavyo andikwa kwa lugha ya kiswahili na hutumika katika mataifa mengine pia katika sanaa kuna baadhi ya wasanii huimba nyimbo zao kwa lugha ya kiswahili mfano Christiani Bella yeye huimba nyimbo zake kwa lugha ya kiswahili hivyo hu



8. Fikisha ujumbo kupitia lugha ya kiswahili -
Kwahiyo lugha ya kiswahili mbali ya kuwa imefanikiwa kati ka kiuchumi, kisiasa na kijamii lakini kuna matatizo yaliyojitokeza mba lugha hiyo katika kueneza kukuza kiswahili kama vile kadu mba, uhaba wa fedha pamoja na uhaba wa wataalamu wa lugha ya kiswahili katika kukikuza na kukieneza ~~Nch~~ nchi nyingine za Afrika mashariki.

**Kielelezo 8.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetathmini vizuri baadhi ya hoja za mafanikio ya Kiswahili katika nchi za Afrik Mashariki


Watahiniwa, asilimia 0.2 walishindwa kujibu vizuri swali hili na kupata alama hafifu kuanzia 1 hadi 6.5 kutokana na kukosa maarifa na ujuzi wa kutathmini mafanikio ya lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja za kukua kwa sekta nyingine kama vile: *Ukuaji wa biashara, shughuli za kilimo* kinyume kabisa na matakwa ya swali. Katika hoja kuhusu *Amani na mshikamano* alitoa ufafanuzi usioendana na swali na alitoa hoja moja ya *elimu* ambayo ilikuwa sahihi. Vilevile, hakuwa na hitimisho. Kielelezo 8.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa hoja zinazotathmini mafanikio ya lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika ya Mashariki.

8. Lugha ni nyenzo/njia ambayo watu hutumia katika mawasiliano. Lugha ya kiswahili ni lugha ambayo ni ya taifa nchini Tanzania. Kiswahili hakitumiki tu Tanzania bali kinatumika kwenye nchi nyingine kama vile Kenya, Uganda, Congo na hata kuna baadhi ya watu wa nje ambao hujifunza kiswahili. Yafuatayo ni mafanikio ya lugha ya kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki:-

Ukuaji wa biashara: Lugha ya kiswahili ndiyo imekuwa ikitumiwa kwa kiwango kikubwa katika mikataba ya shughuli mbalimbali za kibiashara. Biashara kwa asilimia imewezesha kukua na kuenea kwa lugha ya kiswahili katika nchi za Afrika mashariki. ukuaji wa biashara hupelekea ukuaji wa uchumi.

Elimu: katika nchi mbalimbali katika Afrika Mashariki lugha ya kiswahili inatumika katika kufundishia wanafunzi. Lugha ya kiswahili ni nyepesi na rahisi kueleweka hivyo wanafunzi wanapofundishwa huwafanya waelewe zaidi.

Shughuli za kilimo huleta uchumi mzuri katika nchi. kilimo ndiyo uti wa mgongo katika nchi mbalimbali za Afrika mashariki. kupitia shughuli za kilimo ambapo lugha ya kiswahili ndo ilikuwa ikitumika kama njia ya mawasiliano hii ilisaidia kilimo kukua kwa asilimia


kubwa na hivyo kupelekea maendeleo ya
watu na nchi kwa ujumla.
Amani na ushirikiano: Lugha
ya kiswahili inatumiwa sana kwenye vyo-
mbo vya habari. Vyombo vya habari uzung-
umzia mambo ambayo yanaendelea katika
nchi na hivyo basi wananchi hujua mambo
yote yanayoendelea serikalini na hii uleta am-
ani miongoni mwa watu na ushirikiano kati
kati ya wananchi na serikali.


**Kielelezo 8.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 8.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa baadhi ya hoja sahihi na kushindwa kuzitolea ufafanuzi wa kutosha hivyo kupata alama za wastani.

### 2.4.2 Swali la 9: Maendeleo ya Kiswahili

Swali lilitoka katika mada ya Maendeleo ya Kiswahili, mada ndogo ya asili ya Kiswahili. Swali lililenga kupima maarifa na lilikuwa na alama 20. Swali lilimtaka mtahiniwa atumie hoja sita zenye mifano dhahiri kueleza ubantu wa Kiswahili kwa kutumia uthibitisho wa kihistoria.

Watahiniwa 11082 sawa na asilimia 50.9 ya watahiniwa wote walifanya swali hili ambalo lilikuwa la kuchagua. Asilimia 99.9 walifaulu kwa kiwango cha wastani na zaidi. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na. 7:** *Kufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia*

Watahiniwa asilimia 92.3, walipata alama nzuri kuanzia 12 hadi 19, kwa kuwa walikuwa na maarifa kuhusu mada ya Maendeleo ya Kiswahili. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 10.3 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kutokana na kueleza ubantu wa lugha ya Kiswahili kwa uthibitisho wa kihistoria kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kueleza ubantu wa Kiswahili kwa kutoa hoja kama vile: *ugunduzi wa Ali Idris, ushahidi wa Marco Pollo, ushairi wa Kiswahili, historia ya Kilwa, maandishi ya Morice na ushahidi wa Ali Masud*. Kielelezo 9.1 ni sampuli ya majibu mazuri ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

9. Kiswahili kilianzo pwani ya afrika mashariki kabla ya ujio wa wageni. walipofika walikuta wenyeji wakizungumza kwa ~~kutumi~~ kutumia lugha yao. Katika ushahidi wa kihistoria kuna wataalamu mbalimbali walio elezea kuhusiana na Ubantu wa Kiswahili kama Ifuatavyo.

Ugunduzi wa ALI-Idris huu ni ushahidi wa kihistoria ambapo yapata mwaka 1100-1166 ambapo ~~al~~ ALI-Idrisr aligundua jina la kwanza la zanzibar kuwa ni unguja, Ali-Idris aligundua majina mbalimba ya ndizi kama vile mkono wa tembo, kisukari. huu ndio ushahidi kuwa kiswahili ni kibantu.

Ushahidi wa marco pollo huyu ni mzungu aliyetembea sehemu nyingi katika dunia na aligundua kuwa zanzibar ni kisiwa kizuri kinamzunguko wa maili 200 watu wake wananuabudu mungu, wanamfalme wao, huongea lugha yao na hawalipi kodi kwa mtu. hii inatuthibisha kuwa kiswahili ni kibantu.

Historia ya Kilwa. Katika historia hii ya kilwa inutaja majina ya utani, ambapo waliwapa wafalme wao majina ya utani kama vile Nguo nyingi ambapo waliwapa wafalmee wao ambao ni Alli Bin Hussen hii inathibitisha ~~kuwa~~ Ubantu wa kiswahili.

Ushairi wa Kiswahili huu ni uthibitisho wa Ubantu wa kiswahi kwa mara ya kwanza shairi lilitungwa kwa lugha ya kiswahili

9. Katika Shairi la Fumo Liyongo katika
Ubeti mmoja wapo kinasema
" Kimo kama mtukufu,
Mpana tena mrefu,
Majimopi yu maaru,
Watu huja humwangaliya."
hii inathibitisha kuwa kiswahili ni
kibantu.
Maandishi ya morice, morice katika
maandishi yake ametenga watu wa
pwani ya afrika mashariki katika makundi
matatu. Waafrika, wa·Waarabu
na Wasuriyama, Waafrika na wasuriyama
waliungana na kutumia lugha moja
ya Kisuriyama na pia walioana na kuza
a watoto waliitwa machotara, lugha
hiyo ya Kisuriyana inasemekana kuwa
ndiyo kiswahili cha sasa. hivyo
inathibitisha kuwa kiswahili ni kiba
ntu.
Ushahidi wa Ali-Masudi katika
Ushahidi huu Ali-masudi aliwagawa
Wazenji waliokhi pwani ya afrika
mashariki, hao wazenji ni watu wa bara
walioongea kiswahili. hii inathibiti
sha kuwa kiswahili ni kibantu.
Hivyo basi katika ~~Uth~~ Uthibitisho
wa kihistoria inadhihirisha kuwa kisw
ahili kilianza kabla ~~kuto~~ ya kufika
wageni waafrika walikuwa na lugha
yao.

**Kielelezo 9.1**: Mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Kielelezo 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu baada ya kuelezea ubantu wa Kiswahili kwa kutumia ushahidi wa kihistoria.

Watahiniwa asilimia 6.9 walipata alama za wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5 kutokana na kueleza kwa usahihi baadhi ya hoja za ubantu wa Kiswahili na kushindwa kuelezea baadhi ya hoja kuhusu ubantu wa Kiswahili kwa kutumia uthibitisho wa kihistoria. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa *ushahidi wa Marco Polo, Historia ya Kilwa na ushahidi wa Ibn Batuta* kwa usahihi na alitoa ushahidi wa kihistoria kama vile: *Ali Saidi* na *ushairi wa Kiswahili* ambao haupo kabisa katika ushahidi wa kihistoria. Vile vile, katika *ushahidi wa Al Idris* alitoa maelezo yanayohusu *ushahidi wa Ali Masoud*. Kielelezo 9.2 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kutoa baadhi ya majibu sahihi na yasiyo sahihi.

9 Kwa kutumia hoja sita na mifano dhahiri
Eleza ubantu wa kiswahili kwa kutumia
uthibiti wa kihistoria
Uthibitisho wa kiswahili kupitia kipong-
ele cha kihistoria ni kuwa lugha ya
kiswahili ni moja ya lugha ambayo inapati
kana mwambao wa Afrika mashariki, na
hii lugha asili yake kubwa ni lugha za
kibantu.
Ushahidi wa kihistoria kuhusu lugha
ya kiswahili hapa tunaangalia mambo
mbalimbali ambayo yanathibitisha kuwa
ni kweli lugha ya kiswahili asili yake
ni kibantu kwa kuonyesha baadhi ya
matukio ya kihistoria yanayothibitisha
hilo suala. Zifuatazo ni hoja zinazothibitisha
kiswahili kinatokana na lugha za kibantu
kupitia ushaidi wa kihistoria.
Historia ya kilwa - Hii ni moja ya
uthibitisho wa kiswahili kuwa lugha hii
inatokana na lugha za kibantu na kuwa
lugha ya kiswahili ili kuwepo kwani
tunaona kukutwa kwa majina ya "Mkoma
watu" na "Nguo nyingi" ambayo walipewa
sultani wa kilwa Ali ibn said na mwanae
Mohammed ibn Ali, huyo kuthibitisha
kuwa ni kweli kiswahili kinatoka na
lugha za kibantu.

9 Ushahidi wa Marco Polo. Huyu ni mzungu aliyejishughulisha na masuala mbalimbali ya kijiografia na katika maisha yake aliweza kuzunguka sehemu mbalimbali za dunia na alipata kuandika hivi "Zanzibar kisiwa kikubwa cha mali zaidi ya 200 ambapo watu wake wanaabudu mungu wao na hawalipi kodi na wanalugha zao" kutokana na maandishi hayo inathibitisha kiswahili inatokana na lugha za kibantu.

Ugunduzi wa Ali Saidi. Ugunduzi huu ulifanyika huko sicily chini ya mfalme Rogers II ambapo ulifanyika kuanzia miaka ya 1100 mpaka 1166 na katika ugunduzi wake aliweza kugundua kuwa au jina la kwanza la zanzibar ni Unguja na katika maandishi yake ameandika majina kama Muriani, mkono wa tembo, kikombe na sukari ambayo yalikuwa majina ya ndizi yanayopatikana mwambao wa pwani hivyo kuthibitisha kuwa ni kweli kiswahili inatokana na lugha za kibantu

Ushairi wa kiswahili. Huu pia ni ushahidi wa kihistoria ambao unathibitisha kuwa ni kweli lugha ya kiswahili inatokana na lugha ya kibantu kwani hapa tunaona utenzi wa Fumo Lyongo ulioandikwa katika karne ya 10 au inasadikika ambapo utenzi huu uliandikwa kwa lugha ya kiswahili ambapo hii inathibitisha kuwa ni kweli lugha ya kiswahili inatokana lugha ya

9 kibantu.

Ushahidi wa Ali Idriss. Huu pia ni ushahidi mwingine unaothibitisha kuwa lugha ya kiswahili matokana na lugha za kibantu kwani tunaona katika maandishi yake anaandika juu ya viongozi ambao ni wakilimi kuwa na viongozi ambao walitawala kutokana na nguvu za mungu, ambapo pia anandika juu ya kisiwa cha zenji kwa hiyo jina zanzibar linatona na zenjibar yaani pwani ya zenji hivyo kuthibitisha kuwa kiswahili kinatokana na lugha za kibantu.


Ushahidi wa Ibn Batuta. Huyu ni moja ya watu waliofika mwambao wa pwani ya Afrika mashariki na kuweza kuandika baadhi ya mambo ambapo katika maandishi yake aliweza kuandika kuwa "Basi tulianza safari kutoka mogadishu kuelekea pwani ya waswahili, ambapo inachukua mwendo wa siku mbili au tatu ----", hivyo kutokana na maelezo hayo kuthibitisha kuwa ni kweli kiswahili kinatokana lugha za kibantu.

Hitimisho, lugha ya kiswahili pia ina uthibitisho wa kisimu ambao unadhirisha ni kweli lugha hii ya kiswahili inatokana na lugha za kibantu ambapo kupitia huu uthibitisho mwingine unaoendana kuangalia viongezo kama vile msamiati, tungo za kiswahili na kibantu, vitenzi pamoja na irabu za kiswahili

Kielelezo 9.2 Mtahiniwa aliyepata alama za wastani

Kielelezo 9.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kueleza baadhi ya hoja sahihi na zinazostahili kuhusu ubantu wa lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, asilimia 0.8 ya watahiniwa walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kukosa maarifa kuhusu ubantu wa lugha ya Kiswahili. Wengi wao walitoa hoja za ushahidi wa kiisimu kama vile; *Msamiati, Tungo au sentensi za Kiswahili, Ngeli za majina, Upatanisho wa kisarufi na idadi ya irabu* badala ya kutoa ushahidi wa kihistoria. Kielelezo 9.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.



9. kiswahili kimegadhiliwa na wataalamu mbalimbali ili kujua asili ya kiswahili lakini Malcom Guthorine anathibitisha kuwa kiswahili ni kibantu baada ya kufanya utafiti wa maneno 2200 katika lugha 200 na kukuta maneno 500 ni ya kibantu. kutokana na hivyo ubantu wa kiswahili unathibitishwa na hoja za kihistoria zifuatazo ambazo ni

Msamiati, msamiati unathibitisha ubantu wa kiswahili kwasababu msamiati unaotumika katika lugha ya kiswahili ni sawa na msamiati wa lugha za kibantu hivyo kiswahili ni kibantu.

mfano kiswahili, baba mtu
kisukuma, bhabha moto
kindali, Tata omonto


Tungo au sentensi za kiswahili na kibantu, sentensi za kiswahili zinafanana na za kibantu kwa kiasi kikubwa kimuundo

mfano kiswahili Juma anakula ugali
kijita Juma adya obusima
kisukuma Juma alya bugali

Vitenzi, vitenzi vya vinavyotumika katika lugha ya kiswahili hivyo hivyo hutumika katika lugha za kibantu ambavyo hufanana

mfano kiswahili analima
kisukuma alolema
kindali areroma
kizigua akulima

Ngeli za majina, majina ya lugha za kibantu na lugha ya kiswahili hufanana


9. katika umoja na wingi na upatanisho wa kisarufi mfano. Umoja wingi
kiswahili mtu baba watu
mtoto watoto
kindali mntu abhantu
mwana abhana
kisukuma mnhu bhanhu
mwana bhana
Upatanisho wa kisarufi
kiswahili baba analima baba wanalima
kindali Tata aronoma abatata bharonoma.
Idadi ya irabu, idadi ya irabu hufanana ubantu wa kiswahili kwani irabu ambazo tumika katika lugha za kibantu ni sawa na za kiswahili ambazo ni a e i o u hivyo kiswahili ni kibantu.
Uishilizio ya sentensi na maneno, maneno mengi katika lugha ya kiswahili na lugha za kibantu huishia na irabu 'a' hivyo huthibitisha kuwa kiswahili ni kibantu mfano kiswahili choka
kisukuma soka
kwahiyo kutokana na ushahidi wa kihistoria unathibitisha wazi ubantu wa kiswahili kutokana na msamiati, tungo za sentensi, idadi ya irabu na ngeli za majina

**Kielelezo 9.3**: Mtahiniwa aliyepata alama za hafifu.

Kielelezo 9.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa hoja za kiisimu badala ya hoja za kihistoria kama matakwa ya swali yalivyokuwa.


## 2.5: SEHEMU E: TAFSIRI NA UKALIMANI

Sehemu hii ilikuwa na swali moja. Watahiniwa wote walipaswa kujibu swali hili. Swali lilikuwa na alama 20.

### 2.5.1 Swali la 10: Tafsiri na Ukalimani

Swali lilitoka katika mada ya Tafsiri na Ukalimani hususan katika mada ndogo ya *tafsiri* na *ukalimani* na lililenga kupima Uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja tatu za kufanana na hoja tatu za kutofautiana kati ya Ukalimani na Tafsiri.


Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (21,783) waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa swali pekee katika sehemu hii. Asilimia 99.6 ya watahiniwa waliofanya swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani. na zaidi. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya kufaulu kwa wanafunzi kiasilimia.




**Chati Na 8**: *Kufaulu kwa Watahiniwa Kiasilimia*

Asilimia 91.5 ya watahiniwa walipata alama nzuri kuanzia 12 hadi 19.5, ambapo kati yao, asilimia 11.5 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19.5 kwa kuwa waliweza kutumia hoja tatu kuonesha kufanana na hoja tatu za kutofautina kati ya Tafsiri na Ukalimani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja za kufanana kama vile: *zote zina dhima ya kufikisha ujumbe kwa jamii, zote zinasomewa katika elimu mbalimbali na zote hutumiwa kama chanzo cha ajira.* Pia, alitoa hoja tatu za kutofautiana kati ya Tafsiri na Ukalimani kama vile: *hutofautiana katika maana,*

*hutofautiana katika muda na wakati na ukalimani ni taaluma kongwe na tafsiri ni taaluma changa.* Mtahiniwa huyo aliweza kutoa utangulizi na hitimisho zuri linaloendana na swali. Kielelezo 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali vizuri na kupata alama nzuri.


10 Tafsiri ni mchakato wa uhamilishaji wa mawazo, maana na taarifa zilizopo katika maandishi kutoka Lugha chanzi kwenda Lugha Lengwa. Mfano. Go East, go west home is best - Nyumbani ni nyumbani. Hapa Lugha chanzi ni Kiingereza na Lugha Lengwa ni Kiswahili. Ukalimani ni mchakato wa uhamilishaji wa maana na taarifa zilizopo katika mazungumzo kutoka Lugha chanzi ya mzungumzaji kwenda kwa Lugha Lengwa ya hadhira. Zifuatazo ni Ufanano kati ya Tafsiri na Ukalimani, kama ifuatavyo:-

Zote zina dhima sawa katika jamii. Tafsiri na ukalimani ni taaluma ambazo kwa pamoja zina dhima sawa katika jamii. Kwani hulenga kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa na mfasiri au mkalimani. Hivyo taaluma hizi mbili hufanana katika kutoa dhima sawa katika jamii.

Zote husomewa katika elimu mbalimbali; Taaluma zote mbili katika ya Tafsiri na ukalimani ni taaluma ambazo husomewa katika elimu mbalimbali. Mfano. Vyuoni na hata katika shule za sekondari. Huwezi kuwa mfasiri au mkalimani bora pasipo kusomea taaluma hiyo kwa viwango vya juu. Hivyo Tafsiri na ukalimani ni taaluma ambazo husomewa katika elimu mbalimbali hii ndio ufanano wa taaluma hizi mbili.

Zote hutumiwa kama chanzo cha ajira; Taaluma ya Tafsiri na ukalimani hutumiwa kama chanzo cha ajira. Kwani watu husomea


10 taaluma hizi mbili kama chanzo cha ajira. Mfasiri na mkalimani huweza kuvoma taaluma hii na kuweza kupata ajira na kumpatia kipato. Mfano. Mfasiri wa kimataifa na pia mkalimani wa kimataifa huweza kupata fedha nyingi kutokana na taaluma zao. Hivyo tafsiri na ukalimani ni taaluma zinazofanana katika suala zima la ajira.

Zifuatazo ni tofauti kati ya tafsiri na ukalimani. Tofauti hizo ni kama ifuatavyo:

Hutofautiana katika maana; Tafsiri ni taaluma inayojihusisha na maandiko na ukalimani ni taaluma inayojihusisha na uzungumzaji. Hivyo tafsiri hutoa ujumbe na taarifa kwa njia ya maandishi wakati ukalimani hutoa ujumbe na taarifa kwa njia ya uzungumzaji. Hivyo hizi ndizo tofauti kati ya tafsiri na ukalimani.

Hutofautiana katika muda na wakati. Tafsiri na ukalimani hutofautiana katika suala la muda na wakati. Tafsiri inatumia muda mrefu katika kufikisha taarifa na ujumbe wake katika hadhira lengwa wakati ukalimani hautumii muda mrefu. Kwani ukalimani hutendeka muda huo huo. Hivyo basi huu ndio utofauti kati ya tafsiri na ukalimani.

Ukalimani ni taaluma kongwe na Tafsiri ni taaluma changa. Ukalimani ilitokea pale tu binadamu alipojua kuongea. Hivyo na taaluma ya ukalimani ikaanza kutumika vehemu mbalimbali. Wakati taaluma ya tafsiri ilianza baada ya kutokea kwa


10 ukalimani, na binadamu pale walipojua kuso-
ma na kuandika ndipo taaluma hii inaanza.
Hivyo ni taaluma changa. kwa hiyo hii
ndiyo tofauti kati ya tafsiri na ukalimani.
Hivyo basi taaluma zote mbili kati
ya tafsiri na ukalimani huweza kutumika
kama nyenzo ya mawasiliano baina ya watu,
kutumika katika kupatia watu ajira. Hata
hivyo taaluma hizi hukumbana na changa-
moto mbalimbali kama vile kuchelewesha
kwa fedha za malipo.

**Kielelezo 10.1**: Mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Kielelezo 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa hoja tatu za kufanana na hoja tatu za kutofautiana kati ya Tafsiri na Ukalimani kwa usahihi.

Hata hivyo, asilimia 8.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5. Hii ni kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu kufanana na kutofautiana kwa ukalimani na tafsiri. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maana ya ukalimani na tafsiri isiyo sahihi katika utangulizi wake. Pia, katika hoja za kufanana alitoa hoja kama vile: *ukalimani na tafsiri zote hutumia fasihi* ambayo ilikuwa si sahihi na katika kuonesha tofauti kati ya ukalimani na tafsiri alitoa hoja kama vile: *ukalimani huwa na fanani wawili* hoja ambayo haikuwa sahihi. Kielelezo 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyojitosheleza na kupata alama za wastani.


10 Ukalimani ni Kitendo kubadilisha maneno iliyo kutoka kwa lugha chanzi kwenda lugha lengwa kwa njia ya mazungumzo wa ~~kati~~ lugha chanzi ya mwanzo kwa Kiingereza na lugha lengwa lengwa Kiingereza lugha ya Kiswahili. Wakati tafsiri ni Kitendo cha kubadilisha maana kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa kwa njia ya maandishi mfano unabadili maneno kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili.

Ukalimani na tafsiri hufanana kwa hoja zifuatazo

Ukalimani na tafsiri zote hutumia faili kwa mfano katika Ukalimani mkalimani hutumia faili simultaneous kwa kuwasilisha mawazo yake kwa njia ya mazungumzo. Wakati mfasiri hutumia faili andishi kuwasilisha mawazo yake kwa ujumla.

Ukalimani na tafsiri hufikisha ujumbe kwa hadhira wakati Ukalimani hufikisha ujumbe kwa njia ya mazungumzo na tafsiri hufikisha ujumbe kwa hadhira kwa njia ya maandishi

Ukalimani na tafsiri huwa na ushawishi wake, wakati katika Ukalimani kuna fanani ambaye anafikishia ujumbe jamii kwa njia ya mazungumzo vile vile katika tafsiri mfasiri kuna. Fanani ambaye ndiye mwandishi mwenye ambaye anafikishia ujumbe jamii kwa njia ya maandishi



10 Ukalimani na tafsiri hutofautiana kama ifuatavyo,
Wahusika, katika kazi ya kukalimani kuna jamaa wawili jamaa wa kwanza kutoka lugha chanzi na jamaa wa pili kutoka lugha lengwa pamoja na hadhira, wakati katika tafsiri kuna jamaa mmoja tu ambaye ndiye mwandishi
Ghalama, Ukalimani hauna gharama ukilinganisha na tafsiri kwani katika ukalimani mkalimani anahitaji maandalizi ya kwenda kukalimani ilimradi awe anajua lugha chanzi wakati katika tafsiri mfasiri huhitaji maandalizi ya kutosha mfano kwa malimizi ya kamusi mbili yaani za lugha mbili husika.
Muda au suala la wakati Ukalimani huweza kufanyika kwa muda mfupi na ukaeleweka zaidi wakati suala la kufasiri linahitaji muda wa kutosha au maandalizi ya kutosha vilevile katika kazi ya ukalimani mhusika ni rahisi kumwambia jamaa kutoka lugha chanzi arudie kama neno hakusikia vizuri wakati katika kufasiri ni vigumu kumlekebisha mfasiri hata kama kuna neno limekosea.
Ukalimani na tafsiri kwa ujumla husaidia kufikisha ujumbe katika jamii vilevile kuweza kujifunza lugha au kuwa mahiri wa lugha zaidi ya moja kwa wahusika na jamii kwa ujumla.

**Kielelezo 10.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 10.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani baada ya kutoa hoja ambazo siyo sahihi kuhusu kufanana na kutofautiana kati ya Tafsiri na Ukalimani.

Aidha, asilimia 0.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha

kuhusu dhana ya ukalimani na tafsiri. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yanayoonesha tofauti kati ya ukalimani na tafsiri kama vile: *Mkalimani hutoa maana ya lugha chasili kwenda lugha lengwa*, hoja ya pili alitoa ufafanuzi usiojitosheleza na katika mfanano alitoa hoja mbili zinazofanana na kutoa maelezo yanayokinzana. Pia, alitoa hoja inayoeleza kuwa *mkalimani na mfasiri wote wanatumia matini* wakati matini hutumika kwenye uwanja wa tafsiri tu na hata hitimisho alilotoa halikuendana na swali. Kielelezo 10.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.



10. Ukalimani ni kitendo cha kutoa maana ya kitu au jambo fulani kupitia njia ya mdomo. Mkalimani hutoa maana ya kilichoongewa na mtu wa Lugha chasili kwenda lugha lengwa. Mkalimani huweza kutoa maelezo pale mtu wa Lugha chasili anapomaliza kuongea au baada ya sentensi mbili au kifungu cha maneno. Tafsiri ni kitendo cha kutoa maana ya kitu au jambo kutoka lugha chasili kwenda lugha lengwa kwa njia ya maandishi. Zifuatazo ni tofauti kati ya ukalimani na tafsiri:-

Njia: Mkalimani hutumia njia ya mdomo kutoa maana ya lugha chasili kwenda Lugha lengwa lakini kwenye tafsiri mfasiri hutumia njia ya maandishi.


Kwenye ukalimani huwa na mkalimani ambaye ndo hutoa lugha chasili kwenda Lugha lengwa na mtu wa lugha chasili ambaye anaweza kuwa labda ni mzungu lakini mfasiri huwa peke yake

Kwenye ukalimani mkalimani huonana na hadhira lakini mfasiri haonani na hadhira kwasababu huandika peke yake.

Zifuatazo ni kufanana kwa ukalimani na tafsiri:-

Mfasiri na mkalimani wote huwa mahiri wa Lugha. Wote hujua Lugha mbalimbali na huwa na muamiaji ya kutosha ya Lugha hiyo.

Mfasiri na mkalimani wote hujua Lugha chasili na lugha lengwa kwa ufasaha.


mfasiri na mkalimani hawawezi kufanya k-
azi zao kama hawajui wala hawana uma-
hiri wa lugha chasili na lengwa.
Wote huwa na matini husika.
Mkalimani na mfasiri huwa na matini
yao husika.
Kwa ujumla mfasiri na mka-
limani ni watu wa nyenzo muhimu sa-
na katika jamii lakini mfasiri ndiye huwe-
za kuamua kupeleka jamii yake kwenye md-
omo wa simba au la.

**Kielelezo 10.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 10.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuonesha kufanana na kutofautiana kati ya ukalimani na tafsiri kwa kutoa hoja zenye ufafanuzi usiojitosheleza .

## 3.0 SEHEMU YA II: MTIHANI WA KISWAHILI KARATASI YA PILI.

## 3.1 TATHMINI KWA KILA SWALI


## 3.2 SEHEMU A: FASIHI KWA UJUMLA

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ambayo yalimtaka mtahiniwa kutumia maarifa aliyojifunza katika fasihi. Mtahiniwa alipaswa kujibu swali moja. Kila swali lilikuwa na alama 20.

### 3.2.1 Swali la 1: Nadharia ya Fasihi.

Swali lilitoka katika mada ya Maendeleo ya Fasihi, mada ndogo ya nadharia ya fasihi. Swali lililenga kupima Uchambuzi na lilimtaka mtahiniwa abainishe mambo sita yanayozingatiwa na wahakiki wa kazi za fasihi katika kipengele cha mtindo.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 2,458 sawa na asilimia 11.3 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa swali la kuchagua. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo asilimia 71 walifaulu kwa kiwango cha wastani na zaidi. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 1:** *Kufaulu kwa Watahiniwa Kiasilimia*

Asilimia 53.1 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifanya vizuri na kupata alama za juu kuanzia 12 hadi 20. Aidha, asilimia 11 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 20 kwa kuwa waliweza kubainisha mambo sita yanayozingatiwa na wahakiki wa kazi ya fasihi katika kipengele cha mtindo kama vile: *Matumizi ya masimulizi*, *Matumizi ya nyimbo*, *Matumizi ya nafsi*, *Matumizi ya barua*, *Matumizi ya dayolojia na matumizi ya tenzi*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha vizuri mambo hayo sita yanayozingatiwa na wahakiki wa kazi za fasihi. Kielelezo 1.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kutokana na kubainisha mambo sita yanayozingatiwa na wahakiki wa kazi za fasihi.

1. Fasihi ni tawi la sanaa linalotumia lugha ili
kufikisha ujumbe kwa hadhira. Kuna aina mbili za
fasihi nazo ni fasihi andishi na fasihi simulizi. Uha
kiki wa kazi za fasihi umejikita zaidi katika mising
i ya fani na maudhui. Wahakiki pia katika kip
engele cha mtindo huweza kuzingatia mambo
mbalimbali. Yafuatayo ni mambo mbalimbali
yanayozingatiwa na wahakiki wa kazi za fasi
hi katika kipengele cha mtindo mambo hayo ni;

Matumizi ya masimulizi ~~Aina ya mtindo~~. mtindo hapa unaozingatiwa
huwa wahakiki wanaangalia ni aina gani ya
mtindo uliotumika. Mara nyingi hapa tunaangali
masimulizi. Mwandishi huweza kubaini kwan
za je masimulizi hayo yana ujumbe gani au
yamebeba nini. Hiyo kwanza ni aina ya mtindo.

1. Matumizi ya nyimbo. Hapa mhakiki huwe
za kuzingatia pia je kuna matumizi ya nyimbo nda
ni yake na je, nyimbo hizo zimebeba ujumbe gani
katika kazi ile. Hivyo basi wahakiki huweza kua
ngalia pia kama kuna matumizi ya nyimbo kati
ka kazi za fasihi ili kubaini mawazo makuu yaliyo
mo katika nyimbo.
Matumizi ya nafsi. Hapa mwandishi
huweza kubaini kama nafsi zote tatu zimetum
ika yaani nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu. Wa
hakiki katika kazi zao pia huweza kuzingatia ma
tumizi ya nafsi zote tatu kwani huweza kuwa nye
nzo katika kazi ya uhakiki mfano katika riwaya ya ~~Rosa~~ mistika
Matumizi ya barua. Wahakiki wa fasihi
pia huweza kuangalia ~~ni m~~ matumizi ya baru
a katika kazi zao na je barua hizo zimebeba
ujumbe gani katika kazi yake. Kwa mfano
katika tamthiliya ya "Ngoswe penzi kitovu cha
uzembe" kuna matumizi ya barua amba
yo yalikuwa na ujumbe ndani yake. Hivyo ba
rua huwa ni kipengele muhimu katika muundo
Matumizi ya dayolojia. Majibizano pia
ni kitu muhimu ambacho wahakiki huweza
kuzingatia katika kazi zao za kifasihi. dayolojia hu
weza kumfanya mhakiki aweze kuelewa na kuba
inia hisia za wahusika tofauti tofauti. Hivyo basi
matumizi ya dayolojia huwa ni muhimu. Kwa mfa
no "Ngoswe Penzi kitovu cha Uzembe" hii ni tamthi
liya yenye majibizano ndani yake kwa m
fano. Ngoswe alipo~~m~~muliza Mazoea "Umefata
nini naye akajibu kinachofuatwa" majibizano
hayo yameweza kuibua hisia za dhamira ya mapenzi

1. Matumizi ya tenzi: Mwandishi au mhakiki wa kazi ya fasihi katika kazi yake huweza kuzingatia pia matumizi ya tenzi na ushairi katika kutunga kazi zao. Kwa mfano. Katika riwaya ya na diwani mbalimbali huwa kuna tenzi ndani yake mfano diwani ya "Wasakatonge" hii ni diwani ambayo ndani yake ina tenzi hivyo wahakiki huweza kuzingatia na kubaini matumizi ya tenzi, ngonjera na hata ushairi katika kazi zao.

Hivyo basi wahakiki huwa ni watumishi muhimu katika jamii kwani huweza kubainisha na kuchambua mawazo makuu yaliyo katika jamii. Wahakiki pia hutusaidia katika kutubainishia mawazo makuu kwa wasomaji ili tuweze kubaini. Pia wahakiki ili kuhakiki kazi ya fasihi lazima wajue historia ya jamii na pia historia iliyomkuza mwandishi wa fasihi.

**Kielelezo 1.1**: Mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Kielelezo 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha mambo sita yanayozingatiwa na wahakiki wa kazi za fasihi na kupata alama za juu.

Aidha, watahiniwa asilimia 18 waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5. Watahiniwa hao waliweza kubainisha baadhi ya mambo yanayozingatiwa na wahakiki wa fasihi katika kipengele cha mtindo na kubainisha baadhi ya hoja kimakosa. Kielelezo 1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kwa usahihi baadhi ya hoja za kuthibitisha kauli hiyo kama vile: *mpangilio mzuri wa matukio* ambayo ni muundo na sio mtindo, *kuzingatia matumizi ya aya na matumizi ya lugha sanifu* mambo ambayo hayakuwa sahihi na hata utangulizi wake alitoa maana ya mtindo isiyojitosheleza hivyo kupata alama za wastani.


SEHEMU A.

1 Mhakiki; ni mtu ambaye anayepitia na kukagua kazi za kifasihi. kama zina makosa au la. na Mtindo ni namna ambavyo muandishi ameweza kuandika na kupangilia vizuri kazi yake. hivyo kwa kutumia kipengele cha mtindo yafuatayo ni mambo sita ambayo mhakiki anatakiwa kuyazingatia.

Kwanza matumizi ya Lugha Sanifu; moja kati ya mambo ambayo mhakiki anatakiwa kuzingatia ni Lugha. hivyo mhakiki anatakiwa aweze kukagua kama kazi imetumia Lugha ambayo imekubalika itumike na jamii, lakini pia Lugha hiyo isiwe ni ya matusi wala kumkera mtu hadi kufanya watu kutosoma kazi yako hivyo mhakiki anatakiwa kuzingatia Lugha sanifu.

Pili matumizi ya nafsi; hata hivyo mhakiki anatakiwa kuzingatia nafsi zilizotumika kama ni zipo sahihi au Lahaa hivyo mhakiki pia kupitia mtindo anaweza kuhakiki matumizi ya nafsi kama yapo nizuri au Lah.

Tatu Mpangilio mzuri wa matukio; Hata hivyo jambo lengine analotakiwa mhakiki kulizingatia kupitia kipengele cha mtindo ni mpangilio mzuri wa matukio na kazi iweze kueleweka kama ni Tamthilia basi anatakiwa haipange kitamthilia na kama ni riwaya pia anatakiwa azingatie masharti ya riwaya.



1 Mne matumizi ya dialojia/monolojia; hata hivyo mhakiki anatakiwa kuzingatia matumizi ya monolojia au dialojia kama mwandishi huyo amepatia au la ili kuweza kumrekebisha endapo atakuwa amekosea.

Tano matumizi ya nyimbo, barua hadithi ndani ya hadithi; hata hivyo mhakiki pia kupitia kipengele cha mtindo anatakiwa aweze kufahamu na kujua kama msanii ameweza kutumia nyimbo ndani ya hadithi, au labla barua ndani ya hadithi na hata hadithi ndani ya hadithi hivyo Mhakiki akikagua kipengele cha mtindo anatakiwa kuweza kubaini matumizi ya nyimbo, barua na hadithi.

Mwisho mhakiki anatakiwa aweze kuzingatia matumizi ya ayau' hivyo basi mwandishi itamlazimu kujua ni aya gani ambazo ametumia mwandishi. hii itaweza kumsaidia mhakiki kufanya vitu kwa ufanisi na ustadi uliokuwa mzuri

Kwa kumalizia zitajwa hapo juu ni mambo ambayo mhakiki anatakiwa kuzingatia kwa kipengele cha mtindo. kama ili vyoelezewa hapo juu lakini pia sifa moja ya mhakiki ni kutokubagua kazi za waandishi wengine. hivyo mhakiki anatakiwa kuthamini waandishi wote

**Kielelezo 1.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 1.2 Kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa utangulizi sahihi na hoja sahihi hivyo akapata alama za wastani.

Hata hivyo, asilimia 28.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha walipata alama za chini kwa kuwa hawakuwa na maarifa na uelewa wa kutosha wa mada ndogo ya Uhakiki, hivyo walieleza sifa za mhakiki wa kazi za fasihi badala ya kueleza mambo sita yanayozingatiwa na wahakiki kama vile: *matumizi ya dayolojia*, *matumizi ya monolojia*, *matumizi ya nafsi mbalimbali*, *matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi*, *matumizi ya barua na hotuba*, *matumizi ya lugha kama picha na matumizi ya majina yanayowiana na kinachozungumzwa*. Kielelezo 1.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeandika sifa za mhakiki badala ya mambo sita yanayozingatiwa na wahakiki wa fasihi.

01. Wahakiki; Ni watu ambao huchambua kazi ya fasihi kuwa ni sahihi na ina ujumbe muun kwa jamii iliyokusudiwa. Mfano riwaya, tamthi-liya, na Mashairi haya yote hutoa ujumbe kwa jamii kwa lengo la kuleta Mabadiliko na ma-endeleo kwa jamii. Yafuatayo ni Mambo yita yanayozingatiwa na wahakiki wa kazi za fasihi.

Wahakiki lazima wazingatie mazingira alikotokea Mwandishi wa kazi ya fasihi; Wahakiki ni lazima wajue Mazingira ambayo ambayo ametokea mwandishi wa kazi ambayo anaenda kuihakiki ili awe na uelewa na ujuzi wa kutambua lengo la mwandishi wa kazi ya fasihi.

Wahakiki lazima wazingatie ujuzi wa uhakiki ili kazi yo fasihi iwe imara lazima Mhakiki awe kuchambua kazi ya fasihi kwa usahihi na haya yote hutokea baada kuwo na ujuzi wa kazi ya uhakiki. kwa kupitia ujuzi mhakiki lazima ataipitia fasihi ya mwandishi kwa ufasaha na kuinchunguza itumike katika jamii iliyokusudiwa.

Wahakiki lazima wawe wamepitia kazi ya wahakiki wengine, ili kuwa na uzoefu zaidi wa kuchambua kazi ya sanaa bila ya shida yoyote. kwani wamepitia wahakiki waliota ngulia hivyo Mhakiki au wahakiki wa fasihi katika kazi zao lazima wahakiki kazi ya wahakiki wenzao waliotangulia ndipo nao wao wahakiki.

Wahakiki lazima wawe makini katika kuhakiki kazi ya fasihi; kwani ndio kazi-

Q1 Iliyobeba ujumbe na dhamira kwa jamii iliyokusudiwa na mwandishi hivyo wahakiki lazima wawe na umakini wanapochambua kazi ya fasihi.

Wahakiki lazima wawe na taaluma na moyo wa kuhakiki; kazi ya uchambuzi na uhakiki wa kazi ya fasihi ni kazi ambayo inahitaji moyo na taaluma ya uhakiki hivyo ili kuwa mhakiki bora lazima mhakiki awe kuwa na moyo na taaluma ya uhakiki.

Wahakiki lazima wachambue kwa ufasaha; Wahakiki lazima wawe kuchambua kazi ya fasihi kwa ufasaha mkubwa ili kuhakiki kazi ya mwandishi inafika salama kwa jamii iliyokusudiwa.

Kwa hivyo; Wahakiki ndio wadau wakubwa wanaofanya kazi yoyote ya fasihi ifae kwa jamii kwani wanaichambua na kufaisha kwa ajili ya jamii iliyokusudiwa.

**Kielelezo 1.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.


Kielelezo 1.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefafanua sifa za mhakiki badala ya kuandika mambo yanayozingatiwa na wahakiki wa kazi za fasihi katika kipengele cha mtindo.

### 3.2.2 Swali la 2: Fasihi kwa Ujumla

Swali lilitoka katika mada ya Maendeleo ya Fasihi, hususan mada ndogo ya nadharia ya fasihi. Swali lililenga kupima tathmini na lilimtaka mtahiniwa athibitishe kwa hoja nne kauli isemayo “Fasihi ni chombo cha jamii, kwa kuhusianisha na binadamu na ubinadamu wake”. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Asilimia 11.9 ya watahiniwa, ndio waliojibu swali hili kwa kuwa lilikuwa la kuchagua. Swali lilijibiwa vizuri ambapo asilimia 92.4 ya

watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na 2 inaonesha viwango vya kufaulu watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 2**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Takwimu zinaonesha kuwa, asilimia 63.4 ya watahiniwa walijibu swali hili vizuri na kupata alama kuanzia 12 hadi 20 kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu fasihi. Miongoni mwao, watahiniwa, asilimia 5.7 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 20 kutokana na kutoa hoja za kuthibitisha kauli isemayo "Fasihi ni chombo cha jamii, kwa kuwa hushughulika na binadamu na ubinadamu wake" kama vile: *kuelimisha jamii, huweka wazi maovu ya jamii, hudumisha utamaduni wa jamii na huhifadhi amali za jamii*. Kilelelzo 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

02. "Fasihi ni chombo cha jamii kwa kuwa huhusika na binadamu na ubinadamu wake."

Fasihi: Ni tanzu ya Sanaa inayotumia lugha kufikisha ujumbe kwa hadhira au jamii inayohusika. Kuna fasihi andishi na fasihi simulizi, Fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya Maandishi na fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya Mdomo. Kwenye fasihi kuna vipengele vya fani na Maudhui. Fani ina vipengele kama vile Mtindo, Muundo, wahusika, Mandhari, na kwenye Maudhui kuna Dhamira, Ujumbe, uhalisia na Migogoro. Zifuatazo ni hoja zinazothibitisha kuwa fasihi ni chombo cha jamii kwa kuwa hushughulika na binadamu na ubinadamu wake:-

Fasihi hushughulika na ubinadamu kwa kuelimisha jamii: Fasihi hutoa mafunzo Mbalimbali katika jamii, huelimisha jamii kuhusu Maisha ya jamii. Mfano riwaya, tamthiliya na ushairi kazi hizi zinapoandikwa huwa na lengo fulani la kuelimisha jamii, Mfano riwaya ya Mfadhili hufundisha jamii kuhusu mapenzi ya dhati, pia tamthiliya ya Morani hufundisha namna ya kujenga jamii mpya. Hivyo pia fasihi simulizi huelimisha Mfano baadhi ya hadithi na nyimbo huwa na ujumbe fulani katika jamii lakini pia Msimulizi au fanani hutumia wanyama au viumbe visivyohai kama wahusika ili kufikisha ujumbe.

Fasihi hushughulika na jamii kwa kuwa huweka wazi Maovu ya jamii: Hii ni kweli kwamba fasihi huhusika na binadamu kwani kazi nyingi za fasihi huweka wazi maovu yanayoendelea katika jamii. Mfano tamthiliya ya Kivuli kinaishi

02. Kimeonesha wazi Maovu ya jamii kama vile Rushwa, Uongozi wa kimabavu, Matabaka. Hivyo tunaona kuwa fasihi huhusika na binadamu. Lakini pia fasihi simulizi huweka wazi Maovu na Mapungufu yanayoendelea katika jamii. Mfano fanani anaposimulia au anapoimba hutoa ujumbe fulani unaolenga jamii, ambao huanika Maovu ya jamii.

Fasihi ni chombo cha jamii kwa sababu hudumisha utamaduni wa jamii; Fasihi simulizi hudumisha utamaduni kwani tunaona jamii mbalimbali za kiafrika hurithi hadithi mbalimbali na nyimbo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hivyo tunaona utamaduni wa jamii unadumu Lakini pia fasihi andishi hudumisha utamaduni pale tunapoona kazi mbalimbali zimeandikwa zinazohusu utamaduni wa jamii husika. Mfano Matambiko, hadithi, ngonjera, sogha, ngano na Miviga.

Fasihi ni chombo cha jamii kwani huhifadhi historia ya jamii; Hii ni kweli kwani kazi ya fasihi hukwenda na wakati, ndiyo Maana tunaona riwaya, tamthiliya na ushairi ni tofauti kulingana na jamii yenyewe. Mfano fasihi kabla ya uhuru (kipindi cha ukoloni) inahusu unyanyasaji na unyonyaji wa kikoloni, Baada ya uhuru inahusu shukrani na furaha ya kupata uhuru, kipindi cha Azimio La Arusha zinahusu ujamaa na kujitegemea, kipindi cha vyama vingi inahusu siasa ya vyama vingi na kipindi cha karne ya (21) ishirini na moja zinahusu matatizo kama Ukimwi (tamthiliya ya kilio chetu) Umaskini na hali ngumu ya Maisha riwaya ya watoto wa Mamantilie. Hivyo tunaona fasihi ni chombo cha jamii na inahusu binadamu.

02. Hivyo basi; Fasihi ni chombo cha jamii kwa kuwa hushughulika na binadamu na ubinadamu wake ijapokuwa fasihi huweza kutumia wahusika wanyama au viumbe visivyohai lakini hulenga binadamu. Hivyo serikali na jamii kwa ujumla wanatakiwa wahimize wanafasihi ili kupata maruno yatokanayo na fasihi.

**Kielelezo 2.1**: Mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Kielelezo 2.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyethibitisha vizuri namna fasihi kama chombo cha jamii kinavyoshughulika na binadamu na ubinadamu wake.

Aidha, asilimia 29 ya watahiniwa walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa baadhi ya hoja zisizojitosheleza kuthibitisha kauli isemayo “Fasihi ni chombo cha jamii, kwa kuwa kinashughulika na binadamu na ubinadamu wake”. Kiwango hiki cha kufaulu kinaonesha kuwa, watahiniwa wengi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu fasihi kwa kuwa katika majibu yao walishindwa kutofautisha methali na misemo na pia walishindwa kutetea hoja zao ipasavyo. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika maneno ‘‘*Asiyefanya kazi na asile*” akidhani ni methali kumbe ni msemo. Kielelezo 2.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

2 fasihi ni kazi ya Sanaa inayotumia Lugha ili kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa na kuna aina mbili ya fasihi nazo ni fasihi andishi na fasihi simulizi. Mathibitisha kauli hii kuwa fasihi ni chombo cha jamii kwa kuwa hushughulika na binadamu na ubinadamu wake kwa mifano dhairi kama ifuatavyo.

fasihi huelimisha jamii; Tunaona kuwa fasihi husaidia kuleta elimu katika jamii kwa kutumia riwaya mfano watoto wa Mama Ntilie pia vitendawili kwa ~~mfano~~ methali mfano Haba na haba ujaza kibaba hapa inaelimisha kuwa mtu anapofanya kitu na kuleta malengo taratibu taratibu mwisho huwe za kufanikiwa pia methali ya Asiye funzwa na Mamae hufunzwa na Ulimwengu.

fasihi huamasisha watu katika jamii; pia tunaona suala la Uhamasishaji wa mtu katika jamii kwa kutumia fasihi ya Kiswahili mfano methali ya Asiye fanya kazi na Asile pia hupeleka mtu kuwajibika ili tu awere kula kwa kwa methali neliyo inayo hamasisha maendeleo katika jamii ya mtu husika.

fasihi huonya na kukosoa jamii; pia tunaona kuwa suala la ukosoaji wa watu katika jamii na kuonya ndio hutili wa mkazo kwa jamii tunaona methali ya Asiye funzwa na mamaye hufunzwa na Ulimwengu, pia Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe, Sheria ni msumeno hukata huku na huko hivyo hupelekea fasihi

2 Na watu kwa uyunda kuweza kuleta hanade ya watu katika maonyo juu ya tabia zao binafsi.

fasihi huburudisha jamii pia tunaona baadhi ya fasihi za maonyesho katika jukwaa la sanaa tunaona vichekesho kama vitimbi, vioja mahakamani na Fataki hivi huleta burudani katika kazi yake na kufanya watazamaji kuburudika miongoni mwao tunaona suala hili kupitia fasihi. pia hadithi za sungura na fisi.

Hivyo basi fasihi ni chombo cha jamii kwa kuwa kushughulika na binadamu na ubinadamu wake kwa kuelimisha jamii, kihamasisha jamii, kutunza historia ya jamii, kukosoa jamii

**Kielelezo 2.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali na kushindwa kutofautisha methali na misemo.

Aidha, watahiniwa asilimia 7.6 waliofanya swali hili walishindwa kuthibitisha kauli waliyopewa hivyo kupata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu fasihi. Watahiniwa walieleza dhana zinazodhibiti uhuru wa mwandishi badala ya kuonesha namna fasihi inavyojishughulisha na binadamu na ubinadamu wake. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu ya dhana kuu za uhuru wa mwandishi kama vile: *Mwandishi kuwa huru kuitawala kazi yake, kuitawala vema lugha yake, falsafa yake na kuzungumzia wahusika anaowahitaji* badala ya kutoa hoja zinazothibitisha kauli isemayo ‘‘Fasihi ni chombo kinachoshughulika na binadamu na ubinadamu wake. Kielelezo 2.3 ni sampuli ya majibu ya


mtahiniwa aliyetoa dhana za uhuru wa mwandishi badala ya kuonesha namna fasihi inavyoshughulika na binadamu na ubinadamu wake.

2. Fasihi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha katika kufikisha ujumbe kwa hadhira yake iliyokusudiwa, Fasihi inaweza kuwa katika maandishi na inaweza kuwa katika masimulizi ya mdomo. Hivyo fasihi ni chombo cha jamii kwa kuwa hushughulika na jamii yaani binadamu na ubinadamu wake kama ifuatavyo;

Mwandishi wa kazi ya fasihi anao uhuru wa kuitawala vyema kazi; Hii ni kwamba mwandishi anakuwa huru katika kueleza matatizo yaliyopo katika jamii bila kuogopa wala kuwa na wasiwasi au ya tabaka fulani, kwahiyo kutokana na hili mwandishi anakuwa na uhuru katika kuikomboa jamii.

Mwanandishi wa kazi ya Fasihi anakuwa huru katika kuitawala vyema lugha yake; Hii huzingatia lugha anayoitumia mwanafasihi katika kuleta mabadiliko yatokanayo na ujumbe unaotolewa katika kazi hiyo ya fasihi ambayo huhusishwa na lugha, katika kutumia lugha mwandishi anatumia lugha rahisi itakayoeleweka kwa jamii na itakayo hamasisha mabadiliko.

Mwandishi anakuwa huru kuitawala vyema falsafa yake; Hii imemzungumzia mhusika mwenyewe kwa kuangalia imani yake kwa kuandika kazi yake sei mwandishi anafalsafa ya kuandika kazi zinazohusu ukombozi au mapenzi au ujenzi wa jamii mpya hii ni falsafa ya mwandishi.


2. Mwandishi anakuwa huru kuwaungumza wahusika anaowahitaji, Hivyo mwandishi anakuwa huru kwa kuchagua kulingana na kazi yake je awatumie wahusika wanadamu na wajinsia na umri gani. Mwandishi akiwa huru anaweza kutumia wahusika kama vijana kwa lengo la kusimama dhana ira zinazowalenga vijana pia wazee hivy hivyo.

Hivyo basi; Mwandishi anapokuwa huru katika kazi za fasihi anaweza kushughulikia mambo yote ya wanadamu kwa kuwaonya na kuwafundisha kutokana na uhuru alionao mwandishi juu ya jamii yake aliyoia ndikia kazi yake.

**Kielelezo 2.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kilelezo 2.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefafanua dhana za uhuru wa mwandishi badala ya kuonesha namna fasihi inavyoshughulika na binadamu, hivyo kupata alama hafifu.


### 3.3 SEHEMU B: USHAIRI

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili yaliyomtaka mtahiniwa kutumia maarifa aliyojifunza katika ushairi kujadili dhamira hasi na kufafanua miundo ya mashairi hususan katika vipengele vya muundo wa shairi. Mtahiniwa alipaswa kujibu swali moja. Kila swali lilikuwa na alama 20.

#### 3.3.1 Swali la 3: Uhakiki wa Ushairi.

Swali lilitoka katika mada ya Fasihi Andishi na lilihusu uhakiki wa vitabu teule vya ushairi. Swali lililenga kupima Tathmini na lilimtaka mtahiniwa kujadili jinsi waandishi katika diwani walivyotekeleza azma ya kupiga vita mambo yanayoweza kuzorotesha maendeleo katika jamii.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa kwa kuwa asilimia 99.4 ya watahiniwa wote walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 3 inaonesha asilimia za viwango vya kufaulu kwa watahiniwa.




**Chati Na. 3**: *Kufaulu Kwa Watahiniwa Kiasilimia*

Swali hili lilijibiwa vizuri sana kwani watahiniwa wengi, asilimia 94.2 walifaulu vizuri kwa kupata alama kuanzia 12 hadi 19. Miongoni mwao watahiniwa 16.4 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha kujadili jinsi gani mwandishi alivyoweza kupiga vita mambo yanayoweza kuzorotesha maendeleo katika jamii kama vile; *rushwa, matabaka, wizi, usaliti, umbea,*

*unafiki, umalaya, uzembe, chuki, dhuluma* na *uongozi mbaya*. Kwa mfano; mtahiniwa mmoja alitumia diwani ya "Chungu tamu" na "Kimbunga" kama kielelezo 3.1 kinavyoonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama za juu.

3. Kujadili kauli kwa kuonyesha jinsi waandishi katika diwani mbili nilizosoma walivyotekeleza azma hii kwa kutoa hoja tatu kwa kila diwani.

Kuzorotesha maendeleo katika jamii ni kurudisha nyuma maendeleo katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Mambo yanayozorotesha maendeleo katika jamii ni pamoja na rushwa, ubaguzi wa rangi, wizi, ulevi, unyanyasaji wa kijinsia na mengine katika hayo. Kwa kutumia diwani mbili ambayo ni "Chungu tamu" na "Kimbunga". Kwa kuanza na diwani ya "Chungu tamu" kama ifuatavyo:

Kuzorotesha maendeleo kwa kukandamiza haki za wanyonge. Msanii ameonyesha hili katika shairi la "Chatu na Kuku". Hili linadhihirisha wazi kuwa wenye nguvu hunyanyasa wasio na nguvu. Katika jamii yetu wapo watu wanaonyanyaswa na watu wenye nguvu. Mwandishi anawaasa wale wanaokandamiza haki za wanyonge waache kwani hurudisha nyuma maendeleo katika jamii.


Kuzorotesha maendeleo kwa kufanya ubaguzi wa rangi. Hili limeonyeshwa katika shairi la "Thomas na Doto". Msanii wa kazi ya fasihi amedhihirisha hilo kwani ubaguzi wa rangi umeonekana katika shairi hilo. Katika jamii yetu wapo watu wanaofanya ubaguzi wa rangi, hasa wazazi ambao hawapendi watoto wao waolewe na watu wenye rangi tofauti. Mwandishi anawaasa wazazi wasiwachagulie wachumba vijana wao, vijana wawe na uhuru wa kujichagulia wachumba wao ili kuwe na maisha mazuri baadaye.

3. Kuzorotesha maendeleo ya jamii kwa watu kuchagua kazi ya kufanya, katika shairi la "Dakitari Askari" mwandishi ameonyesha suala la kutokuchagua kazi ili jamii ijifunze kutoka katika kazi hii. Katika jamii yetu wapo watu wanaochagua kazi ya kufanya ndiyo maana hakuna maendeleo. Kwa hiyo mwandishi anawashauri watu wanaochagua kazi waache hiyo tabia kupitia shairi hilo kwani kuchagua kazi huzorotesha maendeleo ya jamii.

Kwa kuendelea na ~~shai~~ diwani nyingine ya Kimbunga natumia hoja zifuatazo:-

Kuzorotesha maendeleo ya jamii kwa kutoa rushwa, katika shairi la "Rushwa" mwandishi ameonyesha suala hilo kwani rushwa ni adui wa maendeleo na wa haki. Katika jamii yetu wapo watu wanaotoa rushwa na wanaopokea rushwa ndiyo maana hakuna maendeleo. Kwa hiyo mwandishi anawaasa waache tabia ya kutoa na kupokea rushwa kwani rushwa ni adui wa haki na hurudisha maendeleo ya jamii nyuma.

Kuzorotesha maendeleo ya jamii kwa wizi, katika shairi la "Paka" mwandishi ameonyesha hilo kwani wizi siyo jambo zuri katika jamii. Wapo watu ambao ni wezi katika jamii yetu. Mwandishi kupitia shairi lake anawaasa wezi waache tabia ya kuiba kwani wizi huzorotesha maendeleo katika jamii yetu, pia wajifunze kupitia shairi hili kwani linatoa mafunzo mengi na ili wezi wajirekebishe.



3. Kuzorotesha maendeleo ya jamii kwa kutumia madawa ya kulevya; Mwandishi ameonyesha hili katika Shairi la "Vijana wa Zanzibar". Hili hudhihirisha wazi kuwa vijana wengi hutumia madawa ya kulevya katika jamii yetu wapo pia vijana wanaotumia madawa ya kulevya kama vile kokeini, bangi, mirungi, sigara na madawa mengine. Mwandishi anawaasa vijana waache kutumia madawa ya kulevya kwani hupoteza nguvu kazi ya taifa kwa vijana wengi kupotera maisha yao.

Kwa hiyo; kazi mojawapo ya fasihi andishi ni kupiga vita mambo yanayoweza kuzorotesha maendeleo ~~ya~~ katika jamii, ni kweli kwani waandishi wengi wameandika mambo ambayo yanafanyika katika jamii yetu kama vile rushwa, wizi, matumizi ya madawa ya kulevya, ubaguzi wa rangi na mambo mengine kama hayo. Kwa hiyo kupitia kazi za waandishi wote wa diwani zote mbili jamii inafundishwa kuacha mambo yote yanayozorotesha maendeleo katika jamii.

**Kielelezo 3.1**: Mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Kielelezo 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali kwa kuweza kujadili jinsi mwandishi alivyoweza kupiga vita mambo yanayoweza kuzorotesha maendeleo katika jamii.

Aidha, asilimia 5.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa baadhi ya hoja ambazo maelezo yake hayakujitosheleza kujadili jinsi waandishi walivyotekeleza azma ya kupiga vita mambo yanayoweza kuzorotesha maendeleo katika jamii. Watahiniwa hawa walitoa hoja sahihi lakini walishindwa kuzitetea kikamilifu. Kielelezo 3.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutoa hoja zenye maelezo yasiyojitosheleza na kuwepo makosa ya tahajia kama vile: *anatakia vyema jamii yake* badala ya anaitakia mema jamii yake.

3. Kazi moja wapo ya fasihi andishi ni
kupiga vita mambo yanayoweza kuzorotesha
maendeleo katika jamii. Ni kweli kabisa
kutokana na kuwa mwandishi anatakia
vyema jamii yake kuwa na maendeleo mazuri
na kuishi kwa vizuri. Waandishi wa fasihi
andishi wameonesha wazi mambo hayo
kupitia ~~va~~ diwani zao mbili nazo ni:
"KIMBUNGA" ambayo ameitunga Haji Gora na
diwani ya ~~Funga~~ "FUNGATE YA UHURU" ambayo
ameiandika Mohammed S. Khatibu. Kwa
kuanzia na diwani ya "KIMBUNGA" najadili
kauli hiyo:
Suala la Rushwa: hili ni moja wapo
kati ya mambo ambayo yanazorotesha jamii
maendeleo waandishi wa fasihi andishi
wanalipigia vita suala hilo kwani haliteti
maendeleo katika jamii na suala hilo la
rushwa katika jamii zetu bado lipo na
ili tupate maendeleo mazuri katika jamii
zetu hatuna budi kuachana na jambo
hilo kwani rushwa ni adui wa haki
kama mwandishi alivyonesha wazi kupitia
shairi lake la "Rushwa" kama alivyosema:
Rushwa kayenga kambi Nakuondoka hataki
Mfanya kila vitimbi Mkaidi hashindiki
Tumzushieni wimbi Isiwe kutulubiki
Kwahiyo ili kujipatia maendeleo katika
jamii yetu hatuna budi kuachana na
suala zima la upokeaji na utoaji
Rushwa katika jamii zetu.


3. Suala la kumpiga mwanamke katika ndoa, suala hili linazorotesha maendeleo katika jamii kwani nayeye mwanamke ni mtu kama walivyo watu wengine. waandishi wa fasihi andishi wameliona hilo na wanalipigia vita kuachana na suala hilo kwani kwenye jamii zetu mambo hayo yapo mwandishi kaonesha wazi kupitia shairi lake la "Usimpige mkeo" kama anavyoeleza:

Mke hapigwi kwa fimbo wala hapigwi mateke
Hupigiwa kwa mapambo Hilondilo pigo lake
Usyahanbu mambo Utajuta mwenyewe
Kupiga piga si kwema Kaa nae kwa salama.

Suala la kuingilia Ndoa za watu jambo hili huzorotesha maendeleo katika jamii kwani suala kama hilo katika jamii zetu lipo na waandishi wanalipigia vita ili kupata maendeleo katika jamii zetu mwandishi amedhihirisha wazi kupitia shairi la "Paka Shume" kama alivyoeleza:

Paka mtaka uye watu Itakupeka ajali
Watembea kama chatu Nyumbani kwa bwana Ali
Kwani hutopata kitu Mana mwenyewe mkali
Paka chume tahadhari Isikupeke ajali

Ili tuishi vizuri katika ndoa na tupate maendeleo mazuri katika jamii hatuna budi kuachana na suala hilo.
Kwa kumalizia na diwani ya "FUNGATE YA UHURU" kama ifuatavyo:
Suala la uongozi mbaya: Ili kuepo na maendeleo katika jamii ni lazima kuw-



3 Viongozi kwa na uongozi mzuri kwani mwandishi wa fasihi wanalipigia vita suala hilo kwani haliletI maendeleo katika jamii na katika jamii yetu suala hilo bado lipo mfano katika shairi la "~~Vijana~~ ~~wa~~ Viongozi wa Afrika" kama ulivyoelezwa

Viongozi wa Afrika
Huongoza kwa Mabavu
Wao ni wachache na Werevu
Wanafiki
Wazandiki

Suala la kutokuwa na umoja na mshikamano bila ya kuwa na jambo hilo basi maendeleo hayatapatikane kwani watu washikane ili maendeleo yapatikane mwandishi anapigia vita suala hilo kwani ni kikwazo cha kuleta maendeleo na suala hilo lipo katika jamii zetu mfano: Shairi la "Unganeni"

Viongozi wa Afrika tushikane
Wafanye kazi kadhalika tuunganeni
Makaburu mnosumbuka tukutaneni

Suala la udokozi: Suala hili ni kikwazo cha kupata maendeleo katika jamii na waandishi wanalipigia vita kwa sababu katika jamii bado limo ili kupata maendeleo ni lazima tuachane na jambo hilo mfano Shairi la "Paka"

Paka nakuasa wizi
Wacha kuiba samaki.


Kwa hiyo ili kuyapata maendeleo katika jamii yetu hatuna budi kuachana na masuala hayo ambayo waandishi wanapigia vita.

**Kielelezo 3.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na makosa ya tahajia na kushindwa kutetea hoja zake kwa usahihi.

Watahiniwa 20 sawa na asilimia 0.6 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kukosea kutaja baadhi ya majina ya mashairi na wahusika hivyo, kushindwa kujadili kwa usahihi jinsi waandishi wa diwani mbili walivyopiga vita mambo yanayoweza kuzorotesha maendeleo katika jamii. Pia, walitaja majina ya wahusika ambayo hayamo kwenye vitabu walivyotumia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika jina la shairi '*Manzese na Ostabei'* badala ya "Manzese mpaka Ostabei", '*Joseph na Doto'* badala ya 'Thomas na Doto'**,** '*Mwonja Asali'* badala ya 'Usiwe Mwonja Asali' na '*Usiwe Mti Mkavu'* badala ya "Chini ya Mti Mkavu".

Pia alitaja mhusika ''Joseph'' ambaye hayupo kwenye shairi la "Thomas na Doto". Mapungufu mengine yaliyojitokeza katika majibu hayo ni: kuchanganya majina ya mashairi na majina ya diwani kama vile: shairi la "*Tumesalitiwa*" katika diwani ya "Chungu Tamu" ambalo liko diwani ya "Fungate ya Uhuru" hivyo, kupata alama hafifu. Kielelezo 3.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.


3 Fasihi andishi ni fasihi inayotumia maandishi ili kufikisha ujumbe katika jamii yake. Msanii anaweza kuandika riwaya, tamthiliya au shairi ili kulenga jambo fulani katika jamii. Kazi mojawapo ya fasihi andishi ni kupiga vita mambo yanayoweza kuzorotesha maendeleo katika jamii.

Kwa kutumia diwani mbili za "CHUNGU TAMU" ya "Theobald Mvungi" na ~~"Fungate~~ "FUNGATE YA UHURU" ya mwandishi "Mohamed S. Khatibu", Nathibitisha kuwa kazi mojawapo ~~a~~ ya fasihi andishi ni kupoga vita mambo yanayoweza kuzorotesha maendeleo katika jamii kama ifuatavyo:

Nikianza na diwani ya "CHUNGU TAMU" ya msanii "Theobald A. Mvungi", amepiga vita masuala ya Matabaka, Diwani hii ya Chungu tamu imepiga vita suala la matabaka ambapo tunaona katika mashairi ya "Manzese na Osterbei" pia "Joseph na Doto". Mwandishi amewatumia wahusika Joseph kuwakilisha tabaka la juu na sehemu Ostabei kuwakilisha sehemu ya watu wa tabaka la juu pia mhusika Doto kuwakilisha wahuwa tabaka la chini yaani maskini na sehemu Manzese. Manzese ni sehemu ambayo makazi yake yamekaa kiholela hivyo maskini ndio huishi huko Manzese

Kupiga vita uongozi mbaya, Msanii pia ameongelea kuhusu uongozi mbaya ambapo viongozi hutumia vibaya madaraka waliyonayo kwa kwa kuwanyanyasa wananchi. Haya yamedhihirishwa katika mashairi ya "tumesalitiwa" na "mwonja asali"

Kupiga vita suala la rushwa. Rushwa ni adui wa haki ya binadamu. Unapotoa rushwa unamkosesha mtu haki yake aliyotakiwa apate. Msanii ameongelea suala la kupiga vita rushwa katika "Usiwe mti mkavu"

3. Hata hivyo diwani ya "FUNGATE YA UHURU" ya mwandishi "Mohamed S. Khatibu", amekemea maovu kama:-

Kupiga vita matabaka, Diwani hii ya "FUNGATE YA UHURU" imekemea matabaka katika shairi la "CHATU NA KUKU" ambapo Chatu ndio tabaka la juu na kuku amewakilisha tabaka la chini. Siku zote tabaka la juu huwanyonya tabaka la chini.

Kupiga vita unyonyaji, Suala la unyonyaji pia limezungumziwa katika diwani hii ambapo tabaka la juu hunyonya tabaka la chini. Haya yamezungumzwa katika mashairi ya "CHATU NA KUKU" na "WAJA WA MUNGU"

Kupiga vita uongozi mbaya, Mwanii amekemea hili kupitia mashairi ya "VIONGOZI WA AFRIKA" na "WINGU". Ambapo viongozi wamekuwa wakidhulumu mali za wananchi. Suala la uongozi mbaya linakwamisha maendeleo.


**Kielelezo 3.3**:Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 3.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyekosea kuandika baadhi ya majina ya mashairi, majina ya wahusika na kuandika majina ambayo hayamo katika vitabu hivyo na kupata alama hafifu.

### 3.3.2 Swali la 4: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilitoka katika mada ya Fasihi Andishi na lilihusu uhakiki wa vitabu teule vya ushairi. Swali lililenga kupima Uchambuzi na lilimtaka mtahiniwa afafanue miundo ya mashairi katika diwani mbili alizosoma kwa kuzingatia vipengele vitatu vya msingi vya muundo wa shairi. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilikuwa la kuchagua na lilijibiwa na watahiniwa wachache 537 kati ya 21,783 waliofanya mtihani. Asilimia 50.3 ya watahiniwa hao walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 4**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 49.7 ya watahiniwa walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kushindwa kutoa ufafanuzi wa kutosha kuhusu miundo ya mashairi katika diwani walizosoma. Watahiniwa hao walifafanua swali kwa kutumia kipengele kimoja cha muundo wa shairi kinachozingatia idadi ya mishororo/mistari na kuacha vipengele vingine kama vile vina, mizani na beti hivyo kupata alama hafifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua miundo ya mashairi kama vile: *tarbia*, *tathilitha* na *sabilia katika diwani ya "*Kimbunga" na *Takhamisa*, *tarbia* na *muundo wa sabilia* katika diwani ya "Chungu Tamu" na kuacha vipengele vingine muhimu. Kielelezo 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kufafanua kipengele kimoja tu cha muundo wa mashairi.

4. Miundo ni utaratibu wa visa na matukio ya kazi ya fasihi. Katika ushairi muundo ni jinsi mwandishi anavyopanga mashairi yake katika ufamisi ili kuleta mvuto wa kazi yake. Katika diwani ya Kimbunga iliyoandikwa na HAJI GORA na diwani ya Chungu Tamu iliyoandikwa na THEOBALD MVUNGI, waandishi wamejaribu kuonyesha miundo mbalimbali waliyoitumia katika kazi zao. Kwa kuanza na diwani ya Kimbunga mwandishi ametumia miundo ifuatayo katika kazi yake.

Muundo wa tarbia, mwandishi wa diwani ya Kimbunga ametumia muundo wa tarbia ambao una jumla ya mistari minne katika kila ubeti mwandishi ameonyesha hili katika shairi la Rushwa linalosema.

" Rushwa kajenga kambi nakuondoka hataki,
Afanye kila vitimbi, mkaidi hapaidiki,

... Tumzuchiye wimbi, asipate kutuhiliki
tunyenge handaki, Rushwa tukamzike"

Katika shairi la rushwa hapo juu mwandishi ametumia mistari minne ndomana tunauita muundo wa tarbia.

Muundo wa tathilitha, pia mwandishi wa diwani ya Kimbunga Haji Gora ameweza kutumia muundo wa tathilitha ambao una jumla ya mistari mitatu kwa kila ubeti mwandishi anathibitisha hilo katika shairi la kujitawala linalosema

"Kujitawala kisomo, kupiga kubwa hatua
Kujitawala kilimo, njaa kujinasua
Kujitawala simo, njia kusimulia"

Katika shairi la kujitawala mwandishi ameweza kutumia mistari mitatu kwa kila ubeti kuthibitisha muundo wa tathilitha.

Muundo wa sabilia, pia katika diwani ya kimbunga mwandishi ameweza kutumia muundo wa sabilia ambao una jumla ya mistari mitano katika shairi la Punda pale anaposema

"Punda hakumbiki wema, hata kwa mchunga wake,
Humpa ~~mtama~~ mwingi mtama, na maji anufaike
Katu haiwi salama, shukurani zake mateke,
Huyo ndio tabia yake, kurusharusha mateke,
Kuhunga hakikushinda, mwache aende zake"

Mwandishi wa Kimbunga ameweza kutumia mistari mitano katika shairi hili katika kila ubeti mmoja wa shairi.

Kwa kumalizia na diwani ya chungu tamu

mwandishi ameweza kutumia miundombali
bali kama ifuatavyo
4 Muundo wa tarbia, katika diwani hii ya chungu tamu mwandishi ameweza kutumia muundo wa tarbia ambao unajumla ya mistari minne kwa kila ubeti katika shairi. Mwandishi amethibitisha hili katika shairi la Chungu tamu linalosema

~~Chungu tamu~~


" Katika diwani hii,
Chungu tamu si utani
Nimesema ya mwilini
na yale ya akilini"

Mwandishi ametumia mistari minne tu kufikisha ujumbe wake kwa jamii huitwa kwamuundo wa tarbia.

Muundo wa takhimisa, pia mwandishi wa diwani ya chungu tamu ameweza kutumia muundo wa takhimisa ambao unajumla ya mistari sita na kuendelea. Mwandishi anathibitisha hili katika shairi la ulanguzi anaposema

" Ulanguzi twaondoa
Adha hii ya udhia
Yaani twaichukia
Adha isije sirudia
Wote twataka kuyua
Chanzo cha hii tabia"

Katika shairi hili mwandishi ametumia mistari sita ili ujumbe wake alio kusudia uweze kufika katika jamii bila shida au tatizo lolote ukawa unaeleweka.



Muundo wa sabilia, pia mwandishi wa
Chungu tamu amemeza kutumia muundo wa
sabilia ambao unaundwa ya mistari mitano
tu. Mwandishi anathibitisha hili katika sha
iri la Kademokrasia katoweka pale mwandi
shi anaposema
" Historia ya Afrika
Kichekesho kilichotuka
Kutawaliwa na wakufika
Uhuru wa tabaka
Kademokrasi ka mwaka"
Mwandishi ametumia mistari mitano kuonye
sha au kufikisha ujumbe wake kwa jamii
inayomzunguka.
Mwisho napenda kumaliza kwa kusema
diwani hizi zote mbili zimeweza kuakisi
jamii kwa kuonyesha mambo ambayo hate
katika jamii yapo kama rushwa, usaliti, uong
ozi mbaya na uenzi wa jamii mpya.

**Kielelezo 4.1**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua miundo ya mashairi kwa usahihi kwa kuzingatia vipengele vitatu ya muundo wa shairi.

Asilimia 42.1 ya watahiniwa walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kushindwa kutoa ufafanuzi wa kutosha kuhusu baadhi ya miundo ya mashairi katika diwani walizosoma. Mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kueleza vipengele kama vile: *mizani* na *beti* lakini akashindwa *tathilitha* na *sabilia* katika diwani ya *"*Kimbunga" vilevile alifafanua swali kwa kutumia kipengele kimoja tu cha muundo wa shairi kinachozingatia idadi ya mishororo/mistari na kuacha vipengele vingine kama vile: vina, mizani na beti katika kitabu cha Chungu Tamu, hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa 8 sawa na asilimia 8.2 waliofanya swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri na kupata alama kuanzia 12 hadi 19. Miongoni mwao, asilimia 2 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kwa sababu waliweza kufafanua vizuri miundo ya mashairi katika diwani mbili walizosoma kwa kuzingatia vipengele vitatu vya msingi vya muundo wa shairi kama vile: *mizani, beti, vina* na *mishororo*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua miundo ya mashairi kwa kuzingatia vipengele vitatu kama vile: *mizani, vina* na *beti*. Kielelezo 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kutumia diwani ya "Chungu Tamu" na "Kimbunga" na kupata alama za juu.

4. Muundo ni mpangilio wa visa na matukio. Katika ushairi muundo wake hua ni kwa kuangalia mpangilio wa mistari, urari wa vina na mizani, idadi ya beti pamoja na kibwagizo au kituo katika shairi. Kwa kutumia diwani mbili yaani diwani ya "Kimbunga" iliyoandikwa na Haji Gora, pamoja na diwani ya "Chungu Tamu" iliyoandikwa na Theobald A. Mvungi. Kuna muundo mbalimbali ya mashairi imetumika. Kwa kuanza na diwani ya Chungu Tamu ifuatayo ni miundo ya shairi iliyotumika:-

Muundo na urari wa vina na mizani, Mwandishi amepanga baadhi ya mashairi yake kwa kufata urari wa vina na mizani na mengine hayakuweza kufata urari wa vina na mizani mfano katika mashairi ambayo yamefata urari wa vina na mizani ni pamoja na Tishio la binadamu na Fikra za wanyonge; kuala hili linajidhihirisha kama mshairi alivyosema katika shairi la "Tishio la Binadamu"

"Dunia yaugelea, kwenye bahari ya njaa"...
umasi na maradhi, dunia mwaipa adha.

Tunaona katika mstari wa kwanza vina vyake vya kati na vya mizani jumla ni 16. vile vile kuna mashairi kama chatu na kuku, Daktari Askari, na Manzese mpaka ustaabei hayana urari wa vina na mizani yaani vina vyao vimetofautiana na kila mstari haukua idadi ya mizani kumi na sita.

Idadi ya mistari, mwandishi ameweza

4 Kupangilia mashairi yake katika namna tofauti tofauti ya idadi ya mistari kuna mashairi ameyaweka katika idadi ya mistari mitatu, minne, tano na kuendelea. Mwandishi amejidhihirisha katika shairi lenye idadi ya mistari minne ambalo ni "Fikra za waungwana" kama linavyosema:-

"Mume wangu nakupenda, Joseph amenikuwa
Nimekula nae kunda, na nampendelea sana"...
Fikra za waungwana, Anna Kawunga ndoa"

pia kuna mashairi kama Daktari Askari, Manzese mpaka Ostabei na chelu na kuku yenyewe mistari yake mingi ni ya sabitia yaani yameweka idadi ya mistari mitano.

Idadi ya beti, Mwandishi Theobald A. Mvungi, mashairi yake mengi ameyapanga kwa namba mfano katika shairi la "Chungu Tamu" hili kalipanga katika idadi ya beti sita pia shairi la "Tishio la binadamu" Mwandishi amelipa idadi ya beti nne (4), hata hivyo mashairi hayo kuna mashairi kayaandika ni marefu hivyo yana idadi kubwa ya beti mfano wa mashairi hayo ni "chelu na kuku", Manzese mpaka ostabei, Daktari Askari na Thomas na Doto, hayo ni mashairi yenye idadi nyingi ya beti.

Pia katika diwani ya Kimbunga kuna matumizi ya muundo wa mashairi kama yafuatayo

Idadi ya beti, mwandishi Haji Gora yeye mashairi yake ameyaandika na kuyapa idadi ya beti kwa mtindo wa —

4 namba yapo ambayo yameanzia 1 mpaka namba saba (7) suala hili linajidhihirisha katika shairi la "Afrika" lina jumla ya beti nne pia kuna mashairi kama "Jaala za mkarafuu" lina idadi ya beti nyingi.


Idadi ya mistari, mwandishi wa mashairi haya mashairi yake mengi kayaweka katika muundo wa mistari minne yaani Tarbia mfano shairi la kimbunga, Afrika, kisomo cha manufaa, Mkarafuu, Kibwangai, paka na punda na mengine yote kayaweka katika muundo wa Tarbia kama inavyodhihirishwa.

Kibwangai lipoona, ni mtu kakamiliya,
Akaanza kujiuna, na dharau kuzidiya,
Wala hakujali tena, wenzio watomwambiya," ...

Hivyo basi tunaona jinsi mwandishi alivyo panga idadi ya mistari yake ili kuweza kuleta mvuto kwa msomaji;

Urari wa vina na mizani, ili shairi liweze kuimbika vizuri, shairi linapaswa kuandikwa likifata taratibu za ushairi ambayo moja wapo ni urari wa vina na mizani, katika diwani hii mshairi kaandika mashairi yake kwa kufata utaratibu wa kimapokeo yaani kuna vina vya kati na vina vya mwisho na pia idadi ya mizani imekamilika kumi na sita, suala hili linajidhihirisha pale mshairi anaposema katika shairi la "Kibwangai"

"Kibwangai lipoona, ni mtu kakamiliya
Akaanza kujiuna, na dharau kuzidiya" ...


4 Hapo tunapata vina vya kati ambavyo ni "na" na vina vya mwisho ni "ya" vile vile idadi ya mizani jumla ni kumi na sita, hivyo basi kutokana na hayo inapelekea shairi kuimbika kiurahisi.
Hivyobasi maandishi na diwani 2020 mbili yetani ya Kimbunga na Chungu Tamu wamejaribu kuibua ujumbe kwa jamii waliyo tusisitizia kuwa kutokana na mashairi yao inapelekea jamii kuamka kipitera na kuona yale mambo yanayo fanywa na viongozi na baadae kuyakemea mbala hili linajidhihirisha kwa kutumia shairi la "Chungu Tamu" na "Kibwangai".

**Kielelezo 4.2**: Mtahiniwa aliyepata alama nzuri.

Kielelezo 4.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufafanua vipengele vya muundo katika mashairi kama vile: beti, mizani na vina kama vipengele vya muundo katika mashairi.

## 3.4 SEHEMU C: RIWAYA


Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ambayo yalimtaka mtahiniwa kutumia maarifa ya riwaya aliyokuwa nayo kuonesha uhalisia wa maisha kupitia dhamira na kubainisha methali na tamathali za semi mbalimbali. Mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja. Kila swali lilikuwa na alama 20.

### 3.4.1 Swali la 5: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya Fasihi Andishi, mada ndogo ya uhakiki wa riwaya. Swali lililenga kupima Uchambuzi na lilimtaka mtahiniwa kuonesha namna dhamira za waandishi wa riwaya zinavyoonesha uhalisia wa Tanzania ya leo kwa kutoa hoja tatu katika kila kitabu katika riwaya mbili alizozosoma.

Asilimia 98.6 ya watahiniwa walifanya swali hili. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo

asilimia 99.9 walipata alama za wastani na zaidi kuanzia 7 hadi 19. Chati Na.5 inaonesha viwango vya watahiniwa vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Na.5**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 98.6 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za juu kuanzia 12 hadi 19 kwa kuwa waliweza kuonesha namna dhamira za waandishi wa riwaya zinavyoonesha uhalisia wa Tanzania ya leo. Miongoni mwao, watahiniwa asilimia 23.7 walijibu vizuri zaidi na kupata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 wengi walitoa uhalisia kama vile: *kufanya kazi kwa bidii, uongozi bora, mapenzi na ndoa, nafasi ya mwanamke, rushwa, usaliti, matabaka* na *hali ngumu ya maisha*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kuonesha dhamira zinazoakisi uhalisia wa Tanzania ya leo katika riwaya "Mfadhili" na "Usiku Utakapokwisha". Kielelezo 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu kutokana na kukidhi matakwa ya swali.


5. Dhamira ni wazo au mawazo makuu katika kazi ya fasihi. Riwaya ni kazi ya fasihi yenye mtiririko wa visa na matukio ambayo humathu uhalisia wa mambo yanayo endelea katika jamii. Kwa kuhusisha riwaya ya MFADHILI NA Hussein Tuwa na Riwaya ya WIKI UTAKAPOKUWA NA Mbunda Msokile kumeathu uhalisia wa riwaya na jamii ya Tanzania ya leo.

Kwa kuanza na riwaya ya MFADHILI kumesha uhalisia wa Tanzania ya leo.

Mapenzi na ndoa: Mwandishi Hussein Tuwa ameeleza suala mapenzi ya kweli na ya uongo pia ndoa za kweli na za uongo. Amemhusisha Mbuniko Gabi mwenye mapenzi ya kweli, Nyambuya na Jeni wenye mapenzi ya uongo. Kwa kitendo cha Nyambi kumuacha mumewe wa ndoa na kuolewa na mtu mwingine pia Jeni kumuacha Dania siku ya harusi na akiwa hospitali mgonjwa. Pia katika Tanzania kuna watu wasaliti na wenye mapenzi ya uongo kwani kesi nyingi zimeibuka za kupimaniwa na ndoa kuvunjika.

Uongozi mzuri, Msanii amejadili suala hili kwa kumhusisha mama Mlole ambaye ameonekana kiongozi bora baada ya kutatua suala la Hadi bullo la kutaint cheki feki na suala la ugomvi kati ya Dania na Hadi katika kazi pia baada ya Dania kuathiriwa na pombe baada ya kuachwa na Jeni mchumba wake siku ya harusi alibadilika na kuwa mlevi ila mama mlole alimpa likizo ya mshahara Hivyo Pia katika Tanzania kuna viongozi bora, washauri na watatuaji matatizo ya waajiriwa kwa kuwaonya na kuwarekebisha. pia wapo viongozi wenye uwezo wa kuwasaidia waajiriwa hata masuala nje na kazi.

| | |
|---|---|
| 5 | Kufanya kazi kwa bidii; Msanii H. Tuwa anaeleza jinsi Bania na Badi billah walivyokuwa wachapakazi kwani walifanya kazi kwa bidii na kwa nidhamu kubwa ila baada ya kupatwa na matatizo kiwango cha ufanisi kazini kilipungua. Pia katika Tanzania wapo vijana wachapakazi na hata wazee wenye uwezo wa kufanya kazi kwa bidii mfano ni Rais J. P. Magufuli anayesisitiza kazi na sera ya "hapa kazi tu" hivyo nwaya ni halisi. |
| | Pia katika Riwaya ya WIKI UTAKAPOKWISHA inaonesha jinsi gani ina uhalisia wa Tanzania ya leo. |
| | Suala la Rushwa; Msanii ameonesha rushwa kama kikwazo cha mafanikio kwani Mhunko CHIOKO akiwa anatafuta kazi alikuwa akiambiwa kazi zipo ila je ana chochote kama dola kwa wakubwa hupenda dola hivyo kazi haitolewi bila rushwa. Suala hili lipo pia katika Tanzania ya leo hata katika makampuni wahi hupata kazi kwa kujuana au kuwa na chochote hivyo wale wenye fedha hupata kazi ila wa hali ya chini kama CHIOKO hushia kuzurura mtaani. |
| | Hali ngumu ya maisha; Mwandishi amechimuia mandhari ya manzese wahi wa hali ya chini kueleza suala hili la ugumu wa maisha. Chioko na Goma wahusika wakuu hushi manzese kanbu na jalala, hupata mlo mmoja, kutegemea kunua karanga na kuombaomba pia. Hata katika jamii yetu ya Tanzania ya leo wapo wahi wa hali ya chini ambao huishi maisha magumu hawana chakula cha kutosha hupata mlo mmoja hasa wahi wa mitaani na mwisho kushia kuwa wezi kama Goma na kufa kwa sababu ya kupigwa na raia. |



5 Nafasi ya mwanamke katika jamii; Katika riwaya hii mwanamke amechorwa katika makundi mawili. Kwa upande wa chanya amejitokeza kama mshauri, jasiri na mwenye mapenzi ya dhati ila kwa upande ~~wa~~ hasi amejitokeza chombo cha starehe, kiumbe duni na asiye na haki. Mhusika aliyechorwa hapa ni Nelli mchumba wa Chioko ambaye anatakiwa awe uhu walae ili Chioko apate kazi. Pia katika Tanzania ya leo wapo watu wanaowachukulia wanawake upande chanya na wale wa upande hasi kama vile chombo cha starehe na kuhitimisha utu wao ili wapate kazi hasa tabaka tawala kama viongozi wa taasisi mbalimbali kuwaomiza wasichana hasa kuwapa mimba na kuwakana.

Hivyo basi, dhamira za waandishi wa riwaya zinaonesha uhalisia wa Tanzania ya leo kwani mambo yanayojadiliwa katika riwaya ndio mambo yanayotokea katika jamii na si hivyo tu pia waandishi wanapotakiwa kujadili namna za kutatua matatizo ili kuleta jamii yenye usawa na maendeleo.

**Kielelezo 5.1**: Mtahiniwa aliyepata alama nzuri.

Kielelezo 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali vizuri kwa kuonesha dhamira za waandishi wa riwaya zinavyoonesha uhalisia wa Tanzania ya leo.


Aidha, watahiniwa asilimia 0.4 waliofanya swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kwa sababu walishindwa kutoa maelezo

sahihi kwa baadhi ya hoja za kuonesha namna dhamira za waandishi zinavyoonesha uhalisia wa Tanzania ya leo. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa maelezo yasiyojitosheleza kama vile: Moja, Gadi Bulla alikuwa anatumia kilevi jambo ambalo si sahihi, pili Koplo Matata aliwasaliti wakoloni na kuwasaidia akina Denge wakati aliwasaliti Waafrika.

5. Dhamira, Ni ujumbe unaotolewa katika kazi ya fasihi andishi ili ufikie jamii fulani, Ni kweli Kwamba dhamira za waandishi wa riwaya zinaonesha uhalisia wa Tanzania ya leo, Kwa kutumia riwaya ya "Mfadhili" iliyoandikwa na HUSSEIN TUWA pamoja na "Vuta N'kuvute" iliyoandikwa na SHAFI ADAM SHAFI, waandishi wote wameonesha dhamira zenye uhalisia, Kwa kuanza na kitabu cha "Mfadhili" ameonesha kama ifuatavyo:-

Suala la ulevi, Mwandishi wa riwaya hii ameonesha suala la ulevi kwa kumtumia mhusika Dania pamoja na Gaddi Bullah. Dania alikuwa akitumia pombe yenye kilevi kikali baada ya kuachwa na mpenzi wako jerry ambaye baadaye ilikuja kumsababishia matatizo ya Ini, pia Gaddi nae alikuwa anatumia kilevi baada ya kusalitiwa na mke wako Nyambuja na kwenda kuolewa na rafiki yake Gaddi. Kwahiyo ulevi si jambo zuri kabisa kwani unarudisha nyuma maendeleo, na kupata matatizo ya mwili.

Suala la usaliti, Usaliti si jambo zuri kabisa kwa maisha yetu, kwani ni kwenda kinyume na makubaliano ya mwenzio, Mwandishi amemtumia mhusika, Jerry, Dania pamoja na Nyambura, Jerry alimsaliti Dania wakati wa hanisi yao na kumkimbia, pia pale Dania alipohitaji msaada wa Ini jerry alimkimbia Dania na kumuacha hospitali, pia Dania alimsaliti Gaddi na kurudiana na Jerry. Kwahiyo mwandishi ameonesha kuwa usaliti ni uhalisia wa maisha ya leo ya Tanzania.



5. Suala la Dharau, Mwandishi amemtumia m
husika Dania, kwani Dania alikuwa mtu mwe
nye dharau sana alikuwa akimdharau Gaddi ambae
alikuwa kiongozi wako, alikuwa akimwambia afany
e kazi / kuandaa ripoti ya kikao Dania alimdharau
na kuondoka zake, Pia alimdharau pale Gaddi a
limkuta hotelini akiwa na mwanae Junior na k
umwacha pale Gaddi na kuondoka zao.
Siyo tu mwandishi HUSSEIN TUWA ameonesha
dhamira zenye uhalisia bali mwandishi SHAFI AD
AM SHAFI naye ameonesha kwa hoja zifuatazo:-
Kushikilia mila na Dhana potofu, Hili ni s
uala baya kwani bado zipo jamii ambazo bad
o zinashikilia ukale, Kama wazazi wake Yasmin
waliamua kumuozesha yasmini kwa mtu asiyo
mpenda na alikuwa mkubwa kwake ambaye ni
Bwana Raza, Pia hata shibab alikuwa akiami
ni mila na dhana potofu kwani alimuweka yas
mini Utawani, kitendo ambacho yasmini akufu
rahishwa nacho.
Suala la usaliti, Mwandishi ameonesha
hili kwani si suala zuri na lakuigwa amem
tumia mhusika Koplo Matata ambaye aliwasali
ti wakoloni wenzake na kuwasaidia wapigania w
a uhuru ambao ni kina Denge, Mambo, Saleh pa
moja na yasmini na Mwajuma, Pia hata Yasmini
alimsaliti Koplo Matata kwa kumwambia ampe
siri na hata mwambia Denge lakini yasmini
alimsaliti na kumpelekea Denge karafasi aisom
e. Kwahiyo suala la usaliti ni jambo am
balo si la kufuata, pia wapo watu katika
jamii yetu wanaosaliti.

**Kielelezo 5.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Asilimia 1.0 ya watahiniwa walipata alama dhaifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kushindwa kutetea hoja zao kulingana na swali. Walitoa baadhi ya hoja dhaifu sana kwa mfano migogoro na ujumbe badala ya kutumia dhamira mbalimbali katika kuonesha uhalisia wa Tanzania ya leo. Kielelezo 5.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

5. Riwaya zi kitashiki ni
Chombo kinacho onesha uhalisi
a wa Jamii jinsi ulivyo leo,
katika Inchi ya Tanzania, kwani
kuna migogoro Mbalimbali inayo
ikumba jamii ya kitanzania
Mfano Umaskini, Swala la
Mapenzi, chuki, udalili. hivyo
Waandishi wa riwaya huzichonga
kwa namna zao, kuonesha uhali
na jinsi ulivyo. kwa kuzingatia
Riwaye mbili ambazo ni "Mfadhili
Tamba na "Vuta n' kuvute". nayeza
kuhakiki kauli hii. kwa kuanza
Na riwaye ya "Mfadhili"
Mfadhili ni riwaya iliyo
andikwa na "Hussein Tuwa" akio
ngelea swala la Mapenzi na
Ndoa, jinsi livyo ikumba jamii
ya kitanzania, na kurudisha
nyuma Maendeleo, alitumia

5 Wahusika kama vile Gaddi Ballah na Dania hawakuweza kuonesha jinsi mapenzi yanavyoweza kuumiza, hakika pia, ndoa ambazo si za kweli, kama ndoa ya Dania na Jerry. Hivyo riwaya hii inaonesha uhalisia wa Tanzania kupitia dhamira zilizojitokeza katika riwaya hii, kama ilivyo elezwa hapa chini.

Dhamira, katika riwaya hii kuna dhamira mbalimbali kubwa ikiwa ni Mapenzi na ndoa ambapo Msanii ameonyesha Mapenzi ya kweli yaliyo kuwa kati ya Gaddi Ballah na Dania na pia Gaddi kwa Nzambaya na pia Mama Nilole kwa Gaddi na Dania kwa kuwasaidia wao kukuzwa kazi. Pia mapenzi kati ya Nunu kwa Dani kuonesha kumsaidia Dania kipindi chote cha shida yake. Pia, kuna dhamira kama usaliti alio ufanya Nzambaya kwa Gaddi, pia kuna uongozi Uzuri alionyesha Mama Nilole. Hivyo hali iliyojitokeza kati ~~dhana~~ riwaya hii kupitia dhamira zake ni kweli. halisi ya Kitanzania. hivyo tunaweza kuona kweli tupu kupitia riwaya hii.


5 Ujumbe: Mafunzo mbali
Mbali tunafunzwa kupitia
riwaya hii. Mfano, "Rafiki wa
kweli ni yule wa shida na
raha". Mfano Nuru alivyo weza
kumsaidia Dania na kuwa naye
katika kipindi cha shida na raha.
Pia, "Si kila king'aacho ni dhahabu"
ambapo Dania alimpenda Jerry
Jinsi alivyo Mtanashati, Mcheshi
lakini, kumbe ni kwa ajili tu
ya kupeleka Mafatiro kwa Dania.
Baada ya kugundua kuwa hana
Mapenzi ya dhati, kwa kumtoa
roka kipindi chandoa na kum
kimbia kipindi anaumwa. Pia
Ujumbe Mwingine ni kwamba, "Ni
vigumu kumpata Mtu Mwenye
Mapenzi ya dhati" katika duni
a ya sasa. Mfano Gaddi alivyo sali
tiwa na Wanawake wote mpaka Dania
na Nyambura. hivyo kinyemelea
hali hii ipo kweli, katika
jamii ya sasa ya Kitanzania.
Mgogoro: Ni kutoelewana kwa
na uelewano baina ya pande
Mbili, kuli kuwa na Mgogoro
kati ya Gaddi na Nyambura,
baada ya Nyambura kumkataa
Gaddi. Pia kuli kuwa na Mgogo
ro kati ya Gaddi na Dania
baada ya Gaddi kumlikiorisi

5 Ya Dani, pia kama Ngoso
go yule kiafsi alikuwa ndi
Gadi, baada ya kuachwa na
Nyambaga, Mkewe na pia
Dani alikuwa na Ngogoro
na kiafsi, na wote kupinga
vinywaji vikali baada ya kuo
ngwaywa na Jerry. Hivyo basi
Ngogoro hii ipo / pia / katika
Jamii ya leo ya kitanzania
Hivyo kwasasa riwaya
Hii inaonesha uhalisia na kitanz
ania ulivyo.
Kwa kumalizia, riwaya
ya "Vuta N' kuvute" iliyo
Andikwa na "Shafi Adamu
Shafi" akieleza suala la
Ukombozi, Ukombozi wa kifa
Madani, Ukombozi wa kisiasa
na kifikra, Ambapo alieleza
Mzee Kitwana kama Yasmin
Denge, Mwajuma, Bukene Kuza
Inspekta Hamid na Bhoke kuonesha
suala la Ukombozi, ambapo Yasmin
alikuwa akijikomboa na tamaduni
zilizo pitwa na wakati pia
Denge kupinga suala la ukoloni
kwa kusambaza Makaratasi
yaliyo na Uhibe wa kupinga
ukoloni huo. Hivyo kwa sasa
Tanzania bado ipo na hali ya
ukoloni Mamboleo, kwani ulevi

5 lilio ngao ni wa kibendele, na bado tamaduni za zamani zinaendelea Mfano kabila la kimasai bado kuna ukeketaji, na pia Ndoa za kulazimisha watoto wadogo. Hivyo kupitia Riwaya hii kuna dhamira mbalimbali zilizotolewa kwa zikionesha uhalisia wa kitanzania kama zifuatazo.

Dhamira, kuna dhamira ya ukombozi, ambapo kuna ukombozi wa kifikra alioonesha Yasmin kwa kujitambua, na pia kuna ukombozi wa kiuchumi alioonesha Denge kwa kupinga unyonyaji wao kwa wakoloni na pia ukombozi wa kisiasa alioonesha Denge kwa kupinga ukoloni na kusambaza magazeti yenye ujumbe unaofundisha. Pia kuna dhamira kama usaliti jinsi Yasmini alivyo msaliti bwana Raza, na koplo Matata, Pia umaskini alivyooneshwa Mwajuma rafiki yake Yasmin kuishi kwa shida, hali ngumu, na pia Matabaka yaliyo kuwepo kati ya wazungu (Wageni weupe), wahindi, kwa Bwana Raza, na waafrika kama Denge, Mwajuma na Mambo. Hivyo Dhamira zilizojitokeza katika riwaya Hii inaonesha uhalisia uliopo wa kitanzania. Mfano Matabaka.

5 Ujumbe, Mafunzo tunayo-
yapata ni kwamba la Mapenzi
waadhirio wanao pendana Mfano
Yasmini kulazimishwa na wazazi
wake kuolewa na bwana raza
aliye kuwa Umri sawa na baba
yake Miaka hamsini na Yasmi-
ni ni kigori wa Miaka kumi na
tano. Mwandishi anasema "Yasmini
alilazimishwa kuolewa na Mtu
aliye kuwa sawa na Umri wa baba
yake 50 miaka na Yasmini akiwa
ni kigori wa Miaka 15". Pia kuna
"Umoja na Mshikamano ni nguzo ya
kujenga taifa" hii ni pale Deng
Na kundi lake waliokuwa
Na Umoja katika kupinga
Ugonjwa. hivyo Umoja ni nguzo na
Ugangano ni Udhaifu. kwani walisimama
kwa na Umoja wakafanikiwa kuiza.
Hivyo kwa jumbe hizi pia zinadhi...
na kati kati ya kitanzania ya
leo jinsi tuliyo na Umoja pia
kupinga tamaduni zilizo pitwa na
wakati kupitia chini ya Umoja wa Wanawake
Tanzania (UWT).
Migogoro, kuli kuwa
Na Migogoro, kama vile. Mgogoro
ni wa ... ukale na usasa" ambao
apo Yasmini alikuwa akipinga wazazi
wake kuolewa na bwana Raza
pia Yasmini alipinga ndoa ya




**Kielelezo 5.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 5.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kikamilifu na kupata alama hafifu.

### 3.4.2 Swali la 6: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya Fasihi Andishi, mada ndogo ya Uhakiki wa vitabu vya riwaya. Swali lililenga kupima Uchambuzi na lilimtaka mtahiniwa abainishe methali tatu na tamathali za semi tatu kwa kila kitabu, kisha aoneshe jinsi zilivyotumiwa na waandishi wa riwaya mbili alizosoma kama zana za kutolea ujumbe kwa jamii na lilikuwa na alama 20.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 0.4 ya watahiniwa kwa kuwa lilikuwa la kuchagua. Miongoni mwao asilimia 98.8 walijibu vizuri na kufaulu kwa kiwango cha wastani na zaidi. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 6**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 83 sawa na asilimia 0.4 walijibu swali hili na kupata alama nzuri kuanzia 12 hadi 19. Miongoni mwao watahiniwa 69 sawa na asilimia 83.1 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kwa kuwa waliweza kubainisha methali tatu na tamathali tatu za semi kwa kila kitabu kisha kuonesha jinsi zilivyotumiwa na waandishi wa riwaya kama zana za kutolea ujumbe uliokusudiwa kwa jamii zao. Watahiniwa walipata alama za juu japokuwa walikuwa na mapungufu machache ya kuchanganya tamathali za semi, semi na misemo katika majibu yao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutumia methali tatu kama vile: *asiyekujua hakuthamini, umoja ni nguvu utengano ni udhaifu na alipo kilema usikunje kidole* na tamathali mbili za semi

kama vile: *tashibiha na tashihisi* kutoka katika riwaya ya Usiku Utakapokwisha. Pia, aliandika methali kama vile: *subira yavuta heri na umoja ni nguvu utengano ni udhaifu* na tamathali za semi kama vile: *tanakali sauti, takriri na tabaini* katika kitabu cha Vuta N'kuvute kama zana za kutolea ujumbe uliokusudiwa. Kielelezo 6.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu kwa usahihi swali hili na kupata alama za juu.

6 Methali ni semi fupifupi za mafumbo zenye kuelezea maisha na maadili ya jamii. semi hizi huwa na lengo la kuasa, kuelimisha na kuonya kuhusu mambo mbalimbali na maadili pia maisha ya wanajamii mfano:- "Asiyesikia la mkuu huvunjika guu". Tamathali za Semi ni semi za mafumbo zenye kutoa maana fulani iliyojificha.

Kwa kuanza na riwaya ya USIKU UTAKAPOKWISHA iliyoandikwa na MBUNDA MSOKILE methali zilizojitokeza ni.

"Asiyekujua hakuthamini" haya ni maneno yaliyoongelewa na watu baada ya dereva kumsukuma na kumfukuza mwanamke aliyetaka kupita mlango wa dereva lakini dereva akamkataa pia utingo alimfukuza mama mjamzito aliyemuomba kupita mlango wa kutokea kwenye gari kwani asingeweza kupita kwenye mlango wa kuingilia lakini utingo alimsukuma kwa nguvu. hivyo methali hiyo imeonyesha zana ya kuwa mtu asiye kujua haweri kukuthamini wala kukusaidia.

"Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu" haya ni maneno yaliyoongelewa na wafanya biashara wadogowadogo na wauza njugu kama njia ya kujipa matumaini na moyo wa kufanya biashara zao na kutokuogopa wanamgambo methali hii imetoa zana na ujumbe wa kuwa tunapaswa kushirikiana na kuungana katika kila jambo ili tuweze kufanikiwa. na kuepuka vikwazo.

"Alipo kilema usikunje kidole" haya ni maneno yaliyoongelewa na Chioko wakati akifik

6. inia umaskini wao na maisha wanayoishi zana
hii inatoa ujumbe kuwa pale kwenye tatizo au
shida yakupasa kuitatua na sio kujipweteka
pia yakupasa kuwasaidia wenye shida.

Tamathali za semi zilizojitokeza katika kitabu hiki ni:-

Tashhisi, "Fedha zinacheka mifukoni mwangu" maneno haya yaliongelewa na kuoneka na kwenye barua aliyoandika chuchu kwenda kwa Gonza na chioko akieleza jinsi alivyo na pesa nyingi na kwamba amefanikiwa katika maisha zana hii imetoa ujumbe wa kuwa ukiwa na pesa kila kitu kwako huwa rahisi na huwa na furaha.

Tashbiha, "ni maneno yanayolinganisha vitu viwili kwa kutumia maneno "kama", "mithili ya" mfano:- "Maghorofa yamesimama barabarani kama askari wa kikoloni". haya ni maneno yaliyoongelewa na Chioko akiwa dirishani usiku akiangalia mataa yanavyomulika mji na kufikiria maisha yao na huku akiangaza kumsubiria mpenzi wake Nelli zana hii inatoa ujumbe kuwa mji hutulia zaidi wakati wa usiku.

Ritifaa, "hii imejitokeza pale chioko alipokuwa akiangalia maiti ya Gonza ikiwa imelala chini na kuanza kuzungumza nayo "Kwanini hukuwa mvumilivu kwanini hukusubiri, ona sasa umejitafutia mauti, kwanini hukutumia njia sahihi mbona umeniacha peke yangu" chioko alikuwa akiilalamikia maiti ya Gonza ambayo ilikuwa haisiki chochote na wala isingeweza kumjibu, zana hii inatoa ujumbe wa kuwa watu wanapaswa kuwa wavumilivu na kutumia njia sahihi katika kujiletea maendeleo.

6. Kwa kumalizia na riwaya ya VUTA N'KUVUTE iliyoandikwa na SHAFI ADAM SHAFI inaeleza methali hizo ni.


"Asiyekubali kushindwa si mshinda ni" haya ni maneno yaliyoongelewa na Mambo kipindi Denge yupo gerezani alipongea hayo kwa Yasmin ili kumpa moyo wa kupambana na kumsaidia Denge kutoka. zana hii inatoa ujumbe kuwa huwezi kufanikiwa bila ya kushindwa ama kuanguka ili uweze kujifunza zaidi.

"Umoja ni nguvu" haya ni maneno yaliyoongelewa na Mambo akimwambia Yasmin kwamba wanatakiwa kushirikiana kwa kila hali ili waweze kumtoa Denge gerezani. zana hii inatoa ujumbe kuwa ili kuweza kufanikisha jambo tunatakiwa kuungana kwa pamoja ili kulishinda

"Subira yavuta heri" haya ni maneno yaliyoongelewa na Bukheti baada ya kumuoa Yasmin. zana hii inatoa ujumbe wa kuwa inatakiwa tuwe wavumilivu katika kila jambo tunalo lihitaji.

Tamathali za semi zilizojitokeza katika riwaya hii ni :-

Tabaini au msemo, "sina shoga, sina rafiki, sina jirani, sina jamaa, mimi ndani, ndani na mimi". haya ni maneno yaliyoongelewa na Yasmin wakati yupo Tanga kwa shihab alipowekwa uta wani, tabaini nyingine ni kama "mseto si mseto", "hansi si hansi" zana hii inatoa ujumbe kuwa kumuweka mke utawani kunamfanya awe mnyonge, mpweke na asiye na furaha pia humnyima haki na ni dhana potofu.



6. Tanakali sauti, "ngo! ngo! ngo!, hii ni ~~hii ni~~ pale Yasmin ~~mlio wa mlango~~ alipokuwa akigonga mlango wa Mwajuma. Zana hii inatoa ujumbe kuwa yatupasa kubisha hodi katika majumba ya watu kabla ya kuingia.

Takriri, "Yasmin, Yasmin, Yasmin ndio nani hapa" haya ni maneno yaliyoongelewa na mjomba wake Yasmin hakutaka kuongelea habari za Yasmin. Zana hii inatoa ujumbe wa kuwa watu hurudiarudia maneno ili kutoa msisitizo wa wanachokiongea.

Hivyo basi, methali na tamathali za semi hutumiwa na wasanii wa kazi za fasihi kama zana za kutolea ujumbe uliokusudiwa.

**Kielelezo 6.1**: Mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Kielelezo 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali vizuri na kupata alama za juu.

Aidha, watahiniwa 13 sawa na asilimia 15.7 walijibu swali hili na kupata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kuchanganya methali na nahau na kutoa hoja ambazo hazikujitosheleza katika kubainisha methali na tamathali za semi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alipata alama za wastani kutokana na kutumia nahau "*Kumpaka mafuta kwa mgongo wa chupa*" ambayo si methali. Pia, alitumia methali "*Umoja ni nguvu"* katika riwaya ya "Kufikirika" wakati hakuna methali hiyo na pia alikosea kuandika tashibiha kwa kuandika "*Kichwa chake kimeshindiliwa kama mfuko*" badala "*Kichwa*

*chake kimeshindiliwa kama gunia".* Kielelezo 6.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.


6. Wasanii wa kazi ya fasihi hutumia kipengele cha lugha kama tamathali za semi na methali ili kuweza kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kuwasilishwa kwa jamii kama vile kukoroa na kuona kathibitisha dai hili kwa kutumia vitabu vya VUTA N'KUVUTE iliyoandikwa na SHAFI ADAMU SHAFI na KUFIKIRKA iliyoandikwa na SHAABANI ROBART katika kuonyesha jinsi walivyotumia tamathali za semi katika kutoa ujumbe kwa jamii kwa kuanza na kitabu cha VUTA NIKUVUTE kama itavyotavyo Methali kama zitavyotavyo

Heri nusu shari kuliko shari kamili, Mwandishi wa riwaya ametumia methali hii katika kutoa ujumbe kwa jamii kuliko mtu kutaka shari kubwa bora shari dogo kwa mfano Mhusika Yasmin aliyakuwa heri nusu shari kuliko shari kamili na katika jamii zetu huwa la kama hili lipo linatakiwa tuliendeleze katika jamii zetu

Mzoea punda hapandi farasi, mwandishi ametumia methali hii katika kutoa ujumbe kwa wanajamii kwamba mtu akizoea kufanya jambo fulani hawezi kufanya jambo lingine katika maisha yake. Mfano Mhusika Mwajuma alizoea kwa chombo cha starehe kwa wanaume kwa kukidhi haja zao hivyo akiambia a cha kufanya na pia katika ja

5 mii zetu ziwe kama hivi hivyo zinavyotakiwa
tuliupige vita katika jamii
Kimpaka Matata kwa mgongo wa cha
pa', Mwandishi ametumia methali hii
kwa lengo la kutoa ujumbe kwa jamii
mfano katika kitabu kopo Matata ali
kuwa anawapaka Matata waatika ku
u kwa dhahara kwa wazungu hivyo k
atika jamii zetu ziwe kama hivyo
zinavyotakiwa tuliupige vita na pia ame
nesha tamathali za semi kama zitoa
ayo
Tashibiha, ni ulinganishaji wa
vitu viwili kwa kutumia viunganishi
Mfano Ameba nacho kama chai
Mweupe kama mgonjwa wa safura na
pia Kisura rara alikaa kwenye kiti
amevimba kama kiboko kwa kutu
mia tamathali za semi hii ametika
ta ujumbe kwa kuzatoririka kuto
ana vitu vidogo vinavyotokea katika
ajamii
Tashihisi, njia ya kuvipa vitu vi
ivyo na uhai matendo ya binadam
u Mfano Nuru ya chai ilio ilijaza
ndani na kumulika kila kilichopo ki
cha katika nyumba. Msani ametumi
a tamathali ya semi hii kwa kuto
6 ujumbe kwa lugha ya picha kwa jami
ya leo kumilika vitu vibaya vilivyo
jificha kama matatizo na chalifi na
pamoja na umasikini

6. Tabaini, ni aina ya tamathali ya semi
inayoonyesha ukinzano katika ya pande mbili
Mfano Hatua si Hatua, Ugali si ugali
moto si moto na vina ndugu, vinafaa
ni mimi na ndani ainaya kinadingo
tena Mwandishi anetoa ~~t~~ ujumbe kwa
jamii kwamba tusibague tamba pindi
tunapokuwa tumefikwa na matatizo mba
limbali katika jamii Mbali na VUTANI
kuvuta pia kuna KUFIRIKIRIKA ime
onesha methali kama ilivyotajwa
Nyumba ya Mgumba haina vyota
ngoi. Mwandishi ametumia methali
hii kwa kutoa ujumbe kwa jamii ku
amba nyumba ya mtu asiyezaa haina
kuambelea katika jamii yetu hivyo
katika jamii zetu sisi kama hii tio
o tunatakiwa tuipenda vile.
Mwenye kuzi kazi Mwandishi
ametumia methali hii kwa kutoa uju
mbe kwa jamii yake katika kuonyesha
suala la kuwa na haya wa kila kitu
ni kuweza kupata matunda yake hivyo
o ni lazima tupambane kwa kila hali
ili kupata matunda ya kitu fulani mai
shani
~~Mtiha~~
~~Damu~~ ni umojani nguvu utenganodha
~~Mchika mawili moja humponyoka;~~
Mwandishi ametumia methali hii kwa kuto
a ujumbe kwa jamii mchika mawili moja
hivyo waganga waliishirikiana katika mathabu ya



**Kielelezo 6.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache asilimia 1.2 waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6 kutokana na kushindwa kubainisha methali tatu na tamathali za semi tatu kwa kila riwaya mbili alizosoma. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kujibu kwa usahihi swali hili kwa kuwa alikosea kuandika methali “Mzoea punda hupanda farasi” badala ya “Mzoea punda hapandi farasi” na kuelezea kimakosa, ametumia tamathali za semi mbili na hakuzitolea ufafanuzi na katika utangulizi wake alishindwa kufafanua kwa usahihi maana ya methali na hakutoa kabisa maana ya tamathali za semi pia hakuwa na hitimisho. Kielelezo 6.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa kuandika majibu kinyume na matakwa ya swali.

6 Tamathali za semi nyingine ni utani ambapo Msanii anaonesha
"Ama kweli dunia ni ikowtwani"

Bali na Riwaya hiyo Tunaona Riwaya ya VUTA NI' KUVUTE Mwandishi ametumia methali na Tamathali za semi
Mwandishi ametumia Methali kama vile "Asiyekubali kushindwa si mshindani" Tunaona katika riwaya hii mwandishi ameitumia ili kufikisha ujumbe
Methali nyingine ni "Ni bora nusu kuliko shari kamili" ambapo ametumia ili kufikisha ujumbe kwa watu.
Pia methali nyingine ni "Mzoea farasi hupanda farasi" hii ameonesha kufikisha ujumbe kwa jamii
Zifuatazo ni Tamathali za semi kama ifuatavyo
Mwandishi ametumia Tashibiha ambapo anasema
"Bwana Raza ametoa tumbo ya kitambi amevimba kama kiboko!"
Pia Tashibiha nyingine ni "kijana yule aliyetoa macho kama kurunzi"
Tamathali nyingine ni Tashihisi ambapo anasema
"chumbani mle wadudu walitawala hawaoni na mbu walitanua kusindikiza kwa kelele yao"
Tamathali nyingine ni Tabaini anasema
~~"Hatua si hatua ugali si ugali"~~
"Hatua si hatua msito si msito ugali si ugali"

6 Methali ni maneno yenye hekima katika Jamii katika riwaya ya MFADHILI Mwandishi ameonesha Methali na Tamathali za semi kama dhana kutolea ujumbe uliokusudiwa.

Katika riwaya ya Mfadhili Mwandishi ameonesha ~~Tamat~~ Methali ya Heri nusu kuliko shari kamili katika Tamathali hii mwandishi ameonesha kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa Jamii

Methali nyingine ni "ukiyastaajabu ya Musa utayaona firauni" pia Msanii ametumia Methali hii kufikishi ujumbe kwa watu na Jamii inayomzunguka Mwandishi

Methali nyingine ni Mkaidi hafaidi mpaka siku ya Iddi msanii ametumia kufikisha ujumbe kwa watu wale ambao ni wakaidi hawafuati maelekezo kwa wazazi wao.

Zifuatazo ni Tamathali za semi katika riwaya hii

Mwandishi ametumia Tashbiha kuonesha kulinganisha vitu mbalimbali katika riwaya hii ametumia Tashbiha hii inayosema

"paa lake lililojengwa kwa mithili ya dobo la lile dege aina ya concord"

pia ametumia Tashbiha nyingine inayosema "Gari liliruka mbele kama Tiae na kuanza timua vumbi"

Tamathali nyingine ni Tashihisi ambapo Msanii anaonyesha

"Moyo wa nuru uliruka sarakasi na kuanza kukimbia mbio".

**Kielelezo 6.3** Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 6.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha methali tatu na tamathali za semi tatu hivyo kushindwa kuonesha jinsi zilivyotumiwa na waandishi kama zana za kutolea ujumbe.


### 3.5 SEHEMU D: TAMTHILIYA

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ambayo yalimtaka mtahiniwa kutumia maarifa aliyopata katika vitabu vya tamthiliya kuonesha mambo yanayofaa na yasiyofaa kuigwa pamoja na kufafanua wasifu wa wahusika kwa kulinganisha na wazo kuu la mwandishi. Mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja. Kila swali lilikuwa na alama 20.

#### 3.5.1 Swali la 7: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali lilitoka mada ya Fasihi Andishi na lilihusu uhakiki wa vitabu teule vya tamthiliya. Swali lilimtaka mtahiniwa afafanue mambo mawili yanayofaa na mawili yasiyofaa kuigwa katika fasihi kama yalivyoainishwa katika tamthiliya mbili alizosoma.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na watahiniwa wengi 95.2%. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa hao kilikuwa kizuri ambapo, asilimia 99.6 ya waliojibu swali hili walipata alama za wastani na za juu. Chati Na.7 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 7** *Kufaulu kwa Watahiniwa Kiasilimia*

Uchambuzi unaonesha kuwa, asilimia 95.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 12 hadi 19. Kati yao asilimia 23.5 walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kutokana na kujibu kulingana na matakwa ya swali. Wengi walitoa hoja za kuigwa kama vile: *ushiriki katika shughuli mbalimbali, kujitoa mhanga, kukubali uongozi, kuwa na elimu, umoja na mshikamano, ujasiri na uzalendo,* pia, walitoa hoja za kutoigwa kama vile: *uongozi mbaya, dhuluma, udikteta, rushwa na Imani potofu*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kuonesha mambo mawili yanayofaa kuigwa katika fasihi kama vile: *Kujitoa muhanga* na kufanya mageuzi kwa mhusika Mtolewa katika tamthiliya ya "Kivuli Kinaishi" na katika tamthiliya ya "Morani" alieleza mambo mawili yanayofaa kuigwa kama vile: *ujasiri na umoja na mshikamano* kwa kumtumia mhusika Jalia. Kwa upande wa mambo yasiyofaa kuigwa alieleza mambo kama vile, *Rushwa na uongozi mbaya* kwa kumtumia mhusika Bi Kirembwe katika kitabu cha **Kivuli kinaishi** na katika tamthiliya ya **Morani** alieleza mambo kama vile; *Usaliti na uhujumu uchumi* akimtaja mhusika Nungunungu. Kielelezo 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

7 Mambo yanayofaa kuigwa ni yale mambo mazuri yanayofanywa na wahusika ili kuhakikisha maendeleo yanapatikana. Mambo yasiyofaa ni yale mabaya yanayofanywa na wahusika ambayo inabidi tusiyaige ili tuwe na maendeleo katika jamii. Yatupasa tuyaige yale mambo mazuri na yale mambo mabaya tuyaepuke na tuyapinge. Kwa kutumia tamthiliya ya "KIVULI KINAISHI" iliyoandikwa na Said Mohamed na "MORANI" iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo kuna mambo yanayofaa kuigwa na mambo yasiyofaa kuigwa. Katika tamthiliya ya "KIVULI KINAISHI" mambo yanayofaa kuigwa ni

Kujitoa mhanga; kujitoa mhanga ni mtu kuwa tayari na lolote litakalokupata ili kuikomboa jamii kutokana na matatizo yanayoikumba jamii. Katika tamthiliya ya Kivuli Kinaishi, Mtolewa alijitoa mhanga katika kupinga uongozi mbaya unaofanywa na Bibi Kirembwe. Bi Kirembwe alijitangazia kuwa ni mtawala wa milele na alikuwa asikilizi maoni ya raia wake. Mtolewa hata kama alisomeshwa bado alijitoa mhanga kumwambia ukweli Bi Kirembwe. Matokeo yake Mtolewa aliweza kupambana na Bi Kirembwe. Hata katika jamii yatupasa tuwe wahu wa kujitoa mhanga bila kuogopa kitu chochote.

Kufanya mageuzi; kufanya mageuzi ni kitendo cha kufanya kila linalowezekana kufanya mapinduzi kwa kitu fulani. Mtolewa aliweza kufanya mageuzi kwa kuwalisha unga wa rutuba wale wari. Mwandishi anaposema

"Hamtoweza kufahamu mpaka niwafueni mazigo mlizo nao... Hamtatambua mpaka niwafumbueni macho na kuwazibueni masikio".

7 Kutokana na mawazo ya kimapinduzi aliyoyapandikiza kwa wari na viozi vingine ilipelekea kupanyua kwa mapinduzi Gningi. Baadaye wale wazee nao walimsaliti na viungo vyake vya mwili vilimsaliti Bi Kirembwe. Hata katika jamii mapinduzi ni kitu cha muhimu ili kufikia maendeleo. Mambo yasiyofaa kuigwa ni

Rushwa; ni kitendo kisicho cha haki cha kupokea na kutoa kitu ili upate kitu kingine. Katika serikali ya Gningi rushwa ilikuwa imekithiri. Bawabu wa pili aliomba rushwa kwa Mtolewa. Mwandishi anaonesha

"Bawabu wa II aliomba rushwa ya shilingi elfu 5000/= ndipo alimruhusu Mtolewa kuingia lango la Gningi."

Hata katika jamii wapo wapenda rushwa. Rushwa haifai kuigwa hata kidogo, tuachane nayo.

Uongozi mbaya; uongozi mbaya ni kitendo cha kuongoza kwa matakwa yako. Tunaona Bi Kirembwe alikuwa anaongoza kidikteta bila kujali au kusikiliza raia wake. Alijitangazia madaraka ya milele. Pale mwandishi anaposema

"Mimi ndiye mwenye kutahiki kukalia kiti hiki daima"

Uongozi mbaya haufai kuigwa katika jamii yoyote kwani ni chanzo cha umaskini na kutoendelea katika jamii. Kwa kutumia tamthiliya ya "MORANI" mambo yanayopaswa kuigwa ni

Umoja na mshikamano; umoja na mshikamano ni ushirikiano ili kuondoa jambo fulani. Katika tamthiliya hii tunawaona Dongo, Hadikwa, Mapoto na Malongo wanashirikiana ili kuwatokomeza wahujumu uchumi. Jalia, Dongo na wenzake wanashirikiana katika zoezi la

7 Kuwasaka wahujumu uchumi. Umoja na mshikamano ni kitu muhimu na kinachohitajika kwani waliweza kupata majina ya wahujumu uchumi. Katika jamii lazima tujenge umoja na mshikamano ili tujenge jamii yetu.

Ujasiri; ujasiri ni kitendo cha kufanya jambo bila kuogopa utanala wowote au mtu yeyote ili kuleta maendeleo. Katika tamthiliya hii tunamuona Jalia ijapokuwa alikuwa ni mwanamke lakini alikuwa haogopi kusema ukweli. Aliweza kumfuata Nungunungu na kumwambia ukweli kuwa anajihusisha na uhujumu uchumi. Pia aliweza kumfuata Yusufu na Mlemeta pale Jalia anapowaambia

"Unadhani sijui kama mmenunuliwa na Nungunungu. Katika jamii yoyote lazima kuwepo na watu wajasiri wasioogopa kitu chochote ili kuwe na maendeleo.

Mambo ambayo hayafai kuigwa ni

Usaliti; ni kitendo cha kwenda kinyume na makubaliano. Yusufu na Mlemeta walikuwa wapo katika msafara wa kuwapinga wahujumu uchumi, lakini Yusufu na Mlemeta walikuwa wakishirikiana na Mhujumu uchumi Nungunungu Taarifa zote walikuwa wanampelekea Nungunungu hata ilifika wakati Nungunungu anawaagiza Yusufu na Mlemeta wamtafutie wakili kwaajili ya kushinda kesi na alishinda. Usaliti ni kikwazo katika maendeleo yoyote. Hivyo jamii haipaswi kuwa na wasaliti.

Uhujumu uchumi; ni kitendo cha kutumia mali za umma kwa kujinufaisha wewe mwenyewe. Nungunungu aliweza kufanya Hujuma kwa kujinufaisha yeye mwenyewe.

7/ Pale Jalia anapowaambia Yusufu na Mkomota "Mnafahamu Nungunungu anavusha Karafuu na Kahawa nje ya nchi kwa magendo huwemi sawa.. ana hoteli kubwa marekani na akaunti uswisi." Nungunungu alikuwa ni mhujumu uchumi. Hivyo katika jamii lazima tupige vita wahujumu uchumi.

Kwahiyo; mambo mazuri tukiyaiga lazima jamii itakuwa na maendeleo makubwa na yale mambo mabaya lazima tuyaepuke kwani mambo mabaya ndiyo huyelekea Kuzorota kwa maendeleo katika jamii yoyote ile. Maendeleo mazuri yanaletwa na mwanajamii mwenyewe.

**Kielelezo 7.1**: Mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Kielelezo 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kufafanua hoja mbili za kufaa kuigwa na hoja mbili za kutofaa kuigwa kwa fasihi na kupata alama za juu.

Hata hivyo, asilimia 4.4 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kutokuwa na maarifa na uelewa wa kutosha kuhusu mambo yanayofaa na yasiyofaa kuigwa katika fasihi, waliweza kuonesha baadhi tu ya mambo yanayofaa kuigwa. Wengi walitoa hoja za kuigwa na za kutoigwa lakini walishindwa kuelezea hoja hizo ipasavyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua mambo yanayofaa na yasiyofaa kuigwa bila kutolea mifano kutoka kwenye vitabu kama swali lilivyomtaka. Pia hakuandika kabisa utangulizi. Kielelezo 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

7 Morani ni Tamthiliya iliyoandikwa na mwandishi Emmanuel Mbogo katika kuonesha mambo yanayofaa kuigwa na yasiofaa kuigwa. Mambo yanayofaa kuigwa ni pamoja na

Ushirikiano katika jamii: Mwandishi ameeleza kuwa ili jamii yoyote ipate maendeleo lazima watu wake washirikiane kikamilifu katika shida na raha.


Kujituma katika kazi: Mwandishi ametaja kuwa ili maendeleo yapatikane lazima watu wote wafanye kazi kwa bidii na ufanisi. Kujituma au kufanya kazi kwa bidii ndiyo ufanisi mzuri wa maendeleo.

Vilevile mwandishi ametaja mambo yasiyofaa kuigwa na jamii kama ifuatavyo

Wizi: Mwandishi ametaja kuwa wizi haufai katika jamii yoyote ile kwani inadumaza maendeleo kwa yule aliyetafuta mali hiyo. Vilevile inapelekea mtu kupoteza maisha kwani anaweza kufungwa au kuuawa na watu wenye hasira kali.

Uvivu: Mwandishi ametaja kuwa umaskini ni mzigo katika jamii kwani hutokana na watu kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi mzuri. Hivyo haufai kuigwa na jamii yoyote ile.

Ngoswe mama naiyo ni Tamthiliya iliyoandikwa na mwandishi Penina Mlama ikionesha mambo yanayofaa na yasiofaa kuigwa na jamii kama ifuatavyo


7 Mambo yanayofaa kuigwa na jamii yoyote ile ni pamoja na
Utu wema: Mwandishi ametaja kuwa ili jamii yoyote ile iendelee lazima utu uwepo kwa watu wote kwani hupelekea jamii kuwa na upendo, Amani na furaha kwa watu wote.
Uongozi mzuri: Hapa mwandishi ametaja jinsi viongozi wazuri wanavyoleta maendeleo mazuri, kwa kushirikiana na wananchi. Kuna baadhi ya viongozi hufanya kazi zao vizuri kwa kushirikisha jamii yao.
Pamoja na mambo hayo mwandishi amefafanua tena mambo yasiyofaa kuigwa na jamii kama ifuatavyo
Shuruma: Mwandishi ametaja kuwa Shuruma ya kunyang'wanyang'wa mali haifai katika jamii kwani kupelekea utu kuwa mtumwa katika jamii hiyo. Hivyo haifai kuigwa na jamii
Unafiki au umbea: Suala hili nalo mwandishi amelikemea kuwa halifai kuigwa na jamii kwani linapelekea watu kupigana au kuchukiana vilevile linakwamisha maendeleo katika jamii.
Hizo hapo juu ndiyo masuala au mambo yanayofaa kuigwa na jamii katika kuleta maendeleo mfano uongozi mzuri, ushirikiano, utu wema na kujituma katika kazi. Vilevile mambo yasiyofaa ni kama vile wizi, Shuruma, unafiki na uvivu. Haya hayafai kuigwa.

**Kielelezo 7.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua kwa mifano hoja alizotoa hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa wachache, asilimia 0.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kwani walishindwa kuonesha mambo mawili yanayofaa na mawili yasiyofaa kuigwa katika fasihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua mambo yanayofaa na yasiyofaa kwa kufafanua vipengele vya fani kama vile: *Uteuzi mzuri wa mandhari, matumizi mazuri ya lugha, matumizi mengi ya taswira na kutowekwa kwa masuluhisho kwa baadhi ya matatizo* ambayo yalikuwa kinyume kabisa na matakwa ya swali. Kielelezo 7.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili na kupata alama hafifu.

7. Mambo yanayofaa kuigwa ni kitu amba-
cho mtu hufanya kutoka kwa mtu mwingine
na kumletea manufaa. Mambo yasiyofaa kuig-
wa ni mambo ambayo mtu huiga kuto-
ka kwa mtu mwingine na hayana msingi
~~Kwa~~ ~~Kuanz~~ Yafuatayo ni mambo yana-
yofaa kuigwa katika fasihi kutoka katika
~~Tamthiya~~ ya MORANI iliyoandikwa na EMMANUEL
MBOGO pia KIVULI KINAISHI iliyoandikwa na
SAIDI MOHAMED.
Uteuzi mzuri wa mandhari, moja
kati ya mambo ambayo fasihi inatakiwa
kuiga kutoka katika fasihi ni uteuzi
mzuri wa mandhari, wahusika na vitu amba-
vyo vimejadiliwa. Uteuzi mzuri wa mndhari
wahusika ni vitu ambayo vinafaa katika
fasihi kuigwa ili kuipa muonekano
mzuri na welevu kwa hadhira.
Matumizi mazuri ya lugha, iliyosheheni
misemo, nahau, methali na taswira ambayo
imesaidia kupamba kazi ya fasihi na
ujumbe kuweza kufika katika jamii.
Matumizi mazuri ya vitu hivyo husaidi-
a kufikisha ujumbe kwa wepesi. Yafuatayo
ni mambo yasiyofaa kuigwa na fasihi
katika riwaya ya MORAM ~~na~~ KIVULI KINAISHI
Kutowekwa kwa masuluhuhisho
kwa baadhi ya matatizo, fasihi haifai
kuiga hili mfano katika KIVULI KINAISHI
suala la imani za kishirikina, na uongozi
mbaya halijaoneshwa suluhisho na kuone-
sha Bi Kirebwe kuendelea tu kupambana nao

7. wale ambao wanampinga kutokana na uongozi wake mbaya ~~kupata~~ adhabu kali ata kuwatia ulemavu wa maisha.

Matumizi mengi ya taswira ni moja ya mambo ambayo fasihi hafai kuiga kwa kuwa inaleta kutoeleweka kwa hadhira matumizi ya taswira yazizidi kuwa mengi mfano katika tamthiliya ya "KIVULI KINAISHI"

Hivyo basi, fasihi ilitakiwa kuiga hayo kutoka katika tamthiliya hizo na kutoiga hayo pia fasihi inatakiwa kuwa huru ili kutoa uozo ambao unaizunguka jamii bila kuogopea au kuhofia jambo fulani.


**Kielelezo 7.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 7.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa kufafanua vipengele vya fani badala ya kuonesha mambo yanayofaa na yasiyofaa kuigwa katika fasihi hivyo kupata alama hafifu.

### 3.5.2 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali lilitoka katika mada ya Fasihi Andishi na lilihusu uhakiki wa vitabu teule vya tamthiliya. Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua wasifu wa wahusika wawili kwa kuwalinganisha na wazo kuu la waandishi wa vitabu hivyo. Swali lililenga kupima tathmini na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilikuwa la kuchagua na lilijibiwa na watahiniwa wachache (asilimia 6.2). Swali hili lilijibiwa vizuri ambapo asilimia 98.1 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 8**: *Kufaulu kwa Watahiniwa Kiasilimia*

Watahiniwa asilimia 86.1, walipata alama kuanzia 12 hadi 19. Miongoni mwao, asilimia 19.2, walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya wasifu wa wahusika kwa kulinganisha na mawazo makuu ya waandishi wa vitabu husika. Wengi wao walifafanua wasifu kama vile: *kupenda demokrasia, kufichua maovu, kuwa na elimu ya kutosha, uzalendo, kupiga vita uhujumu uchumi, ujasiri na umoja na mshikamano*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua wasifu wa wahusika kwa kulinganisha na mawazo ya waandishi wa vitabu kama vile, katika tamthiliya ya "Kivuli Kinaishi" alimtumia mhusika "Mtolewa" kwa kutoa hoja nne kuwa "*alikuwa mwanamapinduzi, ana msimamo, alikuwa jasiri na alikuwa mvumilivu"* na katika tamhiliya ya "Morani" alieleza wasifu wa mhusika Dongo kama vile" *mwanamapinduzi, mvumilivu na mwenye msimamo* hivyo, kupata alama za juu. Kielelezo 8.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufafanua wasifu wa wahusika na kulinganisha na wazo kuu la mwandishi.

8. Mhusika ni mtu au kiumbe ambaye anatumika kueleza jambo fulani katika kazi ya fasihi. Mhusika huweza kuwa halisi au siyo halisi kutokana na jinsi mwandishi alivyotaka kuipamba kazi yake kwa mfano huweza kutumia wazimwi na miungu kukamilisha kazi yake. Kwa kutumia Tamthiliya ya MORANI iliyoandikwa na "Emmanuel Mbogo" na "KIVULI KINAISHI" iliyoandikwa na "Said Mohamed" waandishi wametumia wahusika kama ifuatavyo, kwa kuanza na KIVULI KINAISHI mhusika "mtolewa" amechorwa kama ifuatavyo :-

Mwana mapinduzi ; mwandishi amemtumia mhusika "mtolewa" kama mwanamapinduzi ambaye alikuwa anapinga uongozi mbaya uliokuwa wa kimabavu chini ya "Bi kirembwe" ambaye alitawala kwa nguvu zake mwenyewe pasipohitaji mtu yeyote aweze kumsaidia katika uongozi wake.

Ana msimamo ; mwandishi amemtumia "Mtolewa" kama mtu mwenye msimamo na lile jambo ambalo amekilisubiria kulitenda na kulifanya kukamilika mtoto alipokuwa akipinga utawala mbaya wa Bi kirembwe na aliweza kukutana na changamoto nyingi ambazo zingemrudisha nyuma lakini alikuwa na msimamo mpaka mwisho wa uhai wake.

Alikuwa jasiri ; mwandishi amemtumia "Mtolewa" kama mtu jasiri ambaye hakuogopa kitu chochote mbele yake ambacho kingemfanya kurudi nyuma katika harakati za kupinga uongozi mbaya wa Bi kirembwe


8\. na kuweza kumtokomeza kabisa utawala huo mbaya uliotumia nguvu ili kuweza kutawala na kuongoza watu.

Alikuwa mvumilivu ; mwandishi amemchora "mtolewa" kama alikuwa mvumilivu kwa mambo yote magumu aliyoyapitia katika kutoa ngoma mbaya na Bi Korembe ikiwemo kutupishwa mshua na Bawabu na kuanza na kuweza kufanyiwa unyanyasaji mkubwa na Bi Korembe lakini alivumilia yote. Pia katika tamthiliya ya MORANI "mwandishi amemtumia mhusika "Dongo" kama ifuatavyo :-

Alikuwa mwana mapinduzi ; mwandishi ~~ata~~ amemtumia "Dongo" kama alikuwa mwana mapinduzi katika kitabu hiki kwa sababu alikuwa alipinga uhujumu uchumi uliokuwa unafanywa na Mungumungu katika jamii na aliweza kupigana na suala hili mpaka mwisho wa uhai wake.

Alikuwa mvumilivu ; mwandishi amemtumia mhusika "Dongo" kama alikuwa mvumilivu kwa mambo yote magumu aliyoyapata wakati wa kupinga uhujumu uchumi ikiwemo mshua ambayo ilitolewa na baka-mavi walipotaka kumtunga "Mungumungu" kushtakiwa na kuhujumu uchumi.

Alikuwa na msimamo ; mwandishi amemtumia "Dongo" kama alikuwa na msimamo juu ya mambo aliyokuwa akiyapata ya mtanzania katika suala la kupinga wahujumu uchumi aliweza kusimama ili kuhakikisha suala hili linakomeshwa katika jamii yetu na



8: Inapendekeza kabisa kwa kupigana vita vikali ili
kuweze kupatikana katika jamii zetu. .
Ablunuwa jasiri ; mwandishi amem
chora "Dongo" kuwa ablunuwa jasiri kwa
sababu alijitoa mhanga kufa au kupona ili
kuweza kupiga vita uhujumu uchumi ambao
o Ablunuwa alishirikiana na Mungurungu na
kuweza kuleta usawa katika jamii ili kuwepo
na demokrasia ya kweli na amani katika
jamii zetu.
Mwandishi ametumia wahusika
hawa katika kazi zao ili kuonesha wasifu wao
katika jamii na katika vitabu kwa sababu
kutokana na wasifu wao hivyo maana tunapa
ta dhamira mbalimbali mfano : Suala la
uongozi mbaya , usaliti , dhuluma , migog
oro , rushwa na umaskini

**Kielelezo 8.1**: Mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Kielelezo 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili vizuri na kupata alama za juu.

Aidha, asilimia 12.8 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya hoja. Watahiniwa hawa walichanganya wahusika wa tamthiliya na kuwapeleka kwenye riwaya, walishindwa kufafanua baadhi ya wasifu wa wahusika na pia walitoa wasifu ambao wahusika hawana. Katika tamthiliya ya "Morani" mtahiniwa mmoja alimtaja mhusika *Dania* ambaye ni mhusika katika riwaya ya Mfadhili na katika tamthiliya ya "Kivuli Kinaishi" alimtumia mhusika Mtolewa kuwa *aliwalisha wari unga wa ndele*

wakati aliwalisha *unga wa rutuba* na alieleza hoja kuwa Mtolewa ni mpiganaji anayepatikana katika riwaya hii wakati yumo katika tamthiliya ya Kivuli Kinaishi. Kielelezo 8.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.



08. Wahusika ni washiriki wa kazi ya
fasihi ambao hubeba dhamira kuu ili kupi-
kisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Kwa
kutumia tamthiliya mbili MORANI iliyoandikwa
na EMMANUEL MBOGO na kumtumia mhusika
Dongo na tamthiliya ya KIVULI KINAISHI
iliyoandikwa na SAID MOHAMED na kumtumia
mhusika Mtolewa kwa lengo la kuwaelezea —

08. wasifu wao na wazo kuu la mwandishi.

Kwa kuanza na MORANI kwa kumtumia mhusika Dongo kuonesha yafuatayo.

Dongo ni mwanamapinduzi. Mhusika huyu amejitahidi katika kuunganisha wananchi katika suala la kuondoa uongozi mbaya ~~ya~~ wa serikali ya Nungunungu kwa sababu viongozi walishindwa kuleta maendeleo. Hivyo basi, kupitia wasifu wake kama Mwanamapinduzi ametoa wazo la mwandishi la kujitoa mhanga.

Dongo ni mpinga rushwa. Mhusika huyu pia alikuwa anachukia masuala ya rushwa akishirikiana na Dania. Hivyo kutokana na wasifu wake ameibua dhana ya rushwa katika kazi hii ya fasihi.

Dongo ni mpenda maendeleo. Mhusika huyu ilifikia wakati alikuwa akinung'unika na kutoa machozi kuhusu jamii yake. Hivyo kupitia wasifu wake ameibua suala la maendeleo ndani ya jamii.

Dongo pia, ni Mchapakazi. Mhusika huyu pia aliweza kuchunguza ~~wa~~ viongozi wote ambao wanakula rushwa ~~hat~~ hadi kuandaa orodha ambayo iliwezesha kuwakamata wahalifu. Hivyo kutokana na wasifu wake dhamira ya ufanisi katika kazi imeibuliwa.

Kwa kumalizia na tamthiliya ya KIVULI KINAISHI kwa kumtumia mhusika Mtolewa.

Mtolewa alikuwa msomi na mwenye elimu. Mhusika huyu alitumia elimu yake vizuri katika maisha yake na ameweza kuitumia elimu hiyo kwa kumwaga unga-

→

08. wa ndele kwa wari ndani ya Giningi. Hivyo-
kupitia uhusika wake anaibua wazo kuu
la umuhimu wa elimu ndani ya jamii.

Mtolewa ni mpiganaji. Mhusika huyu
ameonesha juhudi zake zote katika kuleta
mabadiliko chanya ndani ya Giningi chini ya
Kiongozi Bi Kirembwe. Hivyo basi, kujitoa
mhanga ndio wazo lililojengwa kwenye riwaya
hii kupitia mhusika Mtolewa.

Mtolewa anachukia ukale ndani ya
jamii. Kwa sababu aliamua kuvunja uchawi,
na utamaduni mbaya ambao uliwafanya
Wanaginingi kuonekana wajinga mbele ya
Kiongozi wao Bi Kirembwe. Hivyo mhusika
huyu ~~atw~~ ameweza kuvunja utamaduni kwa
kujenga dhamira ya utamaduni.


Mwanamapinduzi. Mtolewa ni mwana-
mapinduzi kwa sababu alikuja ndani ya
Giningi lakini wari na wananchi wote
waliweza kutambua ubaya wa Bi-Kirembwe
na serikali yake. Hivyo kutokana na wahusika
hao mwangaza ndani ya jamii ya Giningi
ulipatikana.

Hivyo basi, wahusika ni nyenzo kuu
katika kuibua dhamira na ujumbe uliokusudiwa na mwandishi katika kazi yake ya
fasihi.

**Kielelezo 8.2:** Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kuwachanganya wahusika wa riwaya.

Hata hivyo, asilimia 1.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kukosa uelewa kuhusu wasifu wa wahusika. Watahiniwa katika kundi hili waliweza kuchagua wahusika lakini walishindwa kuwaelezea na wengine walichanganya wahusika wa vitabu hivyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya mhusika “Mtolewa” kwamba yumo katika tamthiliya ya “Morani” wakati yumo katika tamthiliya ya “Kivuli Kinaishi” na katika tamthiliya ya “Nguzo Mama” alimtumia mhusika “Chizi” na alitoa maelezo yasiyoonesha wasifu wa mhusika huyo. Kielelezo 8.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.



08 Wahusika, Hawa ni watu au viumbe wanaotumiwa kubeba tabia za watu fulani katika jamii, ambao hu-mba kazi ya fasihi. Kwa kutumia m-husika 'Chizi' wa tamthiliya ya ~~Kivu~~ ~~li Ki~~ NGUZO MAMA na mhusika 'Mtole-wa' wa tamthiliya ya MORANI iliyo-andikwa na Emmanuel Mbogo. katika ku-eleza wasifu wao kulinganisha na wazo kuu la mwandishi.

Kwa kuanza na tamthiliya ya MORANI kutumia mhusika 'Mtolewa':

Mtolewa alianza kuachana na shughuli ya kutengeneza vodka ya wahujumu uchumi wa nchi. Kutokana na kwamba alipowa posa na Ngurumo ni waraka wa wandiko kwenye vodha. Hivyo wazo kuu la mwandishi ni usaliti wa mtolewa kwa akina Idia, Mapoto, Malongo na wengineo.

Mtolewa alikuwa hana elimu ya kutosha, kutokana na hali yake ya ukosefu wa elimu inampelekea kupokea posa ambazo zinapeleka kukwamisha maendeleo ya nchi zima. Hivyo wazo kuu la mwandishi na ukosefu wa elimu. Laiti mtolewa angekuwa anaelimiko vizuri asingekubali kulaghaiwa na posa.

08. Mtolewa alianua kushirikiana na Nungunungu, si yeye peke yake bali pia na Yusuph walianuo kuwunga mkono Nungunungu kutokana na pesa walizopewa. Hivyo wazo kuu la mwandishi ni Uhujumu uchumi. Kwani Mtolewa naye alianza kufanya kazi na Nungunungu kutoka kuhujumu uchumi wa nchi. Kwani Nungunungu alikuwa ni mtu mwenye pesa sana. Jalia anasema:

"...Mtolewa hivi unajua kuwa Nungunungu anahoteli kubwa huko Marekani na akaunti za fedha uswizi..."

Mtolewa pia anaonekana akikubali vijipesa vinavyopelekea kudumaza maendeleo ya nchi. Hivyo wazo kuu la mwandishi ni Rushwa. Nungunungu anampatia Mtolewa Rushwa pamoja na Yusuph ili washirikiane na akina Dengo, Jalia na wengineo. Ambao walikuwa wakifanya kazi za kutengeneza orodha ya wahujumu uchumi. Tunamwona Jalia akisema:

"Mtolewa kama umenunuliwa, sio mimi..."

Kufuatiwa na fauthiliya ya NGUZO MAMA iliyoandikwa na Penina Muhando; kwa kumtumia mhusika 'Chizi' kueleza wasifu wake na wazo kuu la mwandishi.

Chizi alikuwa akieleza


08 kama watu walikuwa wakimuita 'Oh my god' yenye maana ya chizi. Hali hii inaonyesha namna gani chizi hajaeleweka. Hivyo ni wazo la mwandishi ni ukosefu wa Elimu. Kwani neno 'Oh my god' ni neno la kiingereza lenye maana tofauti na ambayo chizi anaelewa.

Chizi ni mtu anayeishi maisha magumu pasipo msaada kutoka kwa ndugu yake Bi Tafu licha ya kuwa mwenyekiti. Hivyo wazo la mwandishi ni umaskini. Kwani Tafafa yote inatambua na tatizo la umaskini na chizi ni moja ya watu wanaokabiliwa na tatizo hilo.

Pia chizi anajaribu kuuliza kuhusiana na Nguzo mama ila viongozi husita, pia wanaanaeleza kuto kufahamu Nguzo mama ni nini. Hivyo kuibua wazo kuu la mwandishi la uongozi mbaya. Tunaona wazi chizi akimuuliza Bi Msaba kuhusu Nguzo mama na Bi Msaba akajibu,

"...mwanangu hata mimi
sijui kabla muulize Bi mse"

Chizi pia anaonekana ni mtu mzima ila hana maendeleo yoyote kwenye maisha yake. Hivyo anaibua wazo kuu la mwandishi la Uvivu. Chizi ni mvivu kwani anasubiria kusaidiwa na viongozi yake. Badala afikirie njia ya kupikuana mwenyewe kimaendeleo. Uvivu unadanga kudumaza maendeleo.


08 Hivyo basi, Waandishi wa tamthilia-
ya hizi mbili wamefanikiwa kuonesha wasifu
mbalimbali wa wahusika waliowatumia pa-
moja na mawazo yao makuu yanayoelezewa
na wasifu wa wahusika hao.

**Kielelezo 8.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 8.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya kwa kuchanganya wahusika na vitabu na kushindwa kufafanua wasifu wao.


## 3.6 SEHEMU E: USANIFU WA MAANDISHI

Sehemu hii ilikuwa na swali moja ambalo lilimtaka mtahiniwa kuonesha uwezo na umahiri katika kusoma kifungu cha habari na kuonesha mbinu za kifani zilizotumika.

### 3.6.1 Swali la 9: Usanifu wa Maandishi

Swali lilitoka katika mada ya Usanifu wa Maandishi na lililenga kupima Uchambuzi. Swali lilikuwa na alama 20.

Swali hili lilikuwa la lazima, hivyo watahiniwa wote 21783 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili.Watahiniwa wengi walipata alama za juu na za wastani. Chati Na. 9 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 9**: *Kufaulu kwa Watahiniwa Kiasilimia*

Asilimia 49.1 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5. Watahiniwa hao walieleza baadhi ya mbinu anuai za kifani zilizotumika katika matini kwa usahihi na kushindwa kubaini mbinu nyingine za kisanaa. Watahiniwa waliweza kutaja mbinu kama vile: *Muundo, mtindo, wahusika, mandhari, matumizi ya lugha (tamathali za semi, misemo, nahau, methali na matumizi ya lugha ya kiingereza)* na mbinu nyingine za kisanaa kama vile: *Mdokezo, tashihisi, tashbiha, sitiari na takriri*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alipata alama za wastani kutokana na kujibu kwa usahihi baadhi ya mbinu za kifani na kukosa zingine kama vile; katika matumizi ya lugha kipengele cha tamathali za semi alitaja tamathali za semi kama: *Mdokezo, tashihisi, tashbiha na sitiari* ambapo alitoa mifano ya tamathali hizo isiyo sahihi na katika lugha ya mtaani alitoa mifano ambayo si lugha ya mtaani hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 9.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata baadhi ya vipengele vya kifani na kupata alama za wastani.

| | |
|---|---|
| 09. | (i) Muundo- Mwandishi ametumia Muundo wa moja kwa moja kwani visa na Matukio vimepangiliwa |
| | (ii) Mtindo- Katika mtindo Mwandishi amefanikiwa kutumia mitindo Mbalimbali ambayo imejenga kazi yake. Mitindo hiyo ni; |
| | @ Matumizi ya nafsi, Mwandishi ametumia nafsi mbalimbali kama vile nafsi ya |

| | |
|---|---|
| 09. | Kwanza umoja alipo sema, Nikamjibu |
| | (iii) Wahusika, Mwandishi wa Matini hii ameweza kutumia wahusika binadamu ambao ni Lenadi, Kishefu, Mahewa na pia ametumia wahusika ambao sio binadamu kama vile paka. |
| | (iv) Mandhari, Mwandishi ametumia Mandhari ya kubuni ambayo ni Mandhari ya sehemu za starehe kwamfano katika baa ziitwayo WANYEJANDA. |
| | (v) Matumizi ya lugha, Lugha iliyotumika katika matini hii ni nyepesi na yenye kueleweka kwa wasomaji. Lugha hii ndani yake imejaa vitu vifuatavyo |
| | @ Nahau, kwa mfano Mkono wa birika ambao unamaanisha uchoyo. |
| | (b) Misemo, kwa mfano Dunia kila mtu anapambana na hali yake. |
| | © Matumizi ya tamathali za semo ambazo ni |
| | (i) Mdokezo kwa mfano; Ah.... Ahaaaa.... aaa! |
| | (ii) Tashihisi kwa mfano Viongozi wapenda rushwa wapo roho juu. |
| | (iii) Tashibiha kwa mfano Moja Moto moja baridi |

09. iv) Sitiari Kwa Mfano
Mara kwa Mara
Moja baridi na nyama choma
Ikanipara niwasogelee kwa karibu

v) Matumizi ya lugha za mtaani
Kwa mfano Masineki, Moja moto
moja baridi na nyama choma

vi) Matumizi ya lugha za kigeni
Kwa mfano lugha ya kingereza kwa
kuwepo na maneno kama Thank you
wife, brother

vii) Matumizi ya nyimbo
Kwa mfano,
Wakati wa ujana wetu, mimi baba yenu,
Shati dukani shilingi sita unapata
Lakini sasa shilingi sita hata mkate
hupati!
Kwa hiyo Mwanguduishi kufuatana na
wakati x2 (Kibwagizo)

09. iv) Sitiari Kwa Mfano
Mara kwa Mara
Moja baridi na nyama choma
Ikanipara niwasogelee kwa karibu

v) Matumizi ya lugha za mtaani
Kwa mfano Masineki, Moja moto
moja baridi na nyama choma

vi) Matumizi ya Lugha za kigeni
Kwa mfano lugha ya kingereza kwa
kuwepo na maneno kama Thank you
wife, brother


vii) Matumizi ya nyimbo
Kwa mfano,
Wakati wa ujana wetu, mimi baba yeny
Shati dukani shilingi sita unapata
Lakini sasa shilingi sita hata mkate
hupati!
Kwa hiyo Mwangu tuishi kufuatana na
wakati x2 (kibwagizo)

**Kielelezo 9.1**: Mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

Kielelezo 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata baadhi ya vipengele vya kifani na kupata alama za wastani.

Aidha, asilimia 44.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri na kupata alama kuanzia 12 hadi 19. Miongoni mwao, asilimia 2.3, walipata alama za juu kuanzia 17 hadi 19 kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya vipengele vya fani vilivyotumika katika kifungu cha habari. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kujibu kwa usahihi kwa kuelezea mbinu za kifani zilizotumika kama vile: *Muundo, mtindo, wahusika, mandhari, matumizi ya lugha (tamathali za semi, misemo, nahau, methali* na *matumizi ya lugha ya kiingereza) na mbinu nyingine za kisanaa kama vile; tanakali sauti.*

Kielelezo 9.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuonesha na kufafanua kwa usahihi mbinu za kifani zilizotumika katika kifungu cha habari na kufaulu kwa kiwango kizuri.


9 Fani ni upande wa kisanii ambao unampa msanii ili kufikisha ujumbe kwa hadhira aliyo kusudiwa. Fani hujumuisha vipengele mbalimbali mfano Muundo, mtindo, wahusika Mandhari pamoja na Matumizi ya lugha. Zifuatazo ni mbinu mbalimbali zilizotumika katika habari hii

9 Muundo ni mpangilio wa visa na matukio katika kazi ya fasihi, katika hadithi hii msanii ametumia muundo wa moja kwa moja kwani anaeleza tukio kuanzia baa walipokuwa wakinywa pombe hadi wanapoondoka nyumbani kwa mteule.

Mtindo ni mbinu ya kipekee anayoitumia msanii ili kujitofautisha kati yake na msanii mwingine. Msanii ametumia mtindo wa masimulizi, taharuki, mtindo wa majibizano (dialojia) masimulizi ya nyimbo na masimulizi ya nafsi zote tatu (mimi) (wao) na (yeye).

Wahusika ni vitu, watu au wanyama wanaohusika katika kazi ya fasihi katika hadithi hii msanii ametumia wahusika mfano. • Mahewa na kishepu hawa walikuwa ni marafiki wa Masineki waliokuwa wakinywa pombe katika baa ya WANYEJANJA

• Masineki ni jirani wa mhusika mkuu ambaye walikutana baa na kunywa pombe pamoja

• Mke wa mwendeshaji, huyu alikuwa ni mtu mbali kama pili pili pale alimwona amepo chelewa kurudi nyumbani

• Paka ni mnyama anayejulikana kwa lugo la kukamata panya ndani ya nyumba.

Mandhari ni mahali/sehemu kazi ya fasihi inapofanyika. Katika hadithi hii tunaona mandhari mbali mbali kama

9 na ni mandhari ya
• Baa ya WANYEJANJA hapa ni sehemu ambapo Masineka na rafiki zake Mahenk na kishefu hustarehekea kwa kunywa pombe.
• Nyumbani kwa mzanni, hapa ni mahali anapo ishi na mkewe kama familia
• Nyumbani kwa Masineka hapa ni sehemu anayo ishi masineka ambaye ni jirani na mzani.
• Matumizi ya lugha, lugha iliyo tumika na msanii ni rahisi na inayo eleweka, iliyo jaa methali, nahau na misemo pia Tamathali za semi na mbinu mbalimbali za kisanii.
• Tashihisi ni tamathali ya semi inayo vipa vitu visivyo binadamu hali ya kutenda kama binadamu mfano anaposema
– Meza yao ilikuwa ikitazama mato beo ya chupa za pombe ambazo zilikuwa zimenuna
• Takriri ni tamathali ya semi inayo onesha kurudia kwa neno, sentensi au kifungu cha maneno mfano
– kwa hiyo wanangu, tuishi kupatana na wakati x2 – Dunia ni tamu ni tamu mno
• Nidaa ni tamathali ya semi inayo onesha kushangazwa na kitu pia huambatana na alama ya mshangao mfano
– Myaau!
– Ah-- Aheaa --aaa!
– ni tamu mno!
– siamini!


9 • Mdokezo ni tamathali ya semi ambayo huonesha kuto maliza kwa maneno yaliyo engelewa na mhusika fulani Mfano
- Myaau... Myaau... Myaau
- Ah... Aheaa... aa

• Tanakali sauti (viigizi) hii ni tamathali ya semi inayo onesha maneno yaliyo tolewa na na uigaji wa sauti, umbo Mfano katika habari
- Ah... Ahaaa... aaa
- Myaauu... Myaau... myaau

• Matumizi ya misemo pia mwa ni ametumia misemo mbalimbali kwa lengo la kuelimisha jamii mfano kutoka katika habari
- Moja moto moja baridi (kupata mnyaji)
- Kupiga maji kwa wingi (kunywa pombe)
- Mfuko mkubwa umejaa mawe (fedha)
- Dunia ni tamu nitamu mno

• Matumizi ya nahau ambazo ni maneno mbalimbali yanayo tolewa na msanii kwa lengo la kuelimisha na kuburudisha jamii mfano kutoka katika habari
- Nimeshavaa mwani (kulewa pombe)
- Mkono wa birika (uchoyo)
- Ukwasi ni utajiri

• Matumizi ya lugha ya kiingereza, pia msanii ametumia lugha ya kingereza katika kuandika kazi yake hii mfano wa maneno ya kingereza ni
- Wife
- Thank you brother


9 Hivyo basi kwa kupitia vipengele ya fani tunaweza kupata dhamira mbali mbali zinazopatikana katika jamii zetu mfano umasikini, ulevi, kuto wajibika, mapenzi na ndoa na tunaweza kupata fanuthali za fani mfano [illegible] kutanya mambo mbalimbali yanayo elimisha jamii

**Kielelezo 9.2**: Mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Kielelezo 9.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuonesha na kufafanua kwa usahihi mbinu za kifani zilizotumika katika kifungu cha habari na kufaulu kwa kiwango kizuri.

Asilimia 6 ya watahiniwa walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kwa sababu hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mbinu za kifani hivyo kushindwa kuonesha mbinu hizo kama zilivyojitokeza katika matini aliyopewa. Wengi wao walijibu kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kuonesha mbinu za kifani kutoka katika matini aliyopewa kwa kuandika mbinu kama vile: *Matumizi ya fungua semi na funga semi, herufi kubwa, nukta, alama ya mshangao na nukta na mkato* ambayo hayakuwa majibu sahihi. Aidha, alitoa mbinu kama *mtindo na muundo* ambazo zilikuwa ni mbinu za kifani lakini maelezo aliyotoa hayakuhusiana na vipengele hivyo ingawa alipata mbinu moja ya matumizi ya nyimbo. Kielelezo 9.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

9 Mbinu za kifani. Ni mbinu ambazo mwandishi anazitumika katika kazi yake zitungo. Mtazo ni mbinu ~~za kifani~~ ambazo zimetumika katika matini

i) Matumizi ya fungua semi na funga semi, yameandikwa ndani ya matini kwa kuwa julisha maneno mbalimbali yaliyosemwa

ii) Matumizi ya ~~elfu~~ elufi kubwa, matumizi ya elufi kwabwa yametumika mwanzoni, ~~katika~~ mwa matini yametumika kwa kiasi kikubwa sana kupitia haya matini mfano neno kama Naa.

iii) Matumizi ya ~~kuuliza~~ alama ya kuuliza

iv) Matumizi ya Nyimbo, Katika matini hii matumizi ya nyimbo yamejitokeza katika sehemu mbali mbali

v) Matumizi ~~ya~~ ya nukta, katika matini hii matumizi ya nukta yametumika mwishoni mwa neno ~~ka~~ na katikati mwa neno

9. vi) Matumizi ya alama ya mshangao, Katika matini hii alama ya mshangao imetumika mwishoni mwa sentensi

vii) Matumizi ya nukta mkato, katika matini hii matumizi ya nukta mkato. yametumika katika katikati ya neno

viii) matumizi ya [illegible] ushairi, katika matini hii matumizi ya ushairi ambao umetumika

ix) Matumizi ya mtindo, Ni mtiririko-wa vina na mizani katika matini ili kufikisha ujumbe kwa jamii husika

x) Matumizi ya muundo, Ni mpangilio wa matukio katika Mwandishi ameyatumia ili kufikisha ujumbe.

**Kielelezo 9.3**: Mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

Kielelezo 9.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa kushindwa kukidhi matakwa ya swali.

## 4.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA

Uchambuzi wa takwimu za kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa 121 Kiswahili unaonesha kuwa, watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri katika mada zote kumi (11).

Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na kile cha mwaka 2018 kimeongezeka katika mada nyingi kama ifuatavyo: *Riwaya* (99.4%), *Maendeleo ya Kiswahili* (99.1%), *Usanifu wa Maandishi* (94.0%*), Tamthiliya* (99.25%), Matumizi ya Lugha (76.2), *Tafsiri na Ukalimani* (99.6%), *Fasihi kwa Ujumla* (81.75%), Matumizi ya Sarufi (82.1). na Ufahamu na ufupisho (97.8) Kwa mwaka 2018, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada hizo kilikuwa ni cha chini ambapo *Maendeleo ya Kiswahili* (92.0%), Matumizi ya Sarufi (68.4), *Usanifu wa Maandishi* (90.5%*), Tamthiliya* (89.8%), *Tafsiri na Ukalimani* (87.2%) na *Fasihi kwa Ujumla* (66.5%). Hata hivyo, kumekuwa na ongezeko la kufaulu kwa mada za *Tafsiri na Ukalimani* (99.6%) na *Utumizi wa Lugha* (76.2%) kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na kiwango kidogo cha kufaulu kwa mwaka 2018.

Aidha, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kwa mwaka 2019 kimepungua katika mada ya *Ushairi* (75.2%) *na Utungaji (98.3)* ikilinganishwa na mwaka 2018 ambapo kiwango cha kufaulu kwa mada ya Ushairi kilikuwa (99.1) na Utungaji kilikuwa (98.7). Pia kiwango cha kufaulu katika mada ya *Riwaya* kimekuwa sawa kwa miaka yote miwili (99.4). Ijapokuwa mwachano wa mada hizi kati ya mwaka 2018 na 2019 ni mdogo, mada ya *Ushairi* imekuwa na mwachano mkubwa zaidi kwani kiwango cha kufaulu kwa mwaka 2019 kimeshuka kwa asilimia 23.9 kikilinganishwa na kile cha mwaka 2018.

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada karibu zote kwa mwaka 2019 kilikuwa kizuri, hivyo, asilimia 100 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 35 katika mada zote. Kiwango hiki ni cha juu zaidi ikilinganishwa na kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kwa mwaka 2019 ambapo asilimia 99.97 walipata alama zaidi ya 35. Ongezeko hili ni asilimia 0.3% la kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada kwa mwaka 2019 linaonesha kuwa, watahiniwa wengi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa.

## 5.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika mtihani wa Kiswahili kwa mwaka 2019 kilikuwa kizuri ambapo asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walipata alama 35 au zaidi. Aidha kiwango kizuri cha kufaulu kimetokana na watahiniwa kuwa na ujuzi na uelewa wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa. Kiwango hiki cha kufaulu kwa watahiniwa kimekuwa na ongezeko la asilimia 0.3 ikilinganishwa na kufaulu kwa watahiniwa kwa mwaka 2018 ambapo wastani wa kiwango cha kufaulu kilikuwa 99.97.

Uchambuzi uliofanyika unaonesha changamoto mbalimbali za watahiniwa wachache walioshindwa kufanya vizuri kama vile: uelewa mdogo wa matakwa ya swali, mtiririko usiokidhi vigezo vya uandishi, uelewa mdogo wa mada mbalimbali na uwezo mdogo katika kujibu maswali. Kadhalika, watahiniwa hao walishindwa kutoa mifano sahihi na ya kutosha katika kujenga hoja za kujibu swali na kutokufuata maelekezo ya swali.

Mwisho, taarifa hii iwe changamoto katika kuwasaidia walimu na wanafunzi kuyaelewa makosa yanayosababisha watahiniwa wachache kutojibu vizuri maswali. Aidha, taarifa hii itakuwa na tija kwa walimu katika ufundishaji, utungaji na usahihishaji wa mitihani, na hivyo kuinua kiwango zaidi cha kufaulu kwa watahiniwa katika somo hili. Pia, taarifa hii italeta msukumo wa kujifunza kwa wanafunzi na hasa ikizingatiwa kuwa Kiswahili ni lugha inayotambulika na kutumika kitaifa na kimataifa ambapo kila mtahiniwa anapaswa awe na uwezo wa kujieleza vizuri, kujiamini na kujivunia lugha hii kama sehemu ya utamaduni wa mtanzania.

## 6.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi inapendekezwa kuwa:

(a) Katika ujifunzaji na ufundishaji wa mada zote: mbinu shirikishi itumike ikiwa ni pamoja na:

  (i) Ufundishaji na ujifunzaji wa mada zote upewe kipaumbele ili kuwawezesha wanafunzi kupata maarifa mahsusi katika mada mbalimbali.

  (ii) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kutosha katika mada zote ili kuongeza umahiri na weledi katika mada hizo.


(b) Walimu pamoja na wadau mbalimbali wa elimu kuendelea kuwatilia mkazo wanafunzi katika kujifunza mada zote ili kuinua kiwango cha kufaulu katika somo la Kiswahili.

**Kiambatisho A**

**ULINGANIFU WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2018 NA 2019**

| Na. | Mada | 2018 | | | 2019 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Idadi ya Maswali** | **Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Asilimia 35 au Zaidi** | **Maoni** | **Idadi ya Maswali** | **Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Asilimia 35 au Zaidi** | **Maoni** |
| 1. | Tafsiri na Ukalimani | 1 | 87.2 | Vizuri | 1 | 99.6 | Vizuri |
| 2. | Riwaya | 2 | 99.4 | Vizuri | 2 | 99.35 | vizuri |
| 3. | Tamthiliya | 2 | 89.8 | vizuri | 2 | 99.25 | vizuri |
| 4. | Maendeleo ya Kiswahili | 2 | 92.0 | vizuri | 2 | 99.1 | Vizuri |
| 5. | Utungaji | 1 | 98.7 | vizuri | 1 | 98.3 | Vizuri |
| 6. | Ufahamu na ufupisho | 2 | 93.4 | vizuri | 2 | 97.75 | Vizuri |
| 7. | Usanifu wa maandishi | 1 | 90.5 | vizuri | 1 | 94.0 | vizuri |
| 8. | Matumizi ya sarufi | 2 | 68.4 | vizuri | 3 | 82.1 | Vizuri |
| 9. | Fasihi kwa ujumla | 2 | 66.5 | vizuri | 2 | 81.75 | Vizuri |
| 10. | Utumizi wa lugha | 2 | 52.9 | wastani | 1 | 76.2 | Vizuri |
| 11. | Ushairi | 2 | 99.1 | vizuri | 3 | 75.15 | Vizuri |

**Kiambatisho B**




**ULINGANIFU WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2018 NA 2019**

